**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

# RIPOTI YA JUMLA YA UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUMU KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2019

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Machi 2019**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

**Dira**

Kuwa Taasisi ya Kuaminika na ya Kutukuka katika Ukaguzi wa Sekta ya Umma.

**Dhamiri**

Kutoa huduma za ukaguzi wa hesabu zenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia raslimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

**Uadilifu**

Kuwa taasisi adilifu inayotoa huduma bila upendeleo.

**Weledi**

Tunalenga kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu kwa kuzingatia taratibu bora.

**Uaminifu**

Tunahakikisha tunakuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.

**Mkazo kwa watu**

Tunalenga kufanikisha matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia wateja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.

**Uvumbuzi**

Kuwa taasisi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya taasisi

**Matumizi bora ya raslimali**

Kuwa taasisi inayothamini na kutumia kwa umakini mkubwa raslimali za umma ilizokabidhiwa.

| | JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA<br><br>OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI | |
|---|---|---|

Mtaa wa Samora , S.L.P. 9080, Dar es Salaam
Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Nukushi: 255(022)2117527, BaruaPepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kwa majibu tafadhali taja Kumb. Na.FA 27/249/33/2017/2018 28 Machi, 2019

Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli,
Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
1 Barabara ya Barack Obama,
**11400 Dar es Salaam.**

**Yah: KUWASILISHA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa Mwaka 2005) na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Umma Na. 11 ya Mwaka 2008, ninawasilisha kwako Ripoti yangu ya tisa ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu.

Ripoti hii inajumuisha ripoti sita za Ukaguzi wa Ufanisi pamoja na ripoti ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi katika Eneo la Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Ripoti hii ya jumla itawasilishwa katika kikao cha Bunge cha mwezi Aprili 2019.

Ninawasilisha.

Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

# YALIYOMO

YALIYOMO ............ I

ORODHA YA VIFUPISHO ............ IV

DIBAJI ............ V

SHUKRANI ............ VIII

MUHTASARI ............ X

HITIMISHO ............ XVI

SURA YA KWANZA ............ 18

UTANGULIZI ............ 18

1.1 USULI WA UKAGUZI ............ 18
1.2 MAMLAKA YA KUKAGUA ............ 18
1.3 MADHUMUNI YA RIPOTI ............ 19
1.3 LENGO KUU LA RIPOTI ............ 20
1.4 MCHAKATO WA UTHIBITISHO WA TAKWIMU ZILIZOTOLEWA KATIKA RIPOTI HII ............ 20
1.5 MUUNDO WA RIPOTI HII ............ 20

SURA YA PILI ............ 22

MFUMO WA USIMAMIZI WA MAENDELEO YA KILIMO NCHINI ............ 22

2.1 UTANGULIZI ............ 22
2.2 HISTORIA YA MAENDELEO YA KILIMO NCHINI TANZANIA ............ 23
2.3 MIKAKATI YA MAENDELEO YA KILIMO NCHINI ............ 24
2.4 MFUMO WA KISHERIA NA UDHIBITI ............ 26
2.5 MODELI YA MKAKATI WA MAENDELELO YA KILIMO NCHINI TANZANIA ............ 26
2.6 HAJA YA KUFANYA UKAGUZI KATIKA SEKTA YA KILIMO ............ 27
2.7 WATENDAJI MUHIMU KATIKA SEKTA YA KILIMO NCHINI ............ 28

SURA YA TATU ............ 31

3.1 UTANGULIZI ............ 31
3.2 UTAMBUZI WA MAHITAJI HALISI YA PEMBEJEO NCHINI HAUKUFANYIKI KWA UFANISI ............ 31
3.3 USAMBAZAJI DUNI WA PEMBEJEO ZA KILIMO ............ 36
3.4 UFUATILIAJI NA TATHMINI KWENYE UPATIKANAJI WA PEMBEJEO NCHINI ............ 44

SURA YA NNE ............ 47

UDHIBITI WA UBORA KWENYE PEMBEJEO ZA KILIMO ............ 47

4.1 UTANGULIZI ... 47
4.2 USAJILI HAFIFU WA PEMBEJEO NA WAUZAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO ... 47
4.4 UENEZAJI HAFIFU WA MAARIFA KWA WAUZAJI WA VIUWATILIFU, WAKULIMA, NA MAOFISA UGANI ... 70
4.5 MAPUNGUFU KATIKA UFUATILIAJI WA SHUGHULI ZA UDHIBITI WA UBORA ... 77

**SURA YA TANO ... 79**

**USIMAMIZI WA MILIPUKO YA MAGONJWA NA VISUMBUFU VYA MIMEA ... 79**

5.1 UTANGULIZI ... 79
5.2 MIFUMO HAFIFU YA KUKINGA MILIPUKO YA MAGONJWA NA VISUMBUFU VYA MIMEA 79
5.3 UDHAIFU KWENYE NJIA ZA UDHIBITI WA MILIPUKO YA MAGONJWA NA VISUMBUFU VYA MIMEA... 85
5.4 USHIRIKIANO HAFIFU KATIKA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA VISUMBUFU VYA MIMEA NA MAGONJWA... 88

**SURA YA SITA ... 92**

**UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI ... 92**

6.1 UTANGULIZI ... 92
6.2 USIMAMIZI USIOJITOSHELEZA WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI KATIKA HATUA ZOTE ZA MIPANGO NA UTEKELEZAJI ... 92
6.3 MIPANGO ISIYOJITOSHELEZA KATIKA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI.... 93
6.4 USIMAMIZI USIOJITOSHELEZA KWENYE SHUGHULI ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI ... 98

**SURA YA SABA ... 111**

**HUDUMA ZA UGANI ... 111**

7.1 UTANGULIZI ... 111
7.2 UTOAJI HAFIFU WA HUDUMA ZA UGANI KWA WAKULIMA ... 111
7.3 MAMBO YALIYOCHANGIA UTOAJI HAFIFU WA HUDUMA ZA UGANI ... 114

**SURA YA NANE ... 125**

**UTOAJI WA HUDUMA SAIDIZI KWA WASINDIKAJI KWA MAZAO YA KILIMO ... 125**

8.1 UTANGULIZI ... 125
8.2 UTOAJI WA HUDUMA SAIDIZI HAFIFU KWA WASINDIKAJI WA MAZAO YA KILIMO; ... 125
8.3 SABABU ZINAZOCHANGIA UTOAJI HAFIFU WA HUDUMA SAIDIZI KWA WASINDIKAJI WA MAZAO YA KILIMO ... 130
8.4 UFUATILIAJI NA TATHMINI KWA SHUGHULI ZA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI 135
8.5 MADHARA YA UTOAJI HAFIFU WA HUDUMA SAIDIZI KWA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI139

SURA YA TISA ........................................ 144
HITIMISHO ........................................ 144
9.1 UTANGULIZI ........................................ 144
9.2 HITIMISHO LA JUMLA ........................................ 144
9.3 HITIMISHO MAALUMU ........................................ 144
SURA YA KUMI ........................................ 148
MAPENDEKEZO ........................................ 148
10.1 UTANGULIZI ........................................ 148
10.2 MAPENDEKEZO MAALUMU KWA WIZARA YA KILIMO ........................................ 148

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| RDS | - | Mfumo wa Data za Kawaida za |
| ASDP | - | Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo |
| ASDS | - | Mkakati wa Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo |
| BXW | - | Ugonjwa wa Migomba |
| CBAF | - | Utabiri wa Kienyeji wa Viwavijeshi |
| CMC | - | Kamati ya Usimamizi wa Mikopo |
| DADPs | - | Programu ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya |
| DAICO | - | Ofisa Kilimo, Umwagiliaji, na Ushirika wa Wilaya |
| FAO | - | Shirika la Chakula na Kilimo Ulimwenguni |
| FFSs | - | Shule za Mafunzo ya Kilimo Mashambani |
| GDP | - | Pato la Jumla la Ndani |
| IPM | - | Udhibiti wa Pamoja wa Visumbufu vya Mimea |
| LGAs | - | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| M & E | - | Ufuatiliaji na Tathmini |
| MITI | - | Wizara ya Viwanda, Biashara, na Uwekezaji |
| MLND | - | Ugonjwa wa Mahindi |
| MTEF | - | Kiunzi cha Matumizi ya Muda wa Kati |
| NIRC | - | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| PHS | - | Huduma za Afya ya Mimea |
| OR-TAMISEMI | - | Ofisi ya Raisi – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| SAGCOT | - | Ukanda wa Kusini wa Ukuaji wa Kilimo Nchini Tanzania |
| SDGs | - | Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| SIDO | - | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogovidogo |
| SMEs | - | Wajasiriamali Wadogo na wa Kati |
| TDC | - | Kituo cha Uendelezaji wa Teknolojia |
| TFRA | - | Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea |
| TOSCI | - | Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu |
| TPRI | - | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu |
| VAEO | - | Ofisa Ugani wa Kijiji |
| WAEO | - | Ofisa Ugani wa Kata |
| WARCs | - | Vituo vya Huduma za Kilimo vya Kata |

# DIBAJI

Nina furaha kuwasilisha Ripoti yangu ya kumi ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu. Ripoti hii ya jumla inahusu ripoti sita za Ukaguzi wa Ufanisi kwa serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, na mamlaka zenye wajibu wa kushughulikia masuala ya maendeleo ya sekta kilimo nchini.

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa wadau (wabunge, maofisa wa serikali kuu na serikali za mitaa, wanahabari, wahisani, na asasi za kijamii na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyopo kwenye ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kufikia mwezi Machi 2019. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizotolewa kwa kifupi unapatikana kwenye ripoti husika za ukaguzi ambazo zilikabidhiwa kwa maofisa masuuli (makatibu wakuu) wa wizara husika.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, kwa mujibu wa Kifungu cha 143 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na Kifungu cha 34 (1) na (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Raisi kila taarifa aliyotoa kwa mujibu wa Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Raisi atamwelekeza waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku saba kupita toka kikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Raisi, kwa sababu zozote zile, atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu unatarajiwa kuniwezesha kupata taarifa na kuwa na udhibiti muhimu wa raslimali zote zilizopo kwa ajili ya Ofisi. Hii ni pamoja na raslimaliwatu na fedha, ambazo zitaiwezesha Ofisi yangu kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote zikiwemo zile ninazozikagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka ya kufanya Ukaguzi wa Ufanisi, Ukaguzi wa Utambuzi, Ukaguzi wa Mazingira, na Ukaguzi Maalumu. Aina hizi za ukaguzi ni zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa miaka mingi.

Kimsingi, Ripoti hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi, na uadilifu katika matumizi ya raslimali za umma hususani katika masuala ya maendeleo ya sekta ya kilimo nchini katika maeneo ya usimamizi wa utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima; na usimamizi wa udhibiti wa visumbufu vya mimea na milipuko ya magongwa ya mimea. Maeneo mengine ni usimamizi wa utoaji wa huduma za usaidizi kwa wajasiliamali wadogo na wa kati nchini; usimamizi wa viuwatilifu katika shughuli za kilimo; usimamizi wa upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo kwa wakulima nchini; pamoja na usimamizi wa shughuli za ujenzi wa miradi ya umwagiliaji Tanzania.

Lengo kuu la kufanya ukaguzi katika maeneo haya ni kuangalia iwapo raslimali zilizotengwa zimetumika kwa ufanisi kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati Ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa ripoti ya utendaji wa serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma kulingana na sheria katika taratibu zilizopo, wajibu wa kuhakikisha uwepo wa ufanisi, uwekevu, na tija katika matumizi ya raslimali za umma ni wa maofisa masuuli. Wakati huohuo, ni wajibu wa maofisa masuuli kuhakikisha kuwa uchunguzi unafanyika na mapendekezo Hakunaiyoyatoa yanatekelezwa kikamilifu.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataandaa taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa raslimali za umma ndani ya serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Hivyo, serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, na Ofisi yangu kwa pamoja zina mchango mkubwa kwa Bunge katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa raslimali za umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora kwa raslimali yanafanana.

Ninapenda kutambua weledi na dhamira ya wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendeakazi, mishahara duni, na wakati mwingine kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma. Aidha, Ofisi yangu inahakikisha ukaguzi wake unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu

yanayochangia au kutarajiwa kuchangia maendeleo ya sekta ya umma hasa usimamizi wa masuala yahusuyo usalama wa wananchi wanapopata huduma mbalimbali. Hivyo, kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa raslimali za umma.

Ninatarajia kuwa Bunge litaiona Ripoti hii kuwa muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa raslimali za umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania.

Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
16 Mtaa wa Samora,
S.L.B. 9080,
**11101 Dar es Salaam**
**28 Machi, 2019**

## SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioweka mazingira wezeshi kwangu kuweza kutimiza wajibu wangu wa kikatiba. Ninapenda kumshukuru kila mfanyakazi katika Ofisi yangu kwa jitihada zake ambazo zimeniwezesha kutoa ripoti kwa wakati. Ninalazimika kuishukuru familia yangu na za wafanyakazi katika Ofisi yangu kwa uvumilivu wao waliouonesha wakati wa kipindi chote cha kutimiza wajibu huu wa kikatiba.

Ninapenda kuishukuru Serikali na Bunge letu tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, shukrani za pekee ziende kwa jumuiya ya wahisani hasa Ofisi ya Ukaguzi ya Uholanzi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Swideni, Serikali ya Swideni kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Swideni, Shirika la Misaada la Watu wa Marekani, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza, Umoja wa Ulaya, Mradi wa Ushirikiano wa Uswisi na Ujerumani ukisimamiwa na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa wa Ujerumani, na Bank ya Dunia kupitia Mpango wa Usimamizi wa Fedha za Umma, na wengine wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika Ofisi yangu. Mchango wao katika kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi, mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano, na nyenzo mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio yetu.

Halikadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na maofisa masuuli wa taasisi Hakunaizozikagua kwa kutoa mchango mkubwa na taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajili ya maandalizi ya ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi ambazo ndizo zimewezesha uandaaji wa Ripoti hii ya jumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, wataalamu wa kujitegemea, na maofisa wastaafu wa serikali kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi kupitia maoni na uhakiki walioufanya katika rasimu za ripoti.

Ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu ambayo Ripoti hii pamoja na ripoti mahususi zitafikishwa kwa ajili ya uchambuzi, majadiliano, na kutoa maelekezo yake. Tunatarajia kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu itatupa maboresho na mwelekeo utakaotokana na mjadala wa ripoti hizi.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru maofisa masuuli na watumishi wote wa taasisi za umma Tanzania nzima. Ninatambua pia mchango wa walipakodi ambao ripoti hii tunaitoa kwao. Mwenyezi Mungu awabariki nyote kadri

mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya raslimali za umma nchini.

# MUHTASARI

Ukaguzi wa Ufanisi unalenga kuboresha uwajibikaji na ufanisi wa taasisi za umma. Pia, unatoa tathmini mahsusi ya namna taasisi ziliokaguliwa zilivyotumia raslimali katika kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi. Kifungu Namba 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi wa Ufanisi.

Ripoti hii ya jumla inaainisha mapungufu yaliyobainika, hitimisho, na mapendekezo ya ripoti saba za ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya kilimo uliofanyika kati ya mwaka 2015 na 2019 kuhusu utoaji wa huduma kwa wakulima; milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea; viuwatilifu kwenye shughuli za kilimo; utoaji msaada na huduma kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; upatikanaji na ufikiaji wa pembejeo za kilimo bora kwa wakulima; usimamizi wa shughuli za ujenzi wa miradi ya umwagiliaji; na utoaji wa huduma za ugani, ambayo inajumuisha taarifa ya ufuatiliaji.

Mtazamo huu maalumu kwenye eneo la kilimo umetolewa ili kutathmini jinsi serikali inavyosimamia maendeleo ya kilimo katika kuhakikisha ufanisi, ushindani, na faida ya sekta ya kilimo katika kuchangia kuboresha maisha ya Watanzania kufikia ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Ripoti hii inabainisha masuala muhimu yaliyobainika katika kaguzi za ufanisi zilizofanywa dhidi ya kile kilichotarajiwa katika upande wa utoaji wa huduma.

Kwa ujumla Ripoti hii ina lengo la kuwasaidia wabunge, serikali, vyombo vya habari, umma, na wadau wengine kuweza kufanya maamuzi yenye kuongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika utendaji wa serikali katika sekta ya kilimo. Aidha, Ripoti hii ya majumuisho hailengi kuwa mbadala wa ripoti saba zilizowasilishwa katika miaka tajwa ya kifedha. Hivyo, msomaji anashauriwa kusoma ripoti za ukaguzi husika ili kuweza kupata undani wa kilichokaguliwa.

Ripoti hii inatoa ufafanuzi wa ripoti mojamoja za ukaguzi wa ufanisi kuhusu kiwango ambacho taasisi za serikali zinasimamia maendeleo ya sekta ya kilimo na kuhakikisha kuna ufanisi katika utekelezaji wa hatua zake katika maendeleo ya sekta ya kilimo. Yafuatayo ni matokeo makuu ya ukaguzi kutoka kwenye kaguzi zilizofanywa.

**Mchakato Usio na Ufanisi wa Kutambua Mahitaji ya Membejeo za Kilimo**
Ukaguzi ulibaini mchakato wa kutambua mahitaji ya pembejeo za kilimo haufanyiki kwa ufanisi ili kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji halisi ya wakulima. Mchakato huo unaambatana na udhaifu katika kukusanya taarifa

za kutumika katika kutambua mahitaji wakati mchakato halisi wa kutambua unafanywa kwa kutowashirikisha wadau wote muhimu katika usambazaji wa pembejeo za kilimo. Upungufu huu ulisababisha uwepo wa takwimu zisizo sahihi katika kutambua mahitaji na kuweka pengo la muda mrefu kati ya mahitaji na upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka minne iliyopita, ugavi wa wastani wa pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mbegu, mbolea, na viuwatilifu ulifikia asilimia 39 tu ya jumla ya mahitaji.

**Usambazaji Usio na Ufanisi wa Pembejeo Bora za Kilimo**
Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo wa usambazaji haukuwa na ufanisi katika kuhakikisha pembejeo bora za kilimo zinawafikia wakulima kwa wakati. Katika halmashauri 4 zilizotembelewa na wakaguzi, ilibainika kuwepo kwa ucheleweshaji wa miezi 3 hadi 5 baada ya kuanza kwa msimu wa kilimo. Licha ya kuwa na idadi ndogo ya wakala wa pembejeo, mfumo wa usambazaji unategemea sana sekta binafsi ambapo wazalishaji au waagizaji toka nje ya nchi wanasambaza pembejeo zao za kilimo kupitia wasambazaji wa ndani na mawakala wa kilimo.

Ukaguzi umebaini pia kulikuwa na udhibiti dhaifu wa mtandao wa usambazaji wa pembejeo za kilimo, jambo ambalo liliruhusu usambazaji na uuzaji wa pembejeo zenye ubora mdogo, bandia, zisizoidhinishwa, na zisizofaa kwa matumizi ya wakulima. Udhibiti dhaifu pia ulisababisha kutofuatwa kwa bei elekezi za mbolea kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea.

**Udhibiti-ubora Hafifu wa Pembejeo za Kilimo**
Ukaguzi ulibaini udhaifu katika shughuli za udhibiti-ubora zilizofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu, na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu. Udhaifu ulibainika katika usajili, ukaguzi, na mafunzo kama namna ya kuhakikisha kunakuwepo udhibiti-ubora wa pembejeo za kilimo.

*Mapungufu katika usajili wa wauzaji na mawakala wa pembejeo za kilimo*: Ukaguzi ulibaini udhaifu katika usajili wa wauzaji na mawakala wa pembejeo za kilimo na ambapo ulitoa mwanya wa uwepo wa wauzaji na mawakala wa pembejeo za kilimo ambao hawakusajiliwa, pamoja na pembejeo za kilimo zisizosajiliwa katika soko. Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 33 ya mawakala wa kilimo hawakusajiliwa kuuza mbegu na mbolea kwenye soko. Ukaguzi ulionesha pia hapakuwa na orodha iliyohuishwa ya viuwatilifu halali vinavyofaa kwa ajili ya matumizi. Matokeo yake, udhaifu wa ukaguzi na usajili wa pembejeo za kilimo ulipelekea kuwepo kwa pembejeo za kilimo zilizoingizwa nchini kinyume cha sheria; uuzaji wa pembejeo za kilimo zilizofungashwa kwa mara ya pili; na usambazaji katika soko wa pembejeo za kilimo zenye ubora wa chini.

*Ukaguzi dhaifu wa pembejeo za kilimo*: Ukaguzi ulibaini kuwa ukaguzi uliofanywa mipakani na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu haukuwa wa kutosha katika kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo zilizosajiliwa tu ndizo zinaagizwa na kuuzwa kwenye soko. Ukaguzi pia ulibaini kuwa hakukuwa na udhibiti wa kutosha katika uagizaji wa mbegu ambapo imepelekea kuwepo kwa uingizaji nchini wa mbegu za bandia na za ubora wa chini. Aidha, ilibainika kuwa hakukufanyika ukaguzi wa kutosha katika sampuli ya mashamba 19 ya mbegu, na mashamba 6 hayakukaguliwa kabisa.

*Mapungufu kwenye uenezaji wa ujuzi kwa wakulima, mawakala wa kilimo na maofisa ugani*: Ukaguzi ulibaini kwamba uenezaji wa ujuzi kwa wauzaji wa viuwatilifu, wauzaji wa mbegu na mbolea, maofisa ugani, na wakulima haukuwa wa kutosha. Tathmini ya ujuzi na ufahamu wa pembejeo za kilimo ilionesha kuwa wakulima hawakuwa na ujuzi wa matumizi mazuri ya mbegu, viuwatilifu, na mbolea. Maofisa ugani hawakuwa na ujuzi wa utoaji wa huduma za utaalamu wa kilimo kwa wakulima ambazo ni pamoja na matumizi sahihi ya mbegu, mbolea, na viuwatilifu. Pia, mawakala wa pembejeo za kilimo hawakuwa na ujuzi wa matumizi bora na sahihi ya viuwatilifu na mbolea ambazo walikuwa wakiuza. Katika Halmashauri ziliyotembelewa, asilimia 80 ya wauzaji wa mbegu za mbolea hawakuwa na ujuzi kuhusu mbegu na mbolea ambazo walikuwa wakiziuza.

**Ufuatiliaji na tathmini Isiyotosheleza katika Usajili, Mafunzo, na Ukaguzi wa Pembejeo za Kilimo**

Ukaguzi ulibaini kwamba ingawa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu ilifanya ufuatiliaji wa viuwatilifu, ufuatiliaji huo haukugusa maeneo yote matatu ya udhibiti-ubora ambayo ni usajili, ukaguzi, na elimu. Ufuatiliaji uliofanywa na Wizara ya Kilimo ulijikita zaidi katika udhibiti wa shughuli za usajili kupitia Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Kinga ya Mimea na Kamati ya Kitaalamu ya Kusajili na Kupitisha ili kuhakikisha kwamba viuwatilifu vilivyosajiliwa vimekidhi vigezo vilivyotakiwa.

**Usimamizi Dhaifu wa Udhibiti wa Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea**

Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Kilimo haikutekeleza ipasavyo mikakati ya kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mimea. Hii ni kutokana na kutokuwa na namna bora za kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mimea kwa njia ya kinga; na udhibiti na uratibu wa pamoja unaoshirikisha wadau tofauti katika kudhibiti milipuko ya magonjwa.

*Udhaifu kwenye njia za uzuiaji wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea:* Ukaguzi ulibaini kwamba mifumo ya kudhibiti na kujikinga na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea ili kuhakikisha vinapungua kwa kiasi kikubwa haikufanya kazi ipasavyo. Ukaguzi ulibaini kuwa

hakukufanyika ukaguzi wa kutosha katika mipaka ya nchi; hakukuwa na ufahamu wa wakulima wa kutumia mbinu unganishi na usimamizi wa kujikinga na visumbufu vya mimea; na kulikuwa na upatikanaji mdogo wa mbegu bora na viuwatilifu vya kudhibiti visumbufu vya mimea.

*Udhaifu kwenye njia za udhibiti wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea:* Wizara ya Kilimo na Chakula na TAMISEMI hazikuchukua kikamilifu hatua za udhibiti wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Ukaguzi ulibaini kuwa ufuatiliaji wa utambuzi wa viuwatilifu haukufanyika. Ilibainika pia kuwa utoaji taarifa na uchukuaji hatua haukufanyika. Aidha, ingawa mipango inayozingatia viashiria hatarishi vya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea ilitengenezwa katika baadhi ya halmashauri zilizotembelewa, mipango hiyo haikutekelezwa kikamilifu.

*Udhaifu katika kuratibu udhibiti wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea:* Ukaguzi ulibaini kwamba kulikuwa na udhaifu katika shughuli za uratibu kwa ngazi za mikoa na wilaya. Uratibu kati ya Wizara ya Kilimo na sekta binafsi, na kati ya sekta binafsi na taasisi za serikali haukufanyika kwa kiasi cha kutosha. Kwa mfano, kutokana na kukosekana kwa maabara, wakaguzi wa Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea walikuwa wakituma sampuli zilizokamatwa katika mipaka kwa ajili ya vipimo kwenda Taasisi ya Utafiti wa Viuwatilifu. Hata hivyo, hakukuwa na mifumo iliyowekwa kusaidia mabadilishano mepesi yenye ufanisi ya sampuli.

**Usimamizi Dhaifu wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji wakati wa Mipango na Utekelezaji**

Ukaguzi ulibaini kwamba shughuli za ujenzi wa miundombinu hazikusimamiwa kwa kiasi cha kutosha katika kanda za umwagiliaji. Matokeo yake, skimu za umwagiliaji hazikukamilika kwa wakati; skimu zilijengwa kwa gharama ya juu kuliko zile zilizokubaliwa; na ziliathirika katika ubora.

*Mipango dhaifu ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji*: Ukaguzi ulibaini kwamba mipango ya jumla kabla ya kuanza shughuli za ujenzi wa skimu za umwagiliaji haikufanywa kwa kiasi cha kutosha. Ukaguzi ulibaini kwamba ni asilimia tatu tu ya miradi ndiyo ilifanyiwa upembuzi yakinifu kati ya miradi iliyopangwa kufanyiwa, kinyume cha Sheria ya Umwagiliaji.

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa utegemezi wa fedha za wafadhili zilizofikia asilimia 90 ya fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya kugharamia miradi ya umwagiliaji kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2017/18. Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba upembuzi yakinifu haukugusa vipengele muhimu kama vile uchunguzi wa udongo, kiasi cha maji, na athari za mazingira. Matokeo yake ni kutotumiwa kwa vipengele hivyo wakati wa ujenzi wa miradi.

*Usimamizi dhaifu wa shughuli za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji:* Ukaguzi ulibaini usimamizi dhaifu wa shughuli za ujenzi hali iliyopelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi. Ukaguzi ulibaini kwamba asilimia 76 sawa na skimu 63 kati ya skimu 83 za umwagiliaji zilichelewa kukamilika. Aidha, asilimia 40 ya skimu zilikamilika zikiwa na ongezeko la gharama. Miradi ilibainika kutokuwa na ratiba nzuri za ujenzi, michoro isiyo na uhalisia, kucheleweshwa kwa malipo kwa wakandarasi, na baadhi ya wakandarasi kuacha kazi kutokana na kutokuwa na vifaa.

**Huduma Hafifu za Ugani kwa Wakulima**

Ukaguzi ilibaini kwamba utoaji wa huduma za ugani hivi sasa si kamilifu na hautoi hakikisho la upelekaji wa mbinu za kisasa za kilimo na uchakataji wa mazao ya kilimo unaochangia kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao na bidhaa zitokanazo na kilimo. Ukaguzi ulibaini kwamba mbinu zilizokuwa zikitumika katika utoaji wa huduma za ugani zilikuwa chache na zilijikita hasa katika utoaji wa huduma kwa njia ya mashamba darasa na vituo vya huduma za kilimo vya kata pekee; wakati mbinu zingine hazikutumiwa kwa kiwango cha kutosha. Aidha, nyenzo zilizokuwa zikitumiwa na maofisa ugani hazikuwa na ufanisi na hazikujumuisha idadi ya kutosha ya wakulima na hasa mbinu ya mashamba darasa ambayo ilijumuisha asilimia moja tu ya wakulima wote waliotembelewa.

*Jitihada hafifu za kuwajengea uwezo maofisa ugani:* Ukaguzi ilibaini kwamba maofisa ugani hawakuwezeshwa kwa nyenzo na maarifa ya kisasa kuhusu utoaji wa huduma za ugani ili kuwapa ujuzi wa mbinu mpya katika utoaji wa huduma za ugani na kuweka taarifa za kisasa kwenye madodoso ya mafunzo. Zaidi, maofisa ugani hawakupewa mafunzo ya kutumia miongozo na hawakupewa mafunzo kuhusu matumizi ya viuwatilifu.

*Utoaji hafifu wa fedha kwa ajili ya huduma za ugani:* Upelekaji wa fedha haukuweza kurahisisha utoaji wa huduma za ugani. Ukaguzi ulibaini udhaifu katika mchakato wa bajeti. Ilibainika kuwa shughuli za ugani zilitengewa kiwango kidogo cha fedha. Istoshe, baaadhi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya huduma za ugani zilitumika kwa shughuli zingine tofauti. Kwa mfano, fedha kwa ajili ya mashamba darasa na mafunzo ya maofisa ugani na wakulima zilitolewa kwa kiwango kinachofikia asilimia 97 wakati utekelezaji wake ulifanywa kwa asilimia 30 tu kwa shughuli za uandaaji wa mashamba darasa. Mafunzo na huduma za ugani yalifanywa kwa asilimia 59 wakati ni asilimia moja pekee ya wakulima ndiyo walipewa mafunzo ya mbinu bora za kilimo.

**Utoaji wa Huduma Saidizi Hafifu kwa Wasindikaji wa Mazao ya Kilimo**

Ukaguzi ulibaini kwamba wajasiriamali na wenye viwanda vidogo wakiwemo wasindikaji wa mazao ya kilimo hawakupewa huduma saidizi za kutosha zinazohitajika kwenye maeneo ya teknolojia, fedha, masoko, na elimu ya biashara ambazo zingerahisisha uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo.

Ukaguzi ulibaini kwamba asilimia tisa pekee ya wajasirimali na wenye viwanda vidogo waliosajiliwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilipatiwa mafunzo wakati asilimia 37 ya walioomba mikopo ya fedha hawakupatiwa licha ya kutimiza vigezo vya kupatiwa mikopo hiyo. Uhamishaji wa teknolojia kwenda kwa wasindikaji haukufanywa kwa kiwango cha kutosha kwa kuwa idadi ya teknolojia zilizohamishwa kwenda kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo ilikuwa chini ya wastani wa idadi ya teknolojia zilizohamishwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17.

*Mipango Hafifu ya Huduma Saidizi kwa Wasindikaji Mazao ya Kilimo:* Ukaguzi ulibaini kwamba mipango ya utoaji wa huduma saidizi haikufanywa kwa kiasi cha kutosha kuweza kutoa hakikisho la ubora wa huduma saidizi zinazotolewa. Ukaguzi ulibaini kwamba wadau muhimu hawakushirikishwa wakati wa kuandaa bajeti na pia shughuli za wasindikaji wa mazao ya kilimo hazikupewa kipaumbele cha kutosha katika ngazi ya wizara wakati wa uandaaji wa bajeti. Katika ngazi ya wizara, bajeti kwa ajili ya maendeleo ya wasindikaji wa mazao ya kilimo ilikuwa ni asilimia 30 tu ya fedha zilizokuwepo huku asilimia 70 iliachwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ndani ya idara ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati.

*Kutofanyika kwa tathmini ya kutosha ya mahitaji ya wasindikaji:* Ukaguzi ulibaini kwamba hakukuwa na mfumo wa kutosha wa ukusanyaji wa mahitaji ya wajasiriamali wadogo na wa kati ambao ungehakikisha unazingatia mahitaji ya sehemu kubwa ya wasindikaji wa mazao ya kilimo. Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ambalo lilitakiwa kukusanya mahitaji hayo liliweza kufanya tathmini ya mahitaji mara 1779 tu ambayo ilikuwa chini ya malengo yake ya kufanya hivyo mara 2150 katika miaka 4 iliyopita.

*Ufuatiliaji usiotosheleza wa shughuli za wasindikaji wa mazao ya kilimo:* Ukaguzi ulibaini kwamba mifumo ya utoaji ripoti na ufuatiliaji wa shughuli za utoaji wa huduma saidizi haukufanywa kwa kiasi cha kutosha. Mfumo uliopo ulikuwa ukitoa taarifa za kitarakimu za viashiria vya mipango ya mwaka katika ngazi ya juu ya utekelezaji, lakini taarifa za kimaelezo hazikutolewa katika ngazi ya usimamizi na ngazi ya uongozi wa juu.

Aidha, ukaguzi ulibaini pia kwamba wasindikaji wengi wa mazao ya kilimo wanatembelewa mara chache au hawatembelewi kabisa na maofisa wa shirika la viwanda vidogo. Katika sampuli ya wasindikaji wa mazao ya kilimo 36 waliotembelewa na timu ya ukaguzi, ni asilimia 6 pekee ndiyo walikuwa wakitembelewa mara kwa mara huku asilimia 94 hawakutembelewa au walitembelewa mara chache sana.

Matokeo yake ni utoaji hafifu wa huduma saidizi kwa wasindikaji mazao ya kilimo uliopelekea kuwa na mchango hafifu wa wasindikaji wa mazao ya kilimo katika uchumi ambapo mchango wao katika pato la taifa kwa sasa ni

asilimia 35 ambalo ni chini ya lengo lililowekwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji ambalo ni asilimia 50.

**Hitimisho**

Kiujumla, ukaguzi unatambua jitihada za Serikali juu ya maendeleo ya kilimo nchini. Hata hivyo, mambo yaliyoonekana kwenye ripoti ya ukaguzi yamepelekea hitimisho kwamba, Serikali haijatekeleza kwa ufanisi mikakati mbalimbali ili kufanya kilimo kuwa na tija, endelevu, na uti wa mgongo wa uchumi wa nchi.

Mikakati muhimu iliyoanzishwa na Wizara ya Kilimo kwa maendeleo ya kilimo haikusimamiwa vizuri na Wizara pamoja na wadau wengine. Udhaifu ulioonekana ulikuwa kwenye usimamizi wa pembejeo za kilimo, ubora wa udhibiti wa pembejeo za kilimo, visumbufu vya mimea na milipuko ya magonjwa, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, uwepo wa huduma za ugani kwa wakulima, na utoaji wa usaidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo.

Mapungufu yaliyoonekana yalisababishwa na udhaifu wa mifumo ya kuhakikisha mipango, utekelezaji, usimamizi, na tathmini ya mikakati iliyotekelezwa na Serikali kwa lengo la kusaidia maendeleo ya sekta ya kilimo.

**Mapendekezo**

Kutokana na hitimisho langu, Wizara ya Kilimo inatakiwa:

1) Ihuishe taarifa zilizopo na kuboresha hatua zilizopo za usajili, ukaguzi, na mafunzo kwa mawakala wa pembejeo za kilimo na wakulima ikiwa ni njia ya kudhibiti ubora kwenye viuwatilifu, mbegu, na mbolea ili kujihakikishia uwepo wa pembejeo zenye ubora katika soko;

2) Iweke mfumo utakaohakikisha kuwa mikakati ya kudhibiti na kuzuia milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea inafanywa kisasa ili kuhamasisha ubora wa mazao ya kilimo ili kupunguza kiwango cha uwezekano wa kutokea uhaba wa chakula na kuimarisha ubora wa mazao katika soko la kimataifa.

3) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, iimarishe uwezo wake katika kutoa huduma saidizi kwa nyanja zote za wasindikaji ili kuhamasisha uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo na hivyo kuiwezesha nchi kuwa ya uchumi wa kati wa viwanda.

4) Iimarishe namna ya kuwasaidia wazalishaji wa ndani ya nchi wa mbegu, viuwatilifu, na mbolea ili kuhamasisha uzalishaji wa pembejeo za kilimo

ndani ya nchi na hivyo kutoa hakikisho la kupatikana kwa pembejeo kwa wakati.

5) Ihakikishe kwamba programu za kuwaendeleza kitaalamu maofisa ugani zinaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji yao na zinatekelezwa kikamilifu zikiwa na malengo ya kuwapatia uwezo wa kutoa huduma za ugani kwa wakulima. Hii ni pamoja na kuwapa maofisa ugani taarifa na ujuzi wa kisasa ya mbinu na teknolojia za kisasa za kilimo.

6) Ipitie mnyororo wake wa maagizo ili kuhakikisha kwamba hatua zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma za ugani katika mamlaka za serikali za mitaa zinatekelezwa katika namna itakayoleta matokeo chanya.

7) Ihakikishe kwamba kazi za usanifu wa miradi ya ujenzi inafanyiwa mapitio ili kujiridhisha kuhusu kutekelezeka kwake kabla ya kuanza shughuli za ujenzi.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Ukaguzi

Ukaguzi wa Ufanisi ni muhimu kwa sababu unalenga kuboresha uwajibikaji na utendaji wa taasisi za Serikali ili wananchi wapate huduma zinazolingana na thamani ya fedha zilizotumika. Vigezo kadhaa hutumika kuchagua maeneo yanayolengwa na ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalumu. Miongoni mwa vigezo hivyo ni malalamiko ya wananchi, umuhimu wa eneo linalokaguliwa, pamoja na sababu za kijamii na kiuchumi.

Ukaguzi wa ufanisi unafanyika ili kufahamu iwapo shughuli, mipango, au miradi inayohusisha raslimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma imesimamiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi. Uwekevu, tija, na ufanisi unaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

- Uwekevu - Kupunguza gharama za raslimali zinazotumika katika shughuli huku kukizingatiwa ubora stahihi.
- Ufanisi - Uhusiano kati ya matokeo, kwa kuzingatia bidhaa, huduma, matokeo na raslimali zilizotumika kuzalishia.
- Tija - Kiwango cha kufikiwa kwa malengo na uhusiano kati ya malengo yaliyokusudiwa na matokeo halisi katika shughuli husika.

## 1.2 Mamlaka ya Kukagua

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008. Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija, na ufanisi katika matumizi ya fedha au raslimali za taasisi ya umma, anaweza kukagua, kuchunguza, na kutoa ripoti, kadri atakavyoona inafaa kuhusu:

(a) Matumizi ya fedha na raslimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mamlaka nyingine za serikali;

(b) Utekelezaji wa majukumu ya maofisa masuuli, wakuu wa idara, na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma; na

(c) Utekelezaji wa matakwa ya sheria ya mazingira, kanuni, na sera ya ndani ya mazingira na viwango".

Ukaguzi wa ufanisi unalenga kuangalia iwapo malengo ya awali yaliyowekwa yamefanikiwa. Vilevile, unaangalia iwapo uwekevu, tija, na ufanisi umezingatiwa. Hatimaye mapendekezo hutolewa kwa ajili ya kuboresha maeneo yaliyoonekana kuwa na mapungufu.

Ukaguzi unafanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinataka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kupanga na kutekeleza ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha ambao utakuwa kigezo cha kuripoti mapungufu yaliyoonekana na kutoa hitimisho kwa kuzingatia lengo la ukaguzi husika.

## 1.3 Madhumuni ya Ripoti

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu wabunge, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika shughuli za Serikali. Ripoti hii inabainisha masuala mbalimbali yaliyoonekana katika kaguzi za ufanisi dhidi ya yale yaliyotarajiwa katika hatua za mipango, utekelezaji, usimamizi wa vihatarishi, na ufutiliaji wa tathmini ya shughuli za maendeleo ya kilimo nchini.

Mwisho, muhtasari wa kila ripoti unatolewa kwa kubainisha mambo yatakayojadiliwa na Kamati za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikisha maofisa masuuli wakati wa kusikiliza hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa Ripoti sita za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo zimefupishwa katika sura zinazofuata. Ili kuweza kupata uelewa wa kina wa masuala mahsusi yaliyojadiliwa katika ripoti hii, msomaji anashauriwa kusoma ripoti binafsi zilizokamilika. Ripoti hizo ni za Kaguzi za Ufanisi katika maeneo yafuatayo:

i) Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima Tanzania (2015);
ii) Usimamizi wa Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Milipuko ya Magongwa ya Mimea Tanzania (2016);
iii) Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usaidizi kwa Wajasiliamali Wadogo na wa Kati Nchini Tanzania (2018);
iv) Usimamizi wa Viuwatilifu katika Shughuli za Killimo;
v) Usimamizi wa Upatikanaji wa Pembejeo Bora za Kilimo kwa Wakulima Tanzania (2019); na
vi) Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji Tanzania (2019)

## 1.3 Lengo kuu la Ripoti

Ripoti hii imelenga kuonesha jinsi Serikali inavyosimamia maendelelo ya sekta ya kilimo ili kuhakikisha inakuwa yenye ufanisi, ya ushindani, na inayoleta faida ili ichangie kuboresha maendeleo ya Mtanzania. Pia, inalenga kufanya sekta ya kilimo kuwa yenye faida na inayokuza uchumi na kuondoa umaskini. Hivyo, sekta ya kilimo inapaswa isimamiwe na kutumika kwa ajili ya malengo ya muda mrefu ya taifa kwa ujumla.

Aidha, kilimo ndicho chanzo kikuu cha mapato kwa Serikali na ndicho kinatoa shunguli nyingi za kiuchumi kwa Watanzania kwa zaidi ya asilimia 75.5[1]. Kwa mujibu wa Ripoti ya Utekelezaji wa Progamu ya Kuendeleza Uchumi Tanzania kwa Mwaka 2017/18, sekta ya kilimo inachangia asilimi 30 ya pato la taifa. Ni muktadha huu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kuandaa Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ili kutoa matokeo ya namna Wizara ya Kilimo inavyosimamia sekta hii muhimu.

## 1.4 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu Zilizotolewa katika Ripoti Hii

Wizara, idara, mashirika, taasisi, na wakala mbalimbali za Serikali zilizokaguliwa zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao juu ya matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya Ripoti hii.

## 1.5 Muundo wa Ripoti Hii

Ripoti hii ina sura kumi. Sura ya Kwanza inatoa utangulizi kuhusu ukaguzi wa ufanisi, mamlaka, na madhumuni ya ripoti kwa ujumla. Sura ya Pili inatoa muhtasari wa muundo wa usimamizi wa sekta ya kilimo nchini Tanzania; na Sura ya Tatu inatoa mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo kwa wakulima nchini.

Sura ya Nne inabainisha mapungufu yaliyoonekana katika utaratibu wa udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo ambazo zimezalishwa au kuagizwa kutoka nje ya nchi; na Sura ya Tano inajadili mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa udhibiti wa visumbufu vya mimea na milipuko ya magongwa ya mimea Tanzania.

Sura ya sita inabainisha mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji nchini; na Sura ya Saba inachambua mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima Tanzania.

[1]Sera ya Taifa ya Kilimo, 2013

Sura ya Nane inabainisha mapungufu katika usimamizi wa utoaji wa huduma za usaidizi kwa wajasiliamali wadogo na wakubwa nchini; na Sura ya Tisa inatoa majumuisho ya kila mapungufu yaliyoonekana katika sekta ya kilimo. Mwisho, Sura ya Kumi inatoa mapendekezo ya jumla ya namna ya kuboresha sekta ya kilimo nchini.

## SURA YA PILI

## MFUMO WA USIMAMIZI WA MAENDELEO YA KILIMO NCHINI

### 2.1 Utangulizi

Tanzania imeendelea kutegemea sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wake kwa kuwa inatoa fursa za ajira kwa asilimia 77.5. Kwa kipindi cha mwaka 2016, sekta ya kilimo imechangia asilimia 29.1 ya pato la taifa ikilinganishwa na asilimia 29.0 kwa mwaka 2015 (Ripoti ya Uchungizi wa Uchumi ya Mwaka 2016). Kwa kipindi cha mwaka 2017/18, mchango wake uliongezeka na kufikia asilimia 30 ya pato la taifa. Sekta ya kilimo inachangia sana ongezeko la ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini nchini. Hivyo, maendeleo ya kilimo yanabaki kuwa chanzo cha maendeleo ya kiuchhumi na kijamii nchini kwa sasa na siku zijazo.[2]

Tanzania ina zaidi ya hekta milioni 44 za ardhi inayofaa kwa kilimo na ni asilimia 33 tu ya kiasi hiki hutumika; na ina hekta milioni 29.4 kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kilimo cha umwagiliaji. Katika ardhi hii ya kilimo cha umwagiliaji, hekta milioni 2.3 zina uwezo wa juu; hekta milioni 4.8 zina uwezo wa kati; na hekta milioni 22.3 zina uwezo mdogo.

Inafahamika wazi kwamba kuna ongezeko kubwa la joto duniani na mabadiliko ya tabia ya nchi, ambayo yana athari mbaya kwa upatikanaji bora wa raslimali za maji kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo duniani kote, Tanzania ikiwemo. Katika hali hii, Tanzania inapaswa kutumia fursa ya kutambua maeneo ya uwezekano wa umwagiliaji.

Pamoja na fursa kubwa ya kilimo, uzalishaji wa mazao nchini Tanzania unakabiliwa na changamoto nyingi zinazohitaji utatuzi. Changamoto hizo ni pamoja na ardhi kuwa na uzalishaji mdogo, nguvukazi, pamoja na mtaji. Hii inasababishwa na ukosefu wa mitaji kwa ajili ya pembejeo za kilimo, mbegu bora, mbolea, pamoja na teknolojia. Changamoto zingine ni utegemezi kwa mvua kwa ajili ya kilimo, utoaji wa huduma duni za kilimo, miundombinu mibovu vijijini, viwanda duni vya usindikaji wa mazao ya kilimo, pamoja na mahusiono yasiyo mazuri katika mlolongo wa mazao ya kilimo. Changamoto zote hizi zinaweza kuzuia taifa kukosa mapato na kuwekeza katika sekta hii muhimu.

Iwapo changamoto hizi hazitatafutiwa ufumbuzi wa haraka na kwa umakini, Tanzania inaweza kulingana na nchi zinazoendelea barani

[2] Hotuba_ya_Wizara_ya_Kilimo_Mifugo_na_Uvuvi_final_Mei_13.05.2017.pdf visited on 18/02/2019

Afrika zenye uwezo mkubwa wa kilimo ambao umeshindwa kusaidia kuinua kiwango cha maisha ya watu wake. Mafanikio ya haraka katika sekta ya kilimo Tanzania yanahitaji Serikali kushirikisha wadau wengine katika kusimamia raslimali na kuongoza shughuli za kilimo ili kufikia maendeleo yanayohitajika. Serikali inapaswa kushiriki katika uwekezaji na umiliki wa michakato ya kimkakati na miundombinu.


## 2.2 Historia ya Maendeleo ya Kilimo Nchini Tanzania

Tangu kupatikana kwa uhuru nchini Tanzania, kilimo kimefanyiwa mageuzi mbalimbali yenye lengo la kukifanya kiwe chenye uzalishaji mkubwa na endelevu. Mipango, mikakati, na sera mbalimbali zimezinduliwa kwa lengo la kuboresha kilimo. Katika kipindi cha mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990 kumekuwa na mlolongo wa mabadiliko katika sekta ya kilimo, ikijumuisha kuruhusu soko huria, kuondolewa kwa ukiritimba wa serikali, kujiondoa kwa serikali katika miradi ya uzalishaji, na kuanza kuitegemea sekta binafsi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Changamoto kubwa ni kwamba mabadiliko haya hayakuzingatia tofauti za kijamii na kiuchumi; na kutozingatia madhara ambayo yangeweza kuathiri sera zinazoimarisha upatikanaji wa fursa za kiuchumi na tofauti za usawa.

Mwaka 1981 Serikali ilizindua Programu ya Taifa ya Uokoaji wa Uchumi, ambayo ililenga kuongeza uzalishaji wa kitaifa na mauzo ya nje ya nchi. Programu hii ilifuatiwa na Mpango wa Urekebishaji wa Mifumo kati ya 1982 na 1985.

Mnamo mwaka 1986, serikali ilianzisha Mpango wa Kuokoa Uchumi, ambao ulifuatiwa na Mpango wa Urekebishaji wa Mifumo wa Benki ya Dunia na wahisani wengine wengi walianza kuongeza msaada wao kwa Tanzania kwa kiasi kikubwa (Kwa taarifa zaidi, tazama **Kielelezo 2.1**).

**Kielelezo 2.1: Vipindi vya mabadiliko mbalimbali ya sekta ya kilimo Tanzania**




## 2.3 Mikakati ya Maendeleo ya Kilimo Nchini


Katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, sekta ya kilimo inajulikana kama eneo muhimu ambapo mpango-mkakati wa kiuchumi utatekelezwa ili kuchangia kujenga msingi imara wa uchumi wenye ushindani na wenye nguvu.

Mpango-mkakati ulitarajia kubadilisha kilimo kutoka kwenye uzalishaji mdogo wa kiuchumi na kuwa uchumi wa viwanda vya kati unaoongozwa na shughuli za kilimo cha kisasa na shughuli za uzalishaji zilizounganishwa kwa ufanisi na kusisitizwa kwa shughuli za viwanda na huduma saidizi katika maeneo ya vijijini na mijini[3].

### 2.3.1 Mipango Mbalimbali ya Serikali ya Kuongeza Tija katika Sekta ya Kilimo

Serikali ya Tanzania imeanzisha na kutekeleza mikakati mbalimbali ya muda wa kati na muda mrefu ya kuimarisha sekta ya kilimo ili kuongeza tija.

**Kielelezo 2.2: Mipango mbalimbali ya Serikali ya kuongeza tija katika sekta ya kilimo**




*Chanzo: Programu ya Maendeleo ya Kilimo*, *2016-2021*

### 2.3.2 Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo uliandaliwa mwaka 2001 ikiwa ni hatua ya kuweka misingi ya mbinu za kuendeleza sekta ya kilimo pamoja na na uchumi wa kitaifa kwa ujumla na kupunguza umaskini hasa katika maeneo ya vijijini. Lengo kuu la Mkakati huu

[3] Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – 1999 – Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Dar es Salaam

lilikuwa ni kujenga mazingira mazuri ya kuongeza tija katika ya sekta ya kilimo kama msingi wa mapato ya kuboresha kilimo na kupunguza umaskini wa vijijini kwa muda wa kati na muda mrefu. Lengo la Mkakati lilikuwa kufikia kiwango cha ukuaji wa kilimo kwa asilimia 5 kwa mwaka hasa kwa njia ya mabadiliko kutokana na ustawi wa kilimo na kilimo cha kibiashara. Ili kufanikisha Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Wizara ya Kilimo imeanzisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

### 2.3.3 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo

Hii ni programu ya kuendeleza sekta ya kilimo na namna ya kuendesha Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Programu hii ni sehemu ya matokeo ya uendeshaji kwa sera na mipango iliyopangiliwa ili kuboresha tena na kuimarisha uchumi wa taifa. Programu hii ni chombo cha serikali kuu kwa ajili ya kuratibu na kufuatilia maendeleo ya kilimo na kuwezesha mageuzi ya kitaifa. Pia, imeanzisha uhusiano wa uendeshaji kati ya Wizara Muhimu za Sekta ya Kilimo na wadau wengine wa kitaifa pamoja na kuanzisha mifumo yenye ufanisi zaidi ya usimamizi.

## 2.4 Mfumo wa Kisheria na Udhibiti


Kilimo kinaongozwa na Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013. Malengo makuu ni kukuza sekta bora ya kilimo yenye ushindani na yenye faida ambayo itachangia kuboresha maisha ya Watanzania na kufikia ukuaji wa kiuchumi na kupunguza umaskini.

Kuna sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamia sekta ya kilimo nchini, ambazo ni: Sheria ya Udhibiti wa Mimea Namba 13 ya Mwaka 1997, Kanuni za Udhibiti wa Mimea ya Mwaka 1998, Sheria ya Mbegu Namba 18 ya Mwaka 2003, Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2011 kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2017, pamoja na sheria na anuni zingine zinazohusiana na masuala mbalimbali ya kilimo.

## 2.5 Modeli ya Mkakati wa Maendelelo ya Kilimo Nchini Tanzania

Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo Tanzania unahusisha mkakati wa ugavi wa pembejeo za kilimo (mbolea, dawa, na mbegu zilizoboreshwa) pamoja na wakulima wenye ujuzi. Usimamizi wakati wa mavuno unahitajika ili kupunguza upotevu wa mazao. Hii inawezekana ikiwa wakulima watapata soko la mavuno ya mazao ili kuongeza thamani.

**Kielelezo 2.3 Modeli ya Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo nchini Tanzania**




## 2.6 Haja ya Kufanya Ukaguzi katika Sekta ya Kilimo

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania iliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi katika maeneo saba ya sekta ya kilimo. Maeneo haya yana umuhimu mkubwa kwa sababu yanaweza kuisaidia Serikali ya Tanzania kutambua fursa zinazotolewa na sekta hii.

Kwanza, utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima ni muhimu kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo kwa sababu ina uwezo wa kubadilisha changamoto zingine zote ili kuboresha maisha na ustawi wa wananchi. Kwa hiyo, kwa kujenga uwezo wa wakulima katika kilimo, kutasababisha nchi iweze kuongeza faida zinazotokana na mabadiliko ya sekta ya kilimo. Huduma za ugani, utafiti, na mafunzo zina umuhimu katika kuunganisha wakulima katika kupata teknolojia mpya, taarifa, na ujuzi ambao ni muhimu katika kuimarisha uzalishaji wa kilimo.

Pili, usimamizi wa udhibiti wa milipuko ya visumbufu na magonjwa ya mazao ya kilimo huhamasisha njia za udhibiti na kuweka pamoja jitihada za kuzuia na kusimamia mlipuko wa visumbufu na magonjwa hayo ya mazao ya kilimo. Kama visipodhibitiwa, visumbufu na magonjwa ya mazao ya kilimo husababisha madhara makubwa kiuchumi na kijamii. Katika kilimo, mlipuko wa visumbufu na

magongwa ya mazao ya kilimo huchangia kushuka kwa uzalishaji wa kilimo.

Tatu, usimamizi wa viuwatilifu unaruhusu nchi kuimarisha ubora wa viuwatilifu hivyo ili kulinda vihatari vya kiafya ya binadamu na uharibifu wa mazingira ili kuhakikisha uendelevu wa uwezo wa ardhi kuzalisha.

Nne, utoaji wa msaada kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ambao ni wadau muhimu katika kukuza maendeleo ya kilimo, unapaswa kuangaliwa kwa makini ili kuweza kuendeleza ukuaji wa uchumi kwa kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Wajasiriamali wadogo na wa kati ni uti wa mgongo katika kukuza ajira pamoja na ubunifu. Pia, wao ni muhimu katika kuwezesha mazingira ya biashara za mazao ya kilimo nchini.

Tano, upatikanaji wa pembejeo za kilimo una mchango mkubwa katika kukuza uzalishaji wa kilimo. Msingi wa maendeleo endelevu ya kilimo ni upatikanaji wa pembejeo za kisasa za kilimo kwa wakulima[4]. Uwepo wa pembejeo za kilimo unasaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao na mavuno na kuboresha ubora wa ardhi hivyo kuhakikisha uwepo wa matokeo bora kwa wakulima. Pembejeo za kilimo pia hupunguza vihatarishi vitokanavyo na hali ya hewa na hivyo kupunguza uharibifu wa baada ya mavuno[5]. Mbolea huboresha hali ya udongo, huhuisha naitrojeni, na huzalisha bakteria muhimu kwenye udongo wanaoboresha uzalishaji.

Mwisho kabisa, uwepo na usimamizi wa ujenzi wa skimu za umwagiliaji ni miongoni mwa masuala muhimu katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kusaidia katika kufikia malengo mengine ya masuala ya kilimo. Kwa kuwa teknolojia ya umwagiliaji ni ngumu, usimamizi wake unahitaji wafanyakazi wenye uzoefu na wenye ujuzi. Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha miundombinu ya shughuli za umwagiliaji ina ubora na inakidhi mahitaji ya sekta ya kilimo.

## 2.7 Watendaji Muhimu katika Sekta ya Kilimo Nchini

Kuna wadau mbalimbali na muhimu katika eneo hili la kilimo nchini Tanzania. Wadau hawa wamegawanywa katika makundi makuu matano, ambayo ni wizara za kisekta, taasisi za uangalizi, mashirika ya kimataifa, taasisi za utafiti wa kilimo, na taasisi zinazotoa usaidizi katika sekta ya kilimo.

*Wizara za kisekta:* Hii ni pamoja na Wizara ya Kilimo ambayo ina wajibu wa kusimamia sekta ya kilimo nchini. Miongoni mwa

[4] http://www.mit.go.tz/uploads/documents/sw/1455888762-Agricultural-Marketing-Policy.pdf visited on 16/5/2017
5 https://www.slideshare.net/JitinKollamkudy/agricultural-inputs-46989116

majukumu ya Wizara hii ni kufanya marekebisho ya sera za Serikali pamoja na taratibu za sekta ya kilimo. Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kilimo katika ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa. Tawala za mikoa zina wajibu wa kujenga mazingira mazuri kwa mamlaka za serikali za mitaa ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi; kusaidia mamlaka za serikali za mitaa katika kujenga uwezo; kutoa msaada wa kitaalamu kwa mamlaka za serikali za mitaa; na kufuatilia utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa. Mamlaka za serikali za mitaa (halmashauri za serikali za mitaa) zina jukumu la kuwezesha uratibu wa kitaalamu kati ya wizara za kisekta na wananchi.

*Taasisi za Uangalizi:* Hizi ni pamoja na taasisi kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea Tanzania, Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Chakula na Dawa Tanzania, na Tume ya Usimamizi wa Mazingira. Taasisi hizi za serikali zina wajibu wa kusimamia utendaji wa wakulima kama vile shughuli za kila siku za wakulima, maofisa wa ugani, wauzaji wa mazao ya kilimo, wasindikaji wa mazao ya kilimo, pamoja na wadau wengine wa kilimo.

*Mashirika ya Kimataifa:* Hizi ni pamoja na taasisi kama vile Shirika la Chakula na Kilimo Duniani, pamoja na Benki ya Maendeleo Afrika, ambazo zina wajibu wa kushirikiana katika ufadhili wa wa sekta ya kilimo, kuimarisha mfumo wa taarifa za kilimo, na kusaidia ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za kilimo.

*Taasisi za Utafiti wa Kilimo Tanzania:* Hizi ni pamoja na Taasisi za Utafiti wa Kilimo Tanzania zilizopo nchi nzima. Taasisi hizi zinahusika na utafiti chini ya Idara ya Utafiti na Mafunzo ya Wizaya ya Kilimo. Taasisi hizi pia zina wajibu wa kukuza na kuratibu shughuli za bioteknolojia za kilimo nchini. Wajibu wake ni kukuza utafiti kwa ajili ya maendeleo ya mazao mbalimbali kwenye kanda zao za kilimo nchini Tanzania.

*Taasisi za usaidizi katika sekta ya kilimo:* Hizi ni pamoja na taasisi kama Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia; na Wizara ya Kazi. Wizara hizi kupitia taasisi za mafunzo kama vile vyuo vikuu, na vituo vya mafunzo ya ufundi vina jukumu la kujenga uwezo wa Watanzania kushiriki katika shughuli za kilimo. Kwa upande mwingine, taasisi hizi zina wajibu wa kutekeleza sheria za kazi katika sekta ya kilimo. Wizara ya Fedha na Mipango ina wajibu wa usimamizi wa fedha na kuhakikisha kuna usimamizi sahihi wa mapato yanayotokana na shughuli za kilimo.

**Kaguzi za Ufanisi Zilizofanyika**
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilifanya kaguzi sita za utendaji, na ukaguzi mmoja wa ufuatiliaji katika sekta hii ya kilimo. Nia ya Ofisi ya Ukaguzi ni kuhakikisha kuwa kuna utendaji bora katika maeneo hayo kwa kuzingatia umuhimu wake kwa uchumi wa nchi. Kaguzi za ufanisi zilizofanyika zililenga maeneo yafuatayo:

Utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima; udhibiti wa visumbufu vya mimea na milipuko ya magongwa ya mimea; usimamizi wa viuwatilifu katika shughuli za kilimo; usimamizi wa upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo kwa wakulima; usimamizi wa utoaji wa huduma za usaidizi kwa wajasiliamali wadogo na wa kati nchini; na usimamizi wa shughuli za ujenzi wa miradi ya umwagiliaji nchini.

Matokeo ya kaguzi na mahitimisho yaliyotokana na ripoti sita za ukaguzi pamoja na ripoti ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi yametumika kutoa picha halisi kwa ujumla katika sekta nzima ya kilimo nchini ambayo yameelezwa katika sura zinazofuata za ripoti hii.

# SURA YA TATU

# UPATIKANAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO

## 3.1 Utangulizi

Upatikanaji wa pembejeo za kilimo ni muhimu katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi. Upatikanaji na usambazaji wa pembejeo bora za kilimo nchini hupelekea ongezeko la uzalishaji kwa wakulima na nchi kwa ujumla wake. Pia, pembejeo za kilimo hupunguza athari zinatokana na hali ya hewa hivyo kupunguza uharibifu wa mazao baada ya mavuno.

Sura hii itaangalia mambo yanayohusiana na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kama mbegu, mbolea, na viuwatilifu. Wahusika wakuu katika kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo nchini ni Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu nchini, Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea, Wakala wa Mbegu Bora za Kilimo, na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu. Taasisi hizi zilizopo chini ya Wizara ya Kilimo zinatekeleza majukumu ya kuhakikisha udhibiti na kusaidia upatikanaji na usambazaji wa pembejeo zenye ubora kupitia uzalishaji na usajili wa mbegu, mafunzo, na ukaguzi kwa wazalishaji na wauzaji wa mbegu, mbolea, na viuwatilifu nchini.

Matokeo ya ripoti hii yamegawanyika katika maeneo yafuatayo: kutambua mahitaji halisi ya pembejeo nchini; usambazaji wa pembejeo za kilimo nchini; na ufuatiliaji na tathmini wa usambazaji na upatikanaji wa pembejeo za kilimo nchini. Vipengele vifuatavyo vinaelezea kwa kina juu ya upatikanaji na usambazaji wa pembejeo bora za kilimo nchini.

## 3.2 Utambuzi wa mahitaji halisi ya pembejeo nchini haukufanyiki kwa ufanisi

Hatua za kutambua mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo haukufanyika kwa ufanisi ili kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa kuzingatia mahitaji ya pembejeo ya wakulima. Hatua zilizotumika zilikuwa na mapungufu katika kukusanya taarifa zitakazotumika kwenye mahitaji ya pembejeo.

Hatua zinazotumika kwenye kuandaa mahitaji zinakwamishwa na uwepo wa ushirikishaji wa wadau wachache katika kubainisha mahitaji ya ujumla na hivyo kupelekea utofauti kwenye mahitaji na pembejeo zilizosambazwa nchini.

### 3.2.1 Uwepo wa vyanzo hafifu vya kuandaa mahitaji ya pembejeo za kilimo

Hatua za kuandaa mahitaji ya pembejeo za kilimo zinatakiwa kujumuisha taarifa kutoka vyanzo mbalimbli ili kupata mahitaji halisi ambayo yatajumuisha makundi yote ya pembejeo zinazohitajika nchini. Kwa sasa, njia inayotumika ni kwa kuangalia mahitaji ya pembejeo kwa miaka iliyopita ambayo haitoi taarifa sahihi za mahitaji kwa sababu hazizingatii mabadiliko yanayoweza kutokea kama vile ongezeko la idadi ya wakulima au uwekezaji mpya unaoweza kufanyika kwenye kilimo na kupelekea mabadiliko kwenye mahitaji ya pembejeo za kilimo.

Kwa upande mwingine, haukufanyika utafiti wa kimsingi ili kujua mahitaji kwa kuzingatia sifa za kijiografia kwa kanda za kilimo zilizopo nchini. Ukaguzi wangu ulibaini hadi kufikia mwaka 2018, Wizara ya Kilimo ilishindwa kufanya utafiti wa wa msingi ili kujua mahitaji halisi ya pembejeo kwa wakulima walioko nchini kwa kuzingatia ekolojia na idadi ya wakulima. Utafiti wa msingi husaidia kujua mahitaji halisi lakini ilionekana Wizara ya Kilimo inatumia makadirio tu ili kuweza kupata mahitaji ya wakulima.

Wizara ya Kilimo ilieleza kwamba kufanya utafiti wa msingi kwenye pembejeo za kilimo ni gharama kwa kuzingatia muda na fedha kwa sababu inatakiwa kujumuisha ngazi ya mkulima, kijiji, kata, wilaya, mkoa, na kisha kujumuishwa kitaifa.

Kuhusu mbolea, Mamlaka ya Mbolea Tanzania kupitia manunuzi ya jumla ya mbolea, inatakiwa kutambua mahitaji halisi ya mbolea ili kuweza kusaidia manunuzi ya mbolea hiyo itakayotumika nchini. Kwa sasa mbolea inayosambazwa nchini haizingatii hali ya uhitaji wa udongo katika maeneo mbalimbali nchini.

Ilibainika pia hakukufanyika utafiti wa msingi ili kujua ustahimilivu wa mbegu kwa kuzingatia kanda mbalimbali za kilimo nchini. Mbegu zinazoingizwa nchini zinategemea mfumo wa nguvu ya soko kwa kuzingatia kanuni ya mahitaji na usambazaji. Wafanyakazi kutoka Wizara ya Kilimo walieleza kwamba mchakato wa kutambua mahitaji ya mbegu haufanyiki kwa ufanisi kwa sasa nchini.

Kwenye viuwatilifu ilionekana pia kuwa zaidi ya silimia 90 ya viuwatilifu vinavyotumika nchini vinaingizwa kutoka nje ya nchi. Uagizaji wa viuwatilifu vinavyohitajika unazingatia zaidi nguvu ya soko na kanuni ya mahitaji na usambazaji. Pia, hakuna utafiti wa msingi uliofanywa na Wizara ya Kilimo ili kuweza kusaidia uingizaji wa viuwatilifu nchini.

Kutofanyika kwa mchakato wa kutambua mahitaji halisi ya pembejeo nchini huathiri uzalishaji wa mazao kwa sababu wakulima hushindwa kuchagua pembejeo tofauti zenye kusaidia maeneo yao ya kilimo.

### 3.2.2 Kutofanyika vizuri kwa mchakato wa kutambua mahitaji ya pembejeo


Ili kuweza kupata kiasi sahihi cha mahitaji ya pembejeo za kilimo nchini, kunahitajika kuwepo kwa mbinu sahihi za kutambua mahitaji husika. Kwa sasa, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu; Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea; na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu hazitumii mbinu sahihi za kutambua mahitaji ya pembejeo za kilimo.

Hakuna mfumo, programu, au njia nyingine sahihi ya kuwezesha kutambua mahitaji sahihi ya pembejeo za kilimo nchini. Hakuna mfumo sahihi unaotumiwa na Wizara ya Kilimo ili kutathmini taarifa zinazohusiana na pembejeo za kilimo nchini. Wizara ya Kilimo ina mpango wa kuanzisha mfumo rasmi unaoitwa Mfumo wa Taarifa za Pembejeo utakaosaidia kutambua mahitaji sahihi ya pembejeo nchini. Mfumo huu pia utatunza takwimu zitakazoonesha pembejeo zilizohitajika na zilizotumika nchi nzima.

Kwa upande mwingine, kumekuwepo na kutoshirikishwa kwa watendaji wote wanaohitajika kujumuishwa kwenye mchakato wa kutambua mahitaji. Ili kupata mahitaji sahihi, kunahitajika kujumuishwa kwa watendaji wote kuanzia ngazi ya mkulima, kijiji, kata, wilaya, hadi mkoa. Pia, kunahitajika ushirikishaji wa wakulima kila mwaka ili kupata mahitaji halisi ya pembejeo kama mbegu na mbolea zinazohitajika na wakulima.

Ukaguzi ulibaini kutoshirikishwa kwa wakulima wakati wa mchakato wa kutambua mahitaji ya pembejeo nchini hivyo kupelekea mahitaji kutojumuisha aina za pembejeo zinazokidhi kanda mbalimbali za kilimo. Timu yangu ya ukaguzi ilitembelea halmashauri nne na ilibaini kukosekana kwa maofisa ugani kwenye vijiji au kata. Hali hii huathiri uwasilishaji wa taarifa sahihi za mahitaji ya pembejeo. Aidha, hali hii hupelekea kukosekana kwa pembejeo zinazohitajika nchini kama vile mbolea aina ya *Sulphate Manganeseine* na mbegu aina za *SEEDCO 719*, *Nitrable*, na *MOP*. Pia, ilibainika pembejeo zinazotumika nchini hazitoshelezi mahitaji ya pembejeo zenye ubora. **Vielelezo 3.1** na **3.2** vinaonesha utofauti wa mahitaji ya pembejeo na pembejeo zilizosambazwa.


**Kielelezo 3.1: Ulinganishi kati ya mahitaji ya mbolea na mbolea zilizosambazwa**




**Chanzo:** *Ripoti ya Bajeti za Wizara ya Kilimo kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18*

**Kielelezo 3.1** hapo juu kinaonesha utofauti mkubwa kati ya kiasi cha pembejeo kilichohitajika na kilichopatikana na pengo limekuwa likiongezeka miaka ya karibuni. Kwa mfano, usahihi wa makadirio ya mahitaji ya mbolea yamekuwa ukipungua kuanzia mwaka 2013/14 na kwa mwaka 2016/17 mbolea iliyosambazwa ilikuwa ni tani 278 wakati mahitaji yalikuwa ni tani 485 sawa na asilimia 57 tu ya mahitaji.

**Kielelezo 3.2: Ulinganishi kati ya mahitaji ya mbegu na mbegu zilizosambazwa**




**Chanzo:** *Ripoti ya Bajeti za Wizara ya Kilimo kuanzia Mwaka 2013/14 hadi 2017/18*

**Kielelezo 3.2** kinaonesha kutobadilika kwa mahitaji ya mbegu kwa kipindi cha miaka minne iliyopita. Hii inaonesha kutofanyika kwa mchakato wa kutambua mahitaji ya pembejeo kwa mbinu bora na

badala yake hutumia takwimu za miaka iliyopita ili kupata mahitaji yajayo ya pembejeo. Pengo kubwa lilitokea katika kipindi cha mwaka 2013/14 na 2014/15 ambapo mahitaji ya mbegu yalikadiriwa kuwa tani 120,000, ambapo mbegu zilizosambazwa zilikuwa tani 11,000 tu. Usahihi wa makadirio ya mbegu umekuwa ukiongezeka kwa kiwango kidogo. Pengo lilikuwa likipungua kwa kasi ndogo hadi mwaka 2016/17 ambapo usambazaji wa mbegu ulifikia asilimia 27 ya mahitaji.

Kwa upande mwingine, makadirio ya viuwatilifu yameongezeka kutoka asilimia 12 ya mwaka 2013/14 hadi kufikia asilimia 58 mwaka 2015/16. Hata hivyo, usambazaji wa viuwatilifu bado uko chini ikilinganishwa na mahitaji hivyo kupelekea usambazaji hafifu wa viuwatilifu. Hii imesababisha wakulima kushindwa kupambana na magonjwa ili kuongeza uzalishaji. Katika kipindi cha miaka 4 iliyopita, wastani wa usambazaji wa pembejeo za kilimo kama mbegu, mbolea, na viuwatilifu umefikia asilimia 39 ya mahtaji yote ya pembejeo nchini.

### 3.2.3 Uwasilishaji wa ripoti za mahitaji ya pembejeo hazihakikishi upatikanaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo

Ukaguzi ulibaini kuwa mchakato wa kutambua mahitaji hauwajumuishi wakulima vijiji wanaotakiwa kujua aina tofauti za pembejeo za kilimo na maofisa ugani wa vijiji ambao hutakiwa kujumuisha mahitaji ya pembezejeo katika vijiji vyao. Maofisa ugani wa kata wanatakiwa kujumuisha mahitaji kutoka kwenye vijiji na kuziwakilisha kwenye halmashauri ambao huwasilisha kwenye ngazi ya mkoa mwezi Juni katika kipindi cha uwasilishaji wa ripoti za mwaka za utekelezaji. Kwenye ngazi ya mkoa hujumuisha mahitaji kutoka kwenye halmashauri na kuziwakilisha Wizara ya Kilimo yenye jukumu la kutambua mahitaji halisi ya nchi nzima.

*Kwenye mbolea:* Wafanyakazi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea walifafanua kuwa kumekuwa na ucheleweshaji wa taarifa za mahitaji kutoka halmashauri hivyo kupelekea kutojumuishwa kwa baadhi ya taarifa kwenye mahitaji ya jumla ya mbolea inayotarajiwa kununuliwa nchini. Kwa mfano, Mkoa wa Rukwa mahitaji huandaliwa mwezi wa 6 kwa kujuishwa kwenye taarifa za mwaka na msimu wa kilimo huanza mwezi Agosti. Muda unaotumiwa kwenye uagizaji au uzalishaji na usambazi wa mbolea nchini hauhakikishi uwepo wa mbolea iliyohitajika kabla ya kuanza kwa msimu mwezi Agosti.

*Kwenye mbegu na viuwatilifu:* Taarifa za mahitaji kutoka halmashauri zinaonesha uwasilishaji wa mahitaji hufanyika mwezi Juni kila mwaka. Kutokana na utofauti katika kuanza kwa misimu ya

kilimo, kipindi tajwa hakioneshi uhalisia wa kuwahi kufika kwa pembejeo kabla ya kuanza kwa msimu kwenye baadhi ya mikoa.

### 3.3 Usambazaji Duni wa Pembejeo za Kilimo

Mfumo wa usambazaji haufanyi kazi vizuri kuhakikisha usambazaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo kwa wakulima. Mfumo wa usambazaji unategemea zaidi sekta binafsi ambapo wazalishaji au waagizaji husambaza pembejeo zao kupitia wasambazaji wa ndani na wauzaji wa pembejeo za kilimo. Mfumo wa usambazaji una mapungufu katika maeneo ya usambazaji kwa wakati, pembejeo bora, na udhibiti wa bei hivyo kuathiri tija ya uwepo wa mfumo imara wa usambazaji wa pembejeo kwa wakulima. Vipengele vifuatavyo vinabainisha mapungufu yaliyoonekana kwenye usambazaji wa pembejeo za kilimo

#### 3.3.1 Kutosambazwa kwa wakati kwa mbegu, mbolea, na viuwatilifu

Kupitia mahojiano na wafanyakazi kutoka Ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea na Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu nchini ilibainika kuwa pembejeo hutakiwa kuwepo nchini mwezi mmoja kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo. Katika halmashauri zilizotembelewa, ukaguzi ilibaini ucheleweshaji wa mbegu, mbolea, na viuwatilifu kwa kati ya miezi mitatu hadi mitano baada ya kuanza kwa msimu. Ucheleweshaji wa pembejeo ulitokea sana kipindi cha usambazaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima. Katika ukaguzi wa usambazaji wa pembejeo za kilimo, yafuatayo yalibainika:

**a) Kwenye mbegu na mbolea**

Katika msimu wa mwaka 2015/16, Wizara ya Kilimo ilitumia mfumo wa vocha kusambaza mbegu na mbolea nchini. Kulikuwa na ucheleweshaji wa vocha za pembejeo zilizotumika kusambazia pembejeo kwa wakulima. Miundombinu hafifu ilichangia kwenye kuongeza gharama za usambazaji wa pembejeo ambapo gharama hizo huwaathiri wakulima nchini.

Kutosambazwa kwa wakati pembejeo pia husababishwa na uwezo mdogo wa wazalishaji wa pembejeo wa ndani kuzalisha pembejeo za kilimo nchini. Uzalishaji wa ndani husaidia upatikanaji kwa wakati wa pembejeo ikilinganishwa na uingizaji wa pembejeo kutoka nje ambao huchukua muda mrefu kwa sababu inajumuisha mchakato wa manunuzi, usafirishaji, na usambazaji mikoani kutokea kwenye mipaka ya kuingilia nchini.

Hata hivyo, ilibainika kuwa uwezo wa kuzalisha na kusambaza pembejeo si wa uhakika. Hayo yalionekana kutokana na uwezo mdogo wa Wakala wa Mbegu katika kuzalisha na kusambaza mbegu bora kwa wakati. Uwezo wa Wakala wa Mbegu katika kuzalisha

mbegu hauhakikishi usambazaji wa mbegu bora kwa wakati kwa wakulima nchini. Pia, uwezo wa Wakala wa Mbegu wa kuzalisha mbegu hauhakikishi utoshelevu wa mahitaji ywa mbegu bora nchini. Wakala wa Mbegu ulilenga kuzalisha asilimia 30 ya mbegu bora zinazohitajika nchini kila mwaka. Kwa kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2017/18, Wakala wa Mbegu uliweza kuzalisha kwa kiwango cha juu msimu katika msimu wa mwaka 2017/18 tu ambapo ulizalisha asilimia 2.2 ya malengo waliyojiwekea ya kuzalisha tani 36,000.

Uzalishaji mdogo wa mbegu bora wa Wakala wa Mbegu ni matokeo ya kukosekana kwa mashamba ya mbegu yenye tija. Ilibainika kwamba ni shamba moja tu la mbegu kati ya mashamba tisa yanayozalisha mbegu nchini ndilo lina uwezo wa kuzalisha mbegu katika kipindi cha mwaka mzima. Shamba hilo pekee ndilo limewekewa mfumo wa umwagiliaji wakati mashamba mengine 8 hutegemea mvua katika kuzalisha mbegu. Pia, kulionekana kuna matumizi madogo ya ardhi inayofaa kuzalisha mbegu kwenye mashamba ya Wakala wa Mbegu. Kati ya hekari 8,500 za ardhi inayofaa kwa kilimo, ni hekari 4020 sawa na asilimia 47 tu ndiyo zinatumiwa kuzalisha mbegu zinazohitajika nchini.

Uzalishaji mdogo wa mbegu iliongeza upungufu wa mbegu bora zinazohitajika na wakulima nchini hivyo kupelekea kutumia mbegu zisizo na kiwango ambazo hazihakikishi ongezeko la uzalishaji wa mazao ya kilimo.

**b) Kwenye Viuwatilifu**

Kumekuwa na kutofikishwa kwa wakati kwa viuwatilifu vinavyotumika nchini kupitia vyama vya ushirika vya mazao. Hali hii ilithibitishwa na kukosekana kwa viuwatilifu nchini. Kwa mfano, Bodi ya korosho ilisambaza zaidi ya tani 12,000 za viuwatilifu kwa wakulima nchini mwaka 2017/18 lakini kulitokea uhaba wa pembejeo kwenye maeneo ya mkoa wa Mtwara. Zaidi ya asilimia 90 ya viuwatilifu vinavyotumika nchini huagizwa kutoka nje ya nchi.

Viuwatilifu vinatumika sana kwenye mazao ya biasahara kama korosho, pamba, na tumbaku. Kukosekana kwa viuwatilifu hupelekea wakulima kukosa pembejeo bora kwa wakati hivyo kutumia viuwatilifu vinavyopatikana hata kama ni vya ubora mdogo na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo.

### 3.3.2 Usambazaji wa pembejeo zisizo na ubora, bandia, zisizothibitishwa, na zisizofaa kulingana na mazingira

Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu nchini, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu zinatakiwa kuhakikisha usambazaji wa pembejeo zenye ubora kama mbegu, mbolea, na viuwatilifu nchini.

**(a) Mbegu**
Ukaguzi ulibaini uwepo wa mbegu ambazo hazikuwa na uwezo wa kuota kama Pioneer 2859, DKC 90-89, SC 627, na SC 403. Pia, kulikuwa na usambazaji wa mbegu ambazo zinaota lakini hazitoi mazao kama ilivyotarajiwa kama vile Pioneer 3253 na SC 625. Aidha, kulikuwa na usambazaji wa pembejeo ambazo hazikujaribiwa tena baada ya kipindi chake cha miezi 7 cha majaribio kupita. Hii pia ilisababishwa na kutofanyika kwa ukaguzi kwa wauzaji, mashamba ya kuzalishia mbegu, na kwenye mipakani.

**(b) Mbolea na viuwatilifu**
Mbolea inayosambazwa nchini haizingatii virutubisho vinavyopatikana kwenye udongo. Pia, kumekuwa na usambazaji wa viuwatilifu kinyume na sheria nchini. Usambazaji huo ulibainika kuwepo kwenye viuwatilifu kama Kumulus, Mo – Karatep, Movil, Mo–Durs, Movor, Quickphos, Aminne, na Mocron 720 EC. Pia, ilibainika wauzaji wa pembejeo walikuwa wakifungua vifungashio na kuuza mbolea au viuwatilifu kwenye vipimo vidogovidogo. Picha zifuatazo zinaonesha vifungashio vya mbegu na mbolea vilivyofunguliwa kutoka kwenye vifungashio vya awali kisha kufungashwa upya kwenye vifungashio vidogovidogo.

**Picha 3.1: Vifungashio vya mbolea na viuwatilifu vilivyofunguliwa katika halmashauri zilizotembelewa kipindi cha ukaguzi**



**Chanzo:** *Uchunguzi wa wakaguzi Novemba 2018 na Februari 2019*

**Picha 3.1** zinaonesha kufunguliwa kwa vifungashio vya viuwatilifu katika Wilaya ya Morogoro Vijijini na kufunguliwa kwa mbolea katika Wilaya ya Hai. Madhara ya kufungua vifungashio vya mbolea na viuwatilifu ni kupungua kwa ufanisi kwa pembejeo hizo kipindi zitakapokuwa zinatumika mashambani. Kusambazwa kwa pembejeo

zenye ubora mdogo hupunguza uzalishaj wa mazao ya kilimo na hivyo kuleta upungufu wa kipato kwa wakulima na nchi kwa ujumla.

### 3.3.3 Bei za juu za pembejeo nchini

Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013 inaitaka Wizara ya Kilimo kuhakikisha wakulima wanapatiwa pembejeo bora. Wakulima kutoka kwenye halmashauri zilizotembelewa kipindi cha ukaguzi walieleza kuwa bei ya pembejeo za kilimo iko juu. Hii ilisababishwa na Serikali kushindwa kutekeleza makubaliano ya utoaji ruzuku kwa wakulima. Ilibainikika makubaliano yalikuwa ni kulipia asilimia 50 ya gharama za pembejeo (Sh. 200,000) kama ruzuku. Hata hivyo, ilibainika kwamba Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 78,500 kama mchango wake ambacho ni sawa na asilimia 39 ya gharama za pembejeo. Hivyo, wakulima walitakiwa kuchangia asilimia 61 badala ya asilimia 50 ya bei ya soko.

Pia, gharama za kununulia pembejeo zilikuwa zikikaribiana na kipato ambacho mkulima hukipata kutokana na kuuza mazao yake ya kilimo mwishoni mwa mwaka 2018. Ilikadiriwa kuwa hekta moja huweza kuzalisha wastani wa magunia 10 ya mahindi; na kama kila gunia litauzwa kwa bei ya soko ya 30,000, mkulima angepata jumla ya shilingi 300,000/=. Jumla ya gharama za kununua pembejeo ni kiasi kinachokadiriwa kufikia shilingi 200,000=/ ambacho ni asilimia 67 ya kipato cha mkulima.

Iligundulika pia wakulima walikosa nafasi za kupata mikopo rasmi ambayo ingewawezesha kununua pembejeo katika kipindi cha msimu wa kilimo. Mikopo iliyotolewa ilihitaji wakulima kuweka dhamana mali na kwenye umoja wa vikundi vya wakulima. Ukaguzi pia ulibaini uwepo wa riba ya kiasi cha asilimia 20 kwa mwaka kwenye mikopo inayotolewa ambayo ni gharama kwa wakulima. Hali hii iliwanya wakulima kuchagua pembejeo za kilimo ambazo za gharama nafuu ambazo hazina ubora na kupelekea kutopata mavuno mengi.

### 3.3.4 Kukosekana kwa njia sahihi za kusimamia bei za pembejeo za kilimo nchini

Kumekuwa na kukosekana kwa njia za kusimamia bei za pembejeo bora za kilimo nchini kama inavyoelezewa hapa chini.


**Kwenye Mbolea**

Kifungu cha nne cha Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009 kinaitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kusimamia bei ya mbolea kwa namna nzuri. Ukaguzi ulibaini kuwa taarifa za bei elekezi zimekuwa haziwafikii watoataarifa na wahusika kama inavyohitajika kufika kwenye ngazi ya mkoa, halmashauri, kata, na kijiji.

Ripoti za ukaguzi wa maduka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea zilionesha baadhi ya wauzaji wa pembejeo kwenye halmashauri hawana taarifa juu ya bei elekezi. Pia, wakulima walionekana kutofahamu juu ya bei elekezi ya mbolea ambapo ni asilimia 17 tu wakulima waliohojiwa ndiyo walikuwa na uelewa juu ya bei elekezi. Kupitia mfumo wa manunuzi ya jumla ya mbolea, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea hutakiwa kufanya ukaguzi ili kuweza kuhakikisha wauzaji wa mbolea wanafuata bei elekezi iliyopangwa.

Ilibainika kutofanyiwa kwa kaguzi mara kwa mara kwa wauzaji wa mbolea hupelekea wauzaji wa mbolea kuuza mbolea kwa bei ya juu zaidi ya bei elekezi. Pia, ilibainika kuwa ni mikoa michache tu ndiyo huweza kufanyiwa ukaguzi kwa wauzaji wa pembejeo. **Kiambatisho 3.3** kinaonesha asilimia ya mikoa ambayo haikufanyiwa kaguzi na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kati ya mwaka 2013/14 na 2017/18.

**Kielelezo 3.3: Asilimia ya mikoa ambayo haikukaguliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kati ya mwaka 2013/14 na mwaka 2017/18**




**Chanzo:** *Taarifa za mwaka za mipango na utekelezaji kuanzia 2013/14 hadi 2017/18*

**Kielelezo 3.3** kinaonesha ongezeko la mikoa iliyokaguliwa nchini kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18. Pia, ilionekana mikoa isiyokaguliwa ilipungua kwa kiwango kidogo kukiwa na ongezeko la dogo la mikoa inayokaguliwa. Idadi ya mikoa isiyokaguliwa ilipungua kutoka asilimia 76 mwaka 2013/14 hadi kufikia asilimia 68 mwaka 2017/18. Hali hii ilisababishwa na ongezeko la fedha zinazotengwa na kutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Kukosekana kwa ukaguzi husababisha wauzaji wa mbolea kuuza mbolea kwa bei ya juu zaidi ya bei elekezi. Ripoti za ukaguzi zilionesha kuwa kuna baadhi ya wauzaji hupandisha bei hadi kufikia asilimia 33 zaidi ya bei elekezi.

**Kwenye mbegu na viuwatilifu**

Kwa sasa hakuna mfumo rasmi wa kuhakikisha usimamizi wa bei elekezi kwenye mbegu na viuwatilifu zinavyouzwa nchini. Ukaguzi ulibaini baadhi ya mbegu zinazozalishwa nchini huuzwa kwa bei ndogo ikilinganishwa na bei ya soko. Hii inatokea kwenye Wakala wa Mbegu za Kilimo, ambao hupata ruzuku kutoka serikalini na kufidia baadhi ya gharama za uzalishaji na uendeshaji. Viuwatilifu vinavyotumika kuzuia visumbufu na magonjwa kwenye pamba, tumbaku, na korosho hutolewa kwa ruzuku na kusambazwa kwa wakulima waliopo kwenye vyama vya msingi vya mazao.

### 3.3.5 Uwepo wa wauzaji wa pembejeo wasiokidhi viwango vya kusambaza pembejeo za kilimo nchini

Ukaguzi ulibaini pia uwepo wa wauzaji wa pembejeo ambao hawakukidhi viwango vya kusajiliwa na kufanya biashara ya mbegu, mbolea, na viuwatilifu nchini kama inavyoelezwa hapa chini.

***Wauzaji wasiokidhi viwango vya usajili***
Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009, Sheria ya Mimea ya Mwaka 1997, na Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 zinamtaka muuzaji yoyote wa pembejeo kufanyiwa usajili kabla ya kuanza biashara ya pembejeo. Kwenye mikoa iliyotembelewa wakati wa ukaguzi, ilibainika uwepo wa wauzaji wasiosajiliwa; wanaofanya biashara kinyume na sheria; wasiothibitishwa kufanya biashara; na wauzaji wa pembejeo wa msimu.

Wauzaji wa msimu walionekana Mkoa wa Mbeya, ambapo katika ukaguzi uliofanyika mwaka 2014/15 kwa wakulima 37, ilibainika wakulima 19 sawa na asilimia 51 walikuwa wauzaji wa msimu wa pembejeo. Pia, ilibainika wauzaji wengi wa pembejeo huuza pembejeo zao kwenye masoko ya mnada ya kila wiki kwenye halmashauri zao husika. Picha nammba 3.2 inaonesha uuzaji wa pembejeo sehemu za wazi kinyume na sheria zinazosimamia ubora wa pembejeo.

**Picha 3.2: Uuzaji wa pembejeo maeneo ya wazi katika mnada**



**Chanzo:** *Tathmini ya wakaguzi Januari, 2018*

**Picha 3.2** inaonesha viuwatilifu na mbolea ya maji ikiwa inauzwa kwenye mnada wa kila wiki na muuzaji ambaye hajasajiliwa na ambaye hajapatiwa mafunzo ya matumizi ya mbolea au viuwatilifu. Alipoombwa kutoa maelekezo, muuzaji hakuweza kumuelezea mkulima juu ya matumizi.


Uwepo wa urasimu katika taratibu za usajili na gharama za juu za usajili ni moja ya sababu zilizotajwa kupelekea baadhi ya wauzaji kushindwa kujisajili kwenye mamlaka husika. Hali hii inapelekea kuendelea kusambaza kwa pembejeo zilizo chini ya kiwango na wauzaji wasiozingatia uhifadhi bora wa pembejeo kama ilivyoonekana kwenye Picha 3.2.

***Wauzaji wasiokuwa na mafunzo ya pembejeo na elimu ya kilimo***
Sheria ya Afya ya Mimea ya Mwaka 1997 na Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 zinamtaka muuzaji wa pembejeo kuwa na elimu, uwezo, na

vifaa vyenye tija ili kutoshusha viwango kwa pembejeo na mbegu kutopungua uwezo wa kuota. Katika halmashauri zilizotembelewa na timu ya ukaguzi ilibainika kulikuwa na wauzaji wa pembejeo wasiokuwa na ujuzi wa kilimo, na ambao hawajapatiwa mafunzo na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu nchini. Hii hupelekea wauzaji kushindwa kutoa maelezo ya matumizi sahihi ya pembejeo kwa wakulima.

Ilibainika pia kuwa katika Halmashauri za Kalambo na Masasi, asilimia 80 ya wauzaji wa pembejeo waliotembelewa walionekana kutokuwa na elimu ya kilimo kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 3.4**.

**Kielelezo 3.4: Asilimia ya wauzaji wa pembejeo wasiokuwa na mafunzo na elimu ya kilimo**




**Chanzo:** *Tathmini kutoka kwa wakaguzi, 2018*

Uwepo wa wauzaji wa pembejeo wasiokuwa na elimu ya pembejeo za kilimo hupelekea kushindwa kutoa ushauri kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya pembejeo.

### 3.3.6 Idadi ndogo ya wauzaji wa pembejeo nchini

Ili kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo nchini ni lazima kuwepo na wazalishaji wa ndani, waagizaji, wasambazaji, na wauzaji wa kutosha watakaouza pembejeo nchini. Ukaguzi ulibaini hakuna usawa katika uwepo wa wauzaji na wasambazaji kwenye mikoa iliyopo nchini hivyo kupelekea kutopatikana au kuchelewa kufika kwa pembejeo zinazohitajika.

Pia, ilibainika kuwa uagizaji wa mbolea na viuwatilifu umefikia asilimia 90 lakini mbegu uagizaji wake ni chini ya asilimia 40. Kumekuwepo na changamoto katika kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo nchini. Changamoto hizo zinatokana na ukubwa wa

maeneo na idadi kubwa ya wakulima wanaohudumiwa na wauzaji wa pembejeo nchini.

***Idadi ndogo ya wauzaji na wasambazaji ikilinganishwa na wakulima waliopo***

Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu nchini zina jukumu la kuhakikisha kuna usimamizi wa pembejeo zilizosambazwa kwa wakulima nchini. Katika mikoa minne iliyotembelewa kipindi cha ukaguzi, ilibainika kuwa kwa wastani muuzaji mmoja anahudumia wakulima 42,000; na msambazaji mmoja anahudumia wastani wa vijiji 792 kwenye mkoa. Pia, ilibainika katika halmashauri 16 zilizopo kwenye mikoa minne (4) hazikuwa na wasambazaji.

***Idadi ndogo ya wauzaji na wasambazaji ikilinganishwa na ukubwa wa maeneo wanayoyahudumia***

Kwenye mikoa iliyotembelewa wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa wauzaji na wasambazaji walikuwa wanapatikana baada ya umbali mkubwa na hawakuweza kusambaza na kuuza pembejeo kwa watu wote kwenye mikoa husika. Ilibainika pia muuzaji mmoja alihudumia eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 643; na msambazaji mmoja alihudumia eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 17,000. Hali hii ilipelekea wakulima kutumia umbali kati ya kilomita 20 hadi 100 kutafuta pembejeo bora za kilimo. Hii inatokana na baadhi wauzaji kutopatikana kwenye maeneo ya mbali kutoka makao makuu ya halmashauri.

## 3.4 Ufuatiliaji na Tathmini kwenye Upatikanaji wa Pembejeo Nchini

Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013 inaitaka Wizara ya Kilimo kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za kilimo nchini zinazotolewa na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu nchini na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea. Kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji cha Idara ya Sera na Mipango ya Wizara ya Kilimo ndiyo yenye jukumu la kufanya kazi hii.

### 3.4.1 Wizara Kilimo kufanya ufuatiliaji na tathmini hafifu kwa Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu nchini na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea

Ilionekana kumekuwa na udhaifu kwenye ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha kuna upatikanaji wa pembejeo nchini. Wizara inatakiwa kufanya ufuatiliaji mara nne kwa mwaka katika Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu nchini na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea. Kwa kufanya hivyo, Wizara ya Kilimo ingeweza kugundua viashiria muhimu vitakavyotumika kupima utekelezaji wa majukumu. Viashiria hivyo muhimu ni kama kutumia mbinu bora za

kilimo (inajumuisha matumizi ya mbegu na mbolea bora), idadi ya maofisa ugani nchini, na jumla ya gharama za utafiti katika kilimo.

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, ilibainika kuwa ufuatiliaji na tathmini kwenye maeneo ya kata ya kujifunzia mbinu za kilimo ulifanyika mwaka 2018. Tathmini kwenye mbegu na mbolea hazipewi kipaumbele na Wizara ya Kilimo katika ufuatiliaji wake. Kutofanyika mara kwa mara kwa ufuatiliaji na tathmini kunatokana na Wizara ya Kilimo kushindwa kutoa kipaumbele kwenye eneo hilo.

### 3.4.2 Tathmini na ufuatiliaji hafifu wa Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu kwenye usambazaji Mbegu

Kumekuwa na ufuatiliaji hafifu wa Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu katika kanda zake zilizopo nchini na wakaguzi wa mbegu walioko kwenye halmashauri katika kutekeleza majukumu yao ya kikaguzi.

***Kutofanyika kwa tathmini na ufuatiliaji kwenye kanda za* Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu**

Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu ina kanda nne ambazo ni Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Mashariki, na Kanda ya Ziwa. Ilibainika kuwa hakukufanyika ufuatiliaji na tathmini wa Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu katika kanda zake kuhusu utoaji wa huduma za kuhakikisha ubora wa mbegu kupitia ukaguzi kwa wauzaji wa mbegu, mashamba ya mbegu, na maeneo ya mipakani. Sababu za kutokufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini ni:

a) Kukosekana kwa miongozo ya ufuatiliaji na tathmini. Ilibainika kuwa hakukukuwepo miongozo ya kufanyia tathmini na ufuatiliaji ili kupima utendaji wa ofisi za kanda za Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu.
b) Kukosekana kwa mipango ya ufuatiliaji na utathmini. Ilibainika hakukuwa na mipango ya kutathmini na kufuatilia utendaji wa ofisi za kanda za Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu.

Hivyo, kukosekana kwa ufuatiliaji na tathmini hupelekea kushindwa kugundua changamoto zinazozikumba ofisi za kanda za Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu katika kutekeleza majukumu yake.

***Kutofanyika kwa tathmini na ufuatiliaji kwenye halmashauri***

Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu pia haikufanya tathmini na ufuatiliaji kwa wakaguzi wa mbegu waliopo kwenye halmashauri nchini. Hii ilitokana na kukosekana kwa makubaliano ya kiutendaji. Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu iliwafanyia mafunzo wafanyakazi wa halmashauri na kuwapa hadhi ya kuwa wakaguzi wa mbegu ili kuisaidia Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu tekeleza shughuli za kikaguzi kwenye halmashauri husika. Ilibainika hakukuwa na mfumo wa uwasilishaji wa taarifa za kiutendaji kutoka kwa wakaguzi hao wa halmashauri. Kukosekana

kwa mipango na miongozo ya kufanya tathmini kwa wakaguzi wa mbegu wa halmashauri hupelekea kutotambua changamoto wanazokutana nazo wakaguzi wa mbegu walioko kwenye halmashauri.

### 3.4.3 Tathmini na ufuatiliaji hafifu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea

Ilibainika kukosekana kwa mfumo wa kutuma ripoti za kiutendaji kutoka kwa wakaguzi wa mbolea waliopo kwenye halmashauri ijapokuwa wakaguzi hawa hushirikishwa na wakaguzi wengine Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea katika ukaguzi kwa wauzaji wa pembejeo.

Kukosekana kwa miongozo ya ukaguzi ndiyo sababu inayopelekea kutofanyika kwa ufuatiliaji na tathmini kwa wakaguzi wa mbegu walioko kwenye halmashauri. Aidha, kukosekana kwa mipango ya kupima utendaji kwa wakaguzi wa mbolea walioko kwenye halmashauri huchangia kutofanyika kwa ufuatiliaji na tathmini. Hali hii husababisha kutokuwepo kwa njia ya kupima utendaji kazi wa wakaguzi wa mbolea walioko kwenye halmashauri. Pia, husababisha kutotambua kwa wakati changamoto zinazowakuta wakaguzi wa halmashauri.

# SURA YA NNE

## UDHIBITI WA UBORA KWENYE PEMBEJEO ZA KILIMO

### 4.1 Utangulizi
Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi wa usimamizi wa udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo. Pembejeo za kilimo zinazoelezewa katika sura hii ni viuwatilifu, mbegu, na mbolea.

Matokeo ya ukaguzi huu yamewekwa katika makundi yanayohusisha, usajili wa pembejeo na wauzaji wa pembejeo za kilimo; ukaguzi wa wauzaji wa pembejeo za kilimo; na utoaji wa elimu ya matumizi sahihi na utunzaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima na wauzaji wa pembejeo za kilimo. Ripoti tatu za ukaguzi zimetumika katika kutoa matokeo ya utekelezaji wa shuguli za udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo. Ripoti hizo zinajumuisha:

- Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Viuwatilifu kwenye Shughuli za Kilimo;
- Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo; na
- Ukaguzi wa Ufanisi katika Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima.

Wahusika wakuu kwenye kaguzi zote tatu zilizohusiana na Udhibiti wa Ubora kwenye Pembejeo za Kilimo ni Wizara ya Kilimo, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viutailifu, Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu; na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Nchini.

### 4.2 Usajili Hafifu wa Pembejeo na Wauzaji wa Pembejeo za Kilimo
Kupitia mahojiano na maofisa wa Wizara ya Kilimo, ilibainisha kuwa kulikuwa na mapungufu kwenye utekelezaji wa shughuli za usajili wa pembejeo za kilimo. Hali hii ilijidhihirisha kwa uwepo sokoni wa pembejeo za kilimo ambazo hazikusajiliwa; na uwepo wa wauzaji wa pembejeo ambao hawakusajiliwa.

#### 4.2.1 Usajili hafifu wa viuwatilifu
Mapitio ya taarifa kutoka Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu yameonesha kwamba usajili wa viuwatilifu ulikuwa hafifu. Hii ilisababishwa na utekelezaji hafifu wa shughuli zinazohusu usajili wa viuwatilifu.

### *i. Utekelezaji hafifu wa tathmini za afya na mazingira*

Iliripotiwa kuwa Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu haijafanya tathmini za kutosha za afya na mazingira ili kuhakikisha usalama wa viuwatilifu vinavyosambazwa nchini. Pia, iliripotiwa kuwa kabla ya kusajili viuwatilifu, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu huwa inafanya tathmini ya kubaini kiwango cha sumu kwenye viuwatilifu kwa lengo la kuhakikisha viuwatilifu vinavyosajiliwa ni salama kwa matumizi.

Iliripotiwa zaidi kwamba baada ya usajili wa viuwatilifu, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu huwa inafanya tathmini ya kiafya kwa wakulima ili kuweza kubaini kiwango cha sumu itokanayo na viuwatilifu kwenye miili ya wakulima.

Timu ya ukaguzi ilifanya mapitio ya Ripoti ya Ufuatiliaji wa Usalama wa Wakulima ya Mwaka 2015 iliyoandaliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kwa lengo la kubaini kiwango cha utekelezaji wa tathmini za afya zilizofanywa kwa wakulima. Kwa mujibu wa ripoti hizo, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu ilifanya jitihada ndogo katika utekelezaji wa tathmini za afya kwa wakulima ili kuweza kubaini vihatarishi vya kiafya. Hii ilitokea licha ya kuwa na ongezeko la matumizi ya viuwatilifu kwa wakulima nchini na kutokea kwa matukio ya wakulima kuathirika na sumu zitokanazo na viutilifu.

Mapitio ya ripoti ya ufuatiliaji yalionesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu toka 2015 hadi 2017, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu iliweza kufanya tathmini ya kiafya kwa wakulima 992 tu. Miongoni mwa wakulima hao 992, wakulima 359 sawa na asilimia 36 walibainika kuwa na kiwango cha sumu cha *cholinesterase* chini ya kiwango kinachokubalika cha 24.5 U/G.

Ilibainika zaidi kuwa wakulima wadogo ambao wanakadiriwa kufikia asilimia 81 ya Watanzania wote, hawajafanyiwa tathmini hizi za afya zinazofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu. Tathmini ya hali ya afya imefanyika sana kwa wakulima walioajiriwa kwenye mashamba makubwa ya uwekezaji, na hii ilifanyika ili kukidhi vigezo vya kusafirisha mazao yao ya kilimo nje ya nchi hususani nchi za Ulaya, Asia, na Marekani.

Kwa upande mwingine, ripoti ilionesha kuwa tathmini chache zimefanyika kwa kutumia viuwatilifu vya aina mbalimbali ili kuweza kubaini madhara ya kimazingira yanayotakana na matumizi ya viuwatailifu hivyo. Matokeo ya tathmini hizo yalibainisha uwepo wa kiwango cha juu cha DDT kuliko kiwango kinachokubalika kwenye udongo. Ilibainika pia kwamba hakukuwa na mbinu zozote zilizochukuliwa ili kuweza kutatua tatizo hilo.

***ii. Hakukuwa na uhuishaji wa mara kwa mara wa orodha ya viuwatilifu vilivyosajiliwa***

Ilibainika kuwa orodha ya viuwatilifu haikuwa inahuishwa mara kwa mara kinyume na taratibu zilizopo ambazo zinataka orodha ziwe zinauhishwa angalau mara mbili kwa mwaka. Iliripotiwa kuwa kuna wakati uhuishaji unaweza kuchelewa kwa muda wa mwaka mmoja hadi miwili. Timu ya ukaguzi pia ilibaini kwamba orodha ya viuwatilifu ambayo ilikuwa inatumika kwa kipindi cha ukaguzi huu ilikuwa imetolewa mwezi Juni 2015. **Jedwali 4.1** linaonesha hali ya kuhuishwa kwa orodha ya viuwatilifu vilivyosajiliwa kwa kipindi cha miaka 7 iliyopita.

**Jedwali 4.1: Orodha ya viuwatilifu vilivyosajiliwa kuanzia mwaka 2010/11 hadi 2017/18**

| Mwaka wa Fedha | Hali ya Kuhuisha | Tarehe ya Kuhuisha |
|---|---|---|
| 2011 | Imehuishwa | Novemba 2011 |
| 2012 | Haikuhuishwa | - |
| 2013 | Imehuishwa | Aprili 2013 |
| 2014 | Imehuishwa | Januari 2014 |
| 2015 | Imehuishwa | Juni 2015 |
| 2016 | Haikuhuishwa | - |
| 2017 | Haikuhuishwa | - |

***Chanzo**: Orodha ya Viuwatilifu Vilivyosajiliwa toka mwaka 2010/2011 hadi 2017/2018*

**Jedwali 4.1** linaonesha kwamba hakukuwa na uhuishaji wa mara kwa mara wa orodha ya viuwatilifu. Kadhalika, ilibainika kuwa imechukua takribani miezi 9 hadi miaka 2 kuhuisha orodha ya viuwatilifu vilivyosajiliwa.

### 4.2.2 Usajili hafifu wa mbegu na mbolea

Timu ya ukaguzi iliweza kutembelea wakulima katika halmashauri za Hai, Mbeya Vijijini, Masasi, na Kalambo na kubaini kwamba kumekuwa na malalamiko kuhusu ubora wa mbegu na mbolea ambazo zinasambazwa sokoni. Malalamiko yaliyobainishwa yalihusu uwepo wa mbegu zilizoshindwa kumea na uwepo wa mbegu zinazomea ila zimeshindwa kuzalisha mazao kwa kiwango kilichokusudiwa. Pia, kumekuwa na malalamiko yanayohusu uwepo wa mbolea zenye kiwango cha chini cha ubora.

Kwa mfano, katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha hasa katika Wilaya za Hai, Meru, na Moshi kumekuwa na usambazaji wa mbegu za mahindi kama vile Pioneer 2859, DKC 90-89, SC 627 na SC 403, ambazo hazikuwa na uwezo wa kumea.

Ukaguzi pia uliweza kubaini kwamba malalamiko hayo yalitokana na utekelezaji hafifu wa shughuli za usajili wa mbegu na mbolea. Kwa

mfano, kabla ya mwaka 2017, ilibainika kuwa utaratibu wa kusajili mbegu ulikuwa unachukua muda mrefu. Hii ni kwa sababu mbegu zilikuwa zinafanyiwa majaribio kwenye mashamba tofauti toka kwenye kanda tatu za ekolojia za kilimo nchini. Mahojiano yaliyofanywa na maofisa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu yalibainisha kwamba hali hii imechangia kushindwa kufuata taratibu za usajili wa mbegu.

### 4.2.3 Usajili hafifu wa wauzaji wa pembejeo za kilimo

Kabla ya mwaka 2017, shughuli za usajili wa pembejeo za kilimo na wauzaji wa pembejeo za kilimo zilikuwa zinafanywa na Wizara ya Kilimo kupitia kitengo cha Pembejeo. Kwa sasa, shughuli za usajili zinafanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, kwa upande viuwatilifu; Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, kwa upande wa mbolea; na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu, kwa upande wa mbegu.

Iliripotiwa kuwa kumekuwa na ukiukwaji wa taratibu za usajili kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo. Hali hii inathibitishwa na uwepo wa mbegu, mbolea, na viuwatilifu ambavyo havijasajiliwa nchini. Kulikuwa na zaidi ya asilimia 50 ya wauzaji wa pembejeo za kilimo ambao hawakuwa wamesajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu.

**Usajili hafifu wa wauzaji wa mbolea na mbegu**

Mahojiano yaliyofanyika na maofisa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu yalibainisha kuwa katika kipindi cha msimu wa kupanda, kumekuwa na matukio ya kuibuka kwa wauzaji wa mbegu kwa wakulima. Wengi wa wauzaji hao hawakuwa wanafuata taratibu zinazowataka wawe wamesajiliwa kabla ya kuuza mbegu.

Vile vile ilibainika kuwa wauzaji hao wa mbegu hawakuwa na taaluma muhimu wa usimamizi wa mbegu. Pia, ilionekana kuwa wauzaji hao hawakuwa na elimu ya aina za mbegu, ekolojia ya mbegu, na namna ya kusimamia mbegu kwenye mazingira tofauti. **Jedwali 4.2** linaonesha idadi ya wauzaji wa pembejeo za kilimo ambao wamesajiliwa na wale wasiosajiliwa kwa kipindi cha miaka ya fedha 2015/16 hadi 201718.

**Jedwali 4.2: Wauzaji wa pembejeo za kilimo wasiosajiliwa**

| Mwaka | Jumla ya Idadi ya Wauzaji wa Pembejeo za Kilimo | Idadi ya Wauzaji wa Pembejeo za Kilimo Wasiosajiliwa | Asilimia ya Wauzaji Wasiosajiliwa |
|---|---|---|---|
| 2015/16 | 296 | 200 | 68 |
| 2016/17 | 104 | 20 | 19 |
| 2017/18 | 1321 | 300 | 23 |

**Chanzo:** *Ripoti ya Hali ya Usajili ya TOSCI kwa mwaka 2015 hadi 2018*

**Jedwali 4.2** linaonesha kuwa uwepo wa wauzaji wa pembejeo za kilimo ambao hawakusajiliwa bado ni tatizo nchini. Vilevile, kulikuwa na maboresho kwenye idadi ya wauzaji wa mbegu wasiosajiliwa. Maboresho hayo yaliyotokana na kufutwa kwa ada ya usajili, hivyo kupelekea kuongezeka kwa idadi ya wauzaji wa mbegu waliosajiliwa.

Ilibainika zaidi kuwa mapitio ya ripoti za ukaguzi zilizofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea mwezi MachI 2018 yalibainisha uwepo wa wauzaji wa mbolea ambao hawakusajiliwa na bado walikuwa wanauza na kusambaza mbolea katika halmashauri zao. Hii ni licha ya kuondoa gharama za usajili ili kuweza kushawishi kila muuzaji wa pembejeo za kilimo aweze kufuata taratibu za usajili na uuzaji wa pembejeo za kilimo.

**i. Usajili hafifu wa wauzaji wa viuwatilifu**

Sheria ya Udhibiti wa Mimea Na. 13 ya Mwaka 1997 inawataka wauzaji wa viuwatilifu kusajiliwa kabla hawajaanza kuuza viuwatilifu. Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanyika na maofisa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kulikuwa na mapungufu kwenye usajili wa wauzaji wa viuwatilifu ambayo yalitokana na uwepo wa wauzaji wasiosajiliwa.

Hali hii ilithibitishwa kipindi ambacho timu ya ukaguzi ilitembelea halmashauri 6 na kubaini uwepo wa wauzaji wa viuwatilifu ambao hawakusajiliwa. Kwa mfano, Mkoa wa Njombe ulikuwa na wauzaji 19, kati ya hao wauzaji 13 hawakuwa wamesajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu.

Vilevile, mapitio ya ripoti ya Wauzaji wa Viuwatilifu ya Mwaka 2017 katika Wilaya ya Itilima yalionesha kuwa wauzaji wa viuwatilifu 12 kati ya 17 hawakuwa wamesajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuatilifu.

### 4.2.4 Sababu zinazochangia usajili hafifu wa pembejeo na wauzaji wa pembejeo za kilimo

**i. Sababu zinazohusu usajili hafifu wa viuwatilifu**

***(a) Taratibu hafifu za usajili na kukosekana kwa sera za kuongoza shughuli za usajili wa viuwatilifu***

Ilibainika hakukuwa na sera inayoweza kutumika kuongoza shughuli za usajili wa viuwatilifu nchini. Ripoti ilionesha kuwa taratibu zinazotumika kwa ajili ya usajili zinahitaji maboresho kwa sababu Sheria inayotumika ya Udhibiti wa Mimea ya Mwaka 1997 ni ya zamani na imepitwa kutokana na mabadiliko yalijitokeza kwenye usimamizi wa viuwatilifu kwa kipindi cha miaka 20.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, ili kuweza kusajili viuwatilifu, inatakiwa vifanyiwe majaribio kwa misimu mitatu ya mazao. Kwa sasa, inaonekana ni changamoto kutekeleza takwa hili kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na maendeleo ya sayansi ambayo yamepelekea kubadilishwa kwa viuwatilifu mara kwa mara. Ilibainika kuwa Sheria ya Udhibiti wa Mimea hairuhusu usajili wa kwanza wa viuwatilifu bila kufuata misimu mitatu ya mazao.

***(b) Kushindwa kufanyika kwa mikutano ya Kamati za Usajili wa Viuwatilifu***

Mapitio ya Ripoti za vikao vya Kamati Ndogo za Kitaalamu za Uidhinishaji na Usajili wa Viuwatilifu na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ulinzi wa Mimea yanaonesha kuwa vikao hivyo havikuwa vinafanyika kwa muda uliopangwa ili kuweza kuthibitisha usajili wa viuwatilifu.

Ilibainika kuwa kwa takribani mwaka mzima hakukuwa na kikao kilichofanyika cha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ulinzi wa Mimea. Hii ilisababishwa na ufinyu wa bajeti ambayo haikuwa inatolewa kwa wakati kwa sababu Wizara ya Kilimo ndiyo ilikuwa inasimamia makusanyo kwa kipindi cha miaka ya nyuma. Hali hii ilisababisha ucheleweshaji kwenye usajili wa viuwatilifu ambavyo vilikuwa vinasubiria usajili.

***ii.* Sababu zinazohusu usajili hafifu wa wauzaji wa pembejeo za kilimo**

***(a) Kukosekana kwa uelewa kuhusu matakwa ya usajili***

Iliripotiwa kuwa baadhi ya wauzaji wa pembejeo za kilimo hawakuwa na uelewa wa matakwa na taratibu za usajili wa pembejeo za kilimo. Hivyo, walikuwa wanauza pembejeo bila kuzingatia matakwa husika ya uuzaji. Hali hii ilisababishwa na uenezaji mdogo wa elimu inayohusu usajili toka kwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu.

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanyika na baadhi ya wauzaji wa pembejeo za kilimo ambao hawakusajiliwa katika halmshauri 4 zilizotembelewa za Hai, Mbeya Vijijini, Masasi, na Kalambo, hawakuwa na uelewa wa taratibu na matakwa ya usajili wao na wapi wanatakiwa kuanzia wakati wa kufanya usajli.

***(b) Ukubwa wa gharama za usajili***

Wauzaji wa pembejeo za kilimo hasa wa viuwatilifu kutoka halmashauri[6] zilizotembelewa na timu ya ukaguzi walibainisha kuwa baadhi ya wauzaji wa pembejeo za kilimo ambao hawajasajiliwa walikuwa wanakwepa kusajiliwa kutokana na gharama kubwa. Kwa wastani ilibainika kuwa gharama za usajili za wauzaji wa viutailifu zilikuwa ni shilingi 500,000/=, na pia kila mwaka walitakiwa kulipia kiasi cha shilingi 55,000 ili kurudia usajili.

Iliripotiwa zaidi kuwa kati ya sababu zilizowafanya wakwepe kusajili maduka yao ilikuwa ni uwepo wa ada za usajili. Hii ilibainishwa baada ya kuondoa ada za usajili kwa wauzaji wa mbegu na mbolea ambapo idadi ya usajili wa wauzaji wa mbegu na mbolea iliongezeka toka 296 hadi 1321 kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2017/18. Kwa upande wa wauzaji wa viuwatilifu, hali iliendelea kuwa mbaya kwa sababu bado wanatakiwa kulipia gharama za usajili.

***(c) Kaguzi zilizofanyika kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo hazikuwa toshelevu***

Ilibainika kuwa usajili hafifu wa wauzaji wa pembejeo za kilimo ulichangiwa na utekelezaji hafifu wa ukaguzi. Mapitio ya Ripoti za ukaguzi yalionesha kuwa utekelezaji hafifu wa kaguzi zilizofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu zimesababisha wauzaji wa pembejeo za kilimo waanze kuuza pembejeo bila kuzingatia matakwa ya usajili.

### 4.2.5 Madhara yatokanayo na usajili hafifu wa pembejeo na wauzaji wa pembejeo za kilimo

***Kuwepo sokoni kwa pembejeo za kilimo zisizosajiliwa na zenye ubora wa chini***

Ukaguzi ulibainisha kuwa kumekuwa na changamoto ya uwepo wa pembejeo za kilimo zisizosajiliwa na zenye ubora wa chini ya kiwango. Kwa upande wa viuwatilifu, ilibainika kuwa viuwatilifu visivyosajiliwa vilionekana kwenye wilaya na mikoa yote Tanzania. Hii ilionekana zaidi kwenye mikoa na wilaya ambazo zimepakana na

[6] Halmashauri za Wilaya za Meru, Itilima, Urambo, Morogoro, Njombe, Masasi, Hai, Mbeya and Kalambo

nchi jirani kama vile Mtwara, Mbeya, Kigoma, Tanga, Kagera na Arusha. Kadhalika, viuwatilifu visivyosajiliwa kama vile Dudu- All 450 EC, Ninja Plus – 5EC, Dudu – Acelamectin 5% EC, Sevin Dudu Dust, Abamite, Doom, Boss, Lava, Lethal, and Romectin zilionekana kwenye maduka 7 kati ya 13 yaliyotembelewa kwenye halmashauri hizo.

Kwa upande wa mbegu, ilionekana kuwa kulikuwa na ushukaji wa mavuno kwenye mazao ya kilimo. Hii ilisababishwa na matumizi ya mbegu zilizokuwa chini ya kiwango. **Jedwali 4.3** linatoa maelezo zaidi kuhusu matukio yaliyobainika ya madhara ya kutumia mbegu zilizokuwa chini ya kiwango.

**Jedwali 4.3: Madhara ya kusambaza mbegu zenye ubora wa kiwango cha chini kwa wakulima**

| Wakulima/ Mashamba | Mkoa | Mzalishaji/ Msambazaji | Aina ya Mbegu | Madhara |
|---|---|---|---|---|
| Mella Farm | Morogoro | Sygenta (T) Ltd | Maize seeds SY (514) | Hakukuwa na mavuno kwenye ekari 200 zilizolimwa. |
| Patrick John Farm | Morogoro | Ultravetis (Hygiene Biotech) | Maize seeds WE 2109 | Hakukuwa na mavuno kwenye ekari 12 zilizolimwa. |
| Wakulima 80 wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai DC | Kilimanjaro | SEEDCO | SEEDCO 513 | Ekari 24 ziliathiriwa na mavuno yalishuka kwa tani 94. |

**Chanzo:** Ripoti za Ukaguzi na Madai ya Wakulima, *Julai 2013 – Juni 2018*

Kwa kuzingatia **Jedwali 4.3** ilibainika kuwa wakulima walipoteza mavuno kwenye ekari 236, ambapo baadhi ya wakulima walipata mavuno pungufu au kukosa kabisa kutokana na matumizi ya mbegu za chini ya kiwango.

## 4.3 Ukaguzi Hafifu wa Pembejeo za Kilimo

Ukaguzi ulionesha kuwa kaguzi zinazofanyika ili kuhakikisha ubora wa pembejeo za kilimo kama vile mbolea, mbegu, na viuwatilifu hazikufanyika kikamilifu kwa wauzaji wa pemebejeo za kilimo kwenye maeneo ya mipakani na kwa wakulima. Hii ni kama invyoelezwa zaidi hapa chini.

### 4.3.1 Ukaguzi hafifu wa viuwatilifu

Wakaguzi wa viuwatilifu wanatakiwa kuwakagua wauzaji wa viuwatilifu na katika maeneo ya mipakani kama inavyotakiwa na Sheria ya Udhibiti wa Mimea Na. 13 ya Mwaka 1997. Pia, wanatakiwa kuwa na mipango-kazi, sera, na taratibu za ukaguzi.

Ilibainika kuwa kaguzi zilikuwa zinafanyika katika maeneo ya mipakani na kwa wauzaji wa viuwatilifu. Ilibainika zaidi kuwa kaguzi hizo hazikuwa zinafanyika kikamilifu ili kuweza kuhakikisha kuwa ni viuwatilifu vilivyosajiliwa tu ndivyo vinauzwa na kusambazwa nchini. Hii ni kwa sababu ukaguzi haukuweza kufanyika kwenye mipaka yote, na kwa wauzaji wote wa viuwatilifu kama inavyoelezwa hapa chini.

***i. Ukaguzi hafifu kwa wauzaji wa viuwatilifu***

Kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Mimea Na. 13 ya Mwaka 1997, wauzaji wa viuwatilifu wanatakiwa wakaguliwe baada ya kupatiwa mafunzo ya uendeshaji wa biashara ya viuwatilifu. Hii inafanyika ili kuweza kubaini iwapo wanakidhi vigezo vya awali vya uuzaji wa viuwatilifu. Vilevile, kabla ya kupatiwa vibali vipya kila mwaka, wanatakiwa pia kukaguliwa tena ili kuweza kutambua iwapo bado wanaendelea kutekeleza taratibu za uuzaji wa viuwatilifu.

Ilibainika pia kuwa kaguzi zinazofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu haziwafikii wauzaji wote wa viuwatilifu kama inavyotakiwa na Sheria ya Udhibiti wa Mimea Na. 13 ya Mwaka 1997. Hali hii ilibainika kutokea katika halmashauri sita za Meru, Itilima, Urambo, Morogoro, Njombe, na Masasi ambazo zilitembelewa na timu ya ukaguzi.

Timu ya Ukaguzi ilifanya mapitio ya majalada 20 ya wauzaji wa viuwatilifu kutoka katika mikoa 8 ya Tabora, Arusha, Simiyu, Dar es Salaam, Morogoro, Njombe, Dodoma, na Mtwara. Katika mapitio ya majalada hayo, ilibainka kuwa kulikuwa na wauzaji wa viuwatilifu nchini ambao hawakusajiliwa. Kwa wale ambao walikaguliwa hawakuweza kukaguliwa mara kwa mara ili kuweza kubaini iwapo kuna maboresho kwenye mapungufu yaliyobainishwa, na iwapo wanakidhi vigezo vya uendeshaji wa biashara ya viuwatilifu.

Kwa mfano, ilibainika kuwa wauzaji wa viuwatilifu hawakuweza kukaguliwa mara kwa mara kwa kipindi cha miaka kumi na mitano (15) toka wafanyiwe ukaguzi wa mara ya kwanza. Pia, ilibainika kuwa licha ya kutokukaguliwa, walipatiwa vibali vya uuzaji wa viuwatilifu na walikuwa wanaendelea na biashara hiyo. Kwa mujibu wa mapitio ya majalada hayo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa katika kusajili upya wauzaji wa viuwatilifu, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu haikuweka mkazo kwenye kukidhi vigezo na taratibu, bali waliangalia zaidi malipo ya kuhuisha vibali vya biashara kama kigezo cha kumsajili upya muuzaji wa viuwatilifu.

Ilibainika kuwa baadhi ya wauzaji wa viuwatilifu walikuwa wanafanya biashara hiyo bila kukaguliwa mara kwa mara kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4.4.**

**Jedwali 4.4: Hali ya Ukaguzi wa Wauzaji wa Viuwatilifu kwenye Halmashauri Zilizotembelewa**

| Jina la Duka/Muuzaji wa Viuwatilifu | Mwaka Alioanzisha Biashara | Idadi ya Kaguzi Zilizofanyika | |
|---|---|---|---|
| | | Kaguzi ya Mara ya Kwanza | Marudio ya Ukaguzi |
| Duka la Viuwatilifu 1 | 2010 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 2 | 2015 | 1 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 3 | 2013 | 1 | 1 |
| Duka la Viuwatilifu 4 | 2016 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 5 | 2008 | 1 | 8 |
| Duka la Viuwatilifu 6 | 2015 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 7 | 2016 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 8 | 2008 | 1 | 2 |
| Duka la Viuwatilifu 9 | 1994 | 1 | 7 |
| Duka la Viuwatilifu 10 | 2015 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 11 | 2010 | 1 | 2 |
| Duka la Viuwatilifu 12 | 2005 | 1 | 2 |
| Duka la Viuwatilifu 13 | 1999 | 1 | 2 |

***Chanzo:** Uchambuzi toka kwenye Taarifa za Mahojiano, Januari 2018*

**Jedwali 4.4** linaonesha kuwa wauzaji wa viuwatilifu 5 kati ya 13 hawakukaguliwa kabisa; 8 kati ya hao walikaguliwa mara moja kabla ya kuanzisha biashara zao; na wauzaji 2 tu ndiyo walikaguliwa mara kwa mara.

Kadhalika, timu ya ukaguzi ilitembelea wauzaji wa viuwatilifu 13 katika halmashauri na kubaini kuwa baadhi ya wauzaji wa viuwatilifu ambao wapo katika vijiji vya mbali walikuwa wanafanya biashara hii bila kuzingatia taratibu za biashara ya viuwatilifu kwa kuwa hakuwahi kukaguliwa hata mara moja. Kwa mfano, timu ya ukaguzi ilitembelea wauzaji wa viuwatilifu 2 katika Wilaya ya Itilima na muuzaji 1 katika Wilaya ya Njombe Mji na kubaini kuwa hawakuwahi kukaguliwa tangu waanze kufanya biashara hiyo ya viuwatilifu, kwa sababu ya umbali wa vijiji vyao na eneo ambalo Ofisi za Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu ipo. Ilibainika zaidi kuwa maduka hayo yalikuwa yamefunguliwa kati ya mwaka 2010 na 2015.

***ii. Ukaguzi hafifu kwenye maeneo ya mipakani***

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanyika na wakaguzi wa viuwatilifu wa Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, kaguzi zinazofanyika kwenye maeneo ya mipaka hazitoshelezi.

Hali hii pia ilidhihirika wakati wa kufanya mapitio ya ripoti za ukaguzi katika maeneo ya mipaka ambazo ziliandaliwa na Wizara ya Kilimo. Ripoti hizi zilionesha kuwa kati ya mipaka 58, mipaka 17 haikuwa inafanya ukaguzi. Hii ilimaanisha kuwa pembejeo za kilimo ambazo

zilikuwa zinaingia nchini kupitia mipaka hiyo hazikuwa zinakaguliwa. Hali hii ilipelekea hatari ya kuingizwa nchini pembejeo za kilimo zisizo na ubora.

### 4.3.2 Taratibu hafifu za ukaguzi wa mbegu

Maofisa kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu walibainisha kuwa Ofisi yao haikuweza kudhibiti ubora wa mbegu zilikuwa zilizokuwa zinaingizwa nchini kwa kuhakikisha kuwa uingizaji wa mbegu unazingatia taratibu. Waliripoti kuwa kulikuwa na utekelezaji hafifu wa shughuli za ukaguzi kwa wauzaji mbegu na katika maeneo ya mipaka. Hii ilidhihirishwa na uwepo wa mbegu ambazo hazikuwa na ubora sokoni.

#### *i. Kaguzi Zilizofanyika kwa wauzaji wa mbegu zilikuwa hafifu*

Mapitio ya Mipango-kazi ya Mwaka na Ripoti za Utekelezaji za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18 yalibainisha kuwa wauzaji wa mbegu waliopangwa kutembelewa kwa mwaka walikuwa chini ya nusu. Vilevile, ilibainika kuwa kaguzi zilizofanyika zilikuwa chache ikilinganishwa na zile zilizopangwa. Jedwali 4.5 linaonesha kuwa idadi ya wauzaji wa mbegu waliokaguliwa kuanzia mwaka 2014 hadi 2018.

**Jedwali 4.5: Idadi ya wauzaji wa mbegu ambao wamepangwa kukaguliwa kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Wauzaji wa Mbegu Waliosajiliwa | Wauzaji wa Mbegu Waliokaguliwa | Asilimia ya Wauzaji Waliokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 2014/15 | 525 | 105 | 20 |
| 2015/16 | 765 | 0 | 0 |
| 2016/17 | 827 | 296 | 36 |
| 2017/18 | 987 | 296 | 30 |

**Chanzo**: *Mipango Kazi ya Mwaka kuanzia 2013/14 hadi 2017/18*

**Jedwali 4.5** linaonesha kuwa idadi kubwa ya wauzaji wa mbegu hawakuweza kufikiwa kipindi cha ukaguzi kwa sababu ni asilimia 30 tu ndiyo waliweza kukaguliwa. Ilibainika zaidi kuwa uwezekano wa kuwafikia wauzaji wote wa mbegu ulishuka kwa asilimia 6 kwa mwaka wa fedha 2017/18

#### ii. *Hakukuwa na ukaguzi uliofanyika mipakani*

Kwa mujibu wa Kanuni za Mbegu za Mwaka 2007, mbegu zinazoingizwa nchini zinatakiwa zikaguliwe na kufanyiwa vipimo kabla ya kusambazwa. Kabla ya usambazaji, mbegu zinatakiwa zifanyiwe vipimo na majibu yatoke ili kuweza kubaini uwezo wake wa kumea.

Wataalamu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu walibainisha kuwa kulikuwa na mbegu ambazo hazikuwa zimethibitishwa. Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu walibainisha kuwa mbegu hizi ziliingizwa nchini kupitia mipaka ya Namanga na Tunduma na kampuni za SEEDCO na PANA Com. Hii ilisababishwa na kukosekana kwa wakaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kwenye mipaka husika.

### *iii. Kaguzi Zilizofanyika kwa Wazalishaji wa Mbegu Zilikuwa Hafifu*

***Uchelewaji wa kutuma maombi ya kukaguliwa kwa mashamba***

Kwa mujibu wa Kanuni za Mbegu kifungu Na. 27(1) za Mwaka 2007, wazalishaji wa mbegu wanatakiwa kutuma maombi ya kufanyiwa ukaguzi ambayo yanatakiwa yaoneshe kila aina ya zao lililolimwa kwa ajili ya kuthibitisha. Maombi yanatakiwa yatumwe ndani ya siku 30 baada ya kupanda ili kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kufanya ukaguzi na kutathmini ubora wa uzalishaji wa mbegu.

Mapitio ya fomu za maombi ya kufanyiwa ukaguzi toka kwa makampuni tofauti ya uzalishaji ambayo timu ya ukaguzi iliyachagua yalibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kutuma maombi ya kufanyiwa ukaguzi. Kati ya wazalishaji wa mbegu 19, kulikuwa na ucheleweshaji wa maombi ya kufanyiwa ukaguzi yapatayo 11, ambayo ni sawa na asilimia 58. Vilevile, ilibainika kuwa hakukuwa na muda kamili ambao wakaguzi wanatakiwa kwenda kufanya ukaguzi baada ya kupokea maombi ya kufanyiwa ukaguzi toka kwa wazalishaji wa mbegu. Hali hii ilibainika kuchangiwa na kushindwa kufanya kaguzi kwa ngazi mbalimbali kama taratibu inavyotaka, hivyo kuathiri ubora wa mbegu zinazozalishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu

***Kaguzi chache zilifanyika kwenye mashamba ya kuzalishia mbegu kwa mujibu wa matakwa ya mbegu husika***

Mapitio ya Ripoti za Taratibu za Ukaguzi za mashamba ya uzalishaji wa mbegu inaonesha kuwa kaguzi mbalimbali zinapaswa kufanya kwenye mbegu zinazozalishwa nchini kulingana na aina ya mbegu. Ilibainika kuwa mbegu hazikuwa zinakaguliwa katika kipindi husika ambacho ilipaswa kukaguliwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4.6.**

**Jedwali 4.6 Kaguzi zinazohitajika kufanywa kwenye mashamba ya kuzalishia mbegu**

| Aina ya Mbegu | Idadi ya Kaguzi | Hatua za Ukaguzi |
|---|---|---|
| Mahindi | 3 | 1. Kabla ya kutoa maua<br>2. Kipindi cha kutoa maua<br>3. Baada ya kuvuna |
| Mpunga | 2 | 1. Kabla ya utoa maua<br>2. Hatua ya ulaji |
| Maharage | 2 | 1. Kipindi cha kutoa maua<br>2. Hatua ya ulaji |

***Chanzo:*** *Taratibu za Ukaguzi na Uchambuzi uliofanywa na wakaguzi, 2018*

Ukaguzi ulibainisha kuwa, hakukuwa na ukaguzi ambao uliofanyika kwenye mbegu za mahindi, maharage, na mpunga kwa mujibu wa hatua husika za uzalishaji. Pia, ilibainika kuwa licha ya kuwa mbegu hizo hazikukaguliwa kwa mujibu wa taratibu husika, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu walizithibitisha ili zitumiwe na wakulima. Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya mashamba 19 yaliyochaguliwa, mashamba 16 hayakuweza kukaguliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kwa mujibu wa Kanuni husika.

### 4.3.3 Taratibu Hafifu za Ukaguzi wa Mbolea


Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea inatakiwa kufanya ukaguzi kila robo mwaka kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo na mipakani ili kuweza kuhakikisha ubora wa mbolea zinazosambazwa.

Ilibainika kuwa kaguzi zilizokuwa zinafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea katika maeneo ya mipaka na kwa wauzaji wa viuwatilifu zilikuwa hafifu. Hii ni kutokana na uwepo wa mbolea ambayo haikuwa na ubora unaohitajika. Hali hii ni kama inavyooneshwa hapa chini.

#### i. Kaguzi hafifu zilifanyika kwa wauzaji wa mbolea

Mapitio ya Mipango-kazi ya mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18 yanaonesha kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea haikuweza kupanga kufanya ukaguzi kwa wauzaji wote wa mbolea kwenye mikoa yote ya Tanzania bara. **Kielelezo 4.1** kinaonesha mikoa ambayo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea ilitakiwa kukagua na mikoa mabayo ilipanga kukagua kwa kipindi ambacho ukaguzi huu umeangalia.

**Kielelezo 4.1: Jumla ya mikoa iliyopaswa kukaguliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea na mikoa iliyopangwa kufanyiwa Ukaguzi kuanzia mwaka 20113/14 hadi 2017/18**




***Chanzo:*** *Ripoti za Kimkakati kuanzia mwezi Julai 2013 hadi Juni 2018*

**Kielelezo 4.1** kinaonesha kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea haikuweza kuweka mipango-kazi ya ukaguzi kwa nusu ya mikoa waliyopaswa kukagua. Hata hivyo, kulikuwa na ongezeko la mikoa iliyopangwa kukaguliwa kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2015/16.

Mapitio ya ripoti za mwaka za utekelezaji za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea yalibainisha kuwa mikoa ambayo ilipangwa kukaguliwa haikuweza kukaguliwa yote. Licha ya kupanga kufanya ukaguzi kwa mikoa michache, bado ukaguzi haukuweza kufanyika katika mikoa hiyo yote kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4.7:**

**Jedwali 4.7: Asilimia ya mikoa iliyokaguliwa kulingana na mipango-kazi**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mikoa Iliyopangwa Kukaguliwa | Idadi Kamili ya Mikoa Iliyokaguliwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2013/14 | 9 | 6 | 67 |
| 2014/15 | 9 | 7 | 78 |
| 2015/16 | 10 | 7 | 70 |
| 2016/17 | 10 | 8 | 80 |
| 2017/18 | 10 | 8 | 80 |

*Chanzo: Mpango-mkakati na Ripoti za Utekelezaji toka mwezi Julai 2013 hadi Juni 2018*

**Jedwali 4.7** linaonesha kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea iliweza kufanya ukaguzi kwenye mikoa michache iliyopangwa kukaguliwa. Hata hivyo, ni asilimia 80 ya mikoa iliyopangwa kukaguliwa ndiyo ilikaguliwa. Kadhalika, mwenendo wa ufanisi unaonesha kuwa idadi

ya mikoa iliyokaguliwa inaongezeka, licha ya kuwa imekuwa nje ya lengo lililokusudiwa kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita.

**ii. Utekelezaji hafifu wa ukaguzi katika maeneo ya mipakani**

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea ilibainisha kuwa kumekuwa na upungufu wa wakaguzi wa kuwezesha kufanyika kwa ukaguzi nchini. Mamlaka haina wakaguzi kwenye mipaka ambao walitakiwa kusimamia udhibiti wa ubora wa mbolea inayoingizwa nchini. Ilibainika kuwa kwa sasa kumekuwa na matumizi makubwa ya mbolea aina ya "foliar" inayoingizwa nchini kupitia mipaka yetu. Hii ilithibitishwa na uwepo wa aina hii ya mbolea kwenye maduka mbalimbali nchini.

Sheria inataka maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kuwepo kwenye maeneo ya mipakani ili kuweza kufanya tathmini iwapo mbolea inayoingizwa au kusafirishwa nchini ni yenye ubora unaohitajika. Ilibainika kuwa takribani asilimia 90 ya mbolea inayotumika nchini inaingizwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Kadhalika, kulibainika kuwepo kwa changamoto za kiutendaji katika Bandari ya Dar es Salaam. Changamoto hizo ni kukosekana kwa maabara ya kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Mboleakuweza kupima mbolea. Mamlaka inatumia maabara za Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuawatilifu, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Kituo cha Utafiti Mlingano, na Shirika la Viwango Tanzania kama mbadala. Hali hii ilipelekea Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kuchukua muda mrefu kukamilisha vipimo vya mbolea, na matumiz ya maabara hizi yaliongeza gharama za upimaji.

Ilibainika pia kuwa kulikuwa na wakaguzi wachache katika Bandari ya Dar es Salaam. Hii ni kwa sababu kuna wakati wakaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea huwa wanapangiwa majukumu mengine. Hali hii iliathiri utaratibu wa kufanya ukaguzi. Kwa ujumla, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea ina jumla ya wakaguzi 108, ambapo wakaguzi 8 walikuwa wamepangwa Makao Makuu na wakaguzi 100 walipangwa katika mamlaka za serikali za mitaa.

### 4.3.4 Sababu zinazochangia ufanyaji hafifu wa ukaguzi kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo na mipakani

Ilibainika kuwa kumekuwa na utekelezaji hafifu wa shuguli za ukaguzi kwa wauzaji wa pembejeo na mipakani. Hali hii ilisababishwa na:

***(a) Uchache wa wakaguzi***

Iliripotiwa kuwa kumekuwa na upungufu wa wakaguzi wenye kukidhi viwango, ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi kwa wauzaji wa viuwatilifu na mipaka.

Ilibainika kuwa wakaguzi wengi ambao wanafanya kazi kwenye kanda za Wizara ya Kilimo na mipakani hawakuwa wamepatiwa mafunzo kwenye eneo la viuwatilifu. Ilionekana zaidi kuwa baadhi ya wakaguzi hawakuwa wanakidhi vigezo vya kufanya ukaguzi. Hii ni kwa sababu wakaguzi hawakuthibitishwa na Wizara ya Kilimo.

Upungufu wa wakaguzi kwa upande wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu ulikuwa wa asilimia 55 na katika Wizara ya Kilimo ulikuwa ni asilimia 28 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4.8.**

**Jedwali 4.8: Mgawanyo wa wakaguzi wa viuwatilifu kulingana na mahitaji**

| Kituo cha Kazi | Idadi ya Wakaguzi Wanaohitajika | Idadi ya Wakaguzi Waliopangwa | Upungufu wa Wakaguzi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu | 20 | 9 | 11 | 55 |
| Wizara ya Kilimo | 230 | 165 | 65 | 28 |

***Chanzo:*** *IKAMA ya Wizara ya Kilimo na* Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, *2018*

Ilibainika zaidi kuwa kwa ujumla kulikuwa na wakaguzi 99 nchini (90 walikuwa Wizara ya Kilimo na 9 Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu) ambao walitakiwa kukagua wauzaji wa viuwatilifu 1935.

Kadhalika, hata kama wakaguzi wote wangetumika kufanya ukaguzi, uwiano wa mkaguzi kwa idadi ya wauzaji wa viuailifu ulikuwa 1:20. Hii ilipelekea kuwa na upungufu wa wakaguzi 76. Vilevile, kama upungufu huu wa wakuguzi 76 ungeshughulikiwa kulingana na mahitaji, uwiano ungekuwa 1:11 jambo ambalo lingehakikisha ubora wa kaguzi zinazofanyika.

***(b) Kukosekana kwa vifaa vya ukaguzi mipakani***

Ilibainika kuwa kaguzi zinazofanyika mipakani zilikuwa hafifu kutokana na kukosekana kwa vifaa bora vya ukaguzi ili kufanikisha ukaguzi. Hali hii ilithibitishwa kwenye Mpaka wa Namanga, ambako wakaguzi walieleza kukosa vifaa kama vile glovu, vifunikasura, buti, na skana. Hali hii ilielezwa kukwamisha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa viuwatilifu zinazofanywa na wakaguzi waliopo mipakani

katika kubainisha iwapo viuwatilifu vinavyoingizwa nchini vinakidhi vigezo.

Timu ya ukaguzi ilikagua ili kubaini uwepo wa vifaa vya ukaguzi kulingana na mahitaji katika Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu na matokeo yake ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4.9**:

**Jedwali 4.9: Hali ya uwepo wa vifaa vya ukaguzi**

| Jina la Taasisi | Jina la Kifaa | Idadi Inayohitajika | Idadi ya Vifaa Vilivyopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| Wizara ya Kilimo | Buti ngumu za kukinda miguu | 50 | Hakuna | 50 |
| | Makoti marefu/Mashati ya Mikono Mirefu | 50 | Hakuna | 50 |
| | Kofia | 50 | Hakuna | 50 |
| | Miwani ya Usalama/ Vikingasura | 50 | Hakuna | 50 |
| | Vifaa vya Kukinga Mfumo wa Upumuaji | 50 | Hakuna | 50 |
| | Glovu | Maboksi 30 | Hakuna | Maboksi 30 |
| Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu | Magari | 3 | 1 | 2 |
| | GPS | 3 | 0 | 3 |

***Chanzo:*** *Ripoti za Ukaguzi na Mchanganuo Uliofanywa na wakaguzi*

**Jedwali 4.9** linaonesha kuwa Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu inakosa vifaa muhimu kama vile vifaa vya kujikinga, magari, na GPS ambavyo ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa viuwatilifu mipakani. Hii inamaanisha kuwa viuwatilifu vinavyoingizwa nchini kupitia mipaka mbalimbali ya nchi havikuwa vinakaguliwa ipasavyo na Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu.

### *(c) Adhabu dhaifu hutolewa kwa waagizaji na wauzaji wa viuwatilifu*

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 34 cha Sheria ya Udhibiti wa Mimea ya Mwaka 1997, wakaguzi wamepewa mamlaka ya tutoa adhabu kwa waagizaji na wauzaji wa viuwatilifu pale wanapobaini wamefanya makosa. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa wakaguzi hawakutekeleza kikamilifu utoaji wa adhabu kwa waagizaji na wauzaji wa viuwatilifu. Hii ni kwa sababu wakaguzi hawakutoa adhabu mbalimbali kwa mujibu wa Sheria husika. Ilibainika kuwa hatua

iliyochukuliwa kwa waagizaji na wauzaji wa viuwatilifu walikutwa na makosa ni kupewa barua za onyo tu. Ni mara chache adhabu kama vile faini na kufunguliwa mashitaka au kufungiwa maduka ya viuwatilifu zilikuwa zimetolewa.

Kwa mfano, katika mapitio ya ripoti za ukaguzi zilizofanyika kwa kipindi cha mwezi Julai na Disemba mwaka 2017, ni tukio moja tu la usambazaji wa viuwatilifu visivyokidhi vigezo lililomhusu mfanyabiashara mmoja wa Kichina mkoani Mtwara ndilo lilifikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka. Hukumu ya shauri ilimtaka mfanyabiashara huyo kusafirisha bidhaa hizo zilizokamatwa kwa gharama zake na pia alitozwa faini ya shilingi 44,800,000/=.

Kadhalika, ilibainika kuwa licha ya kutoa barua za onyo pekee, hakukuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuweza kuona ni kwa kiwango gani adhabu zilizotolewa zimetelekezwa. Hii ni kwa sababu kaguzi hazikuwa zinafanyika mara kwa mara kwa waagizaji na wauzaji wa pembejeo ambao walibainika kuwa na makosa.

### *(d) Kukosekana kwa taratibu na mipango ya ukaguzi*

Iliripotiwa kuwa hakukuwa na sera iliyokuwa inaelezea ni kwa namna gani na lini ukaguzi ufanyike, na taratibu zipi zichukuliwe dhidi ya wanaobainika kutenda makosa. Wakaguzi walikuwa wanatumia fomu za ukaguzi kama mwongozo wa kutekeleza majukumu yao ya kikaguzi. Fomu hii ilikuwa inaonesha orodha ya maeneo yanayotakiwa kukaguliwa.

Mapitio ya fomu za ukaguzi wa marejeo yalibainisha kuwa kulikuwa na masuala muhimu yaliyohitaji kuangaliwa mara kwa mara, ila hayakuoneshwa kwenye fomu ya ukaguzi wa marejeo. Kwa mfano, kwenye fomu hizo za ukaguzi wa marejeo, hazikuwa na maelezo ya ukaguzi kwenye mambo kama vile vifaa vya kujikinga na viuwatilifu, kifaa cha kuzimia moto, namna ya kutupa na kuteketeza viuwatilifu, tathmini ya jengo na orodha ya viuwatilifu vilivyokutwa kwenye jengo. Ilibainika kuwa mambo haya yanayokosekana kwenye fomu za ukaguzi yanaweza kukaguliwa na mkaguzi mwenye uzoefu ila inaweza kuwa ngumu kwa mkaguzi asiye na uzoefu kuweza kutambua kwamba anahitajika kukagua mambo hayo yote.

Kadhalika iliripotiwa na maofisa wa Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kuwa hakukuwa na mpango-mkakati wa ukaguzi wala orodha ya maeneo yenye vihatarishi vya viuwatilifu ili kuwezesha upangaji wa kaguzi kwa wauzaji wa viuwatilifu na maeneo ya mipaka.

### i. Sababu zilizopelekea utekelezaji hafifu wa kaguzi za mbegu na mbolea

#### *(a) Kukosekana kwa wakaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kwenye maeneo ya mipakani*

Sababu moja kuu iliyotajwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu ilikuwa ni kukosekana kwa wakaguzi wao kwenye maeneo ya mipakani. Kukosekana kwa wakaguzi wa Mamlaka kwenye mipaka kunapelekea hatari ya uingizaji wa mbegu ambazo hazijasajiliwa nchini. Maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu na Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea wanapaswa kuwa kwenye maeneo ya mipakani ili waweze kukagua pembejeo za kilimo zinazoingizwa au kusafirishwa ili kuhakikisha mbegu hizo hazina maambukizi yeyote na pia ni bora kwenye kuleta mavuno yanayokusudiwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa ni wakaguzi wa Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea tu ndiyo walikuwepo kwenye mipaka yote kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4.10**

**Jedwali 4.10: Utendajikazi wa kila Taasisi kwenye Maeneo ya Mipakani**

| Taasisi | Idadi ya Mipaka Inayotakiwa Kufanya Kazi | Mipaka Inayofanya Kazi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Wakaguzi wa Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea | 57 | 47 | 18 |
| Wakaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu | 57 | 0 | 100 |

***Chanzo:*** *Uchambuzi Uliofanywa na Wakaguzi, 2018*

Kwa mujibu wa **Jedwali 4.10,** hakuna mkaguzi yeyote wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu aliyepangwa kwenye maeneo ya mipakani, isipokuwa wakaguzi wa Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea walikuwepo katika takribani asilimia 82 ya mipaka yote nchini.

#### *(b) Uchache wa wakaguzi kwenye halmashauri na Ofisi za* **Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu**

Sababu nyingine iliyotajwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu iliyopelekea utekelezaji hafifu wa kaguzi ilikuwa ni uchache wa wakaguzi, ambapo idadi ya wakaguzi ilibainika kuwa ndogo ikilinganishwa na mahitaji. Mapitio ya IKAMA yalibainisha kuwa Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu na Ofisi za kanda zilikuwa na idadi ya wakaguzi wapatao 52 kati ya 112 wanaohitajika; na halmashauri kulikuwa na wakaguzi 80 kati ya 182 wanaohitajika.

### *(c) Kuwepo kwa miongozo isiyoeleweka na kukosekana kwa mipango-kakati ya utekelezaji wa shughuli za ukaguzi*

Kwa mujibu wa Kanuni za Kilimo za Mwaka 2007, wakaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu wanatakiwa kutoa ruhusa ya kusafirisha mbegu pamoja na kibali cha kuingiza na kusafirisha mbegu. Kadhalika, ilibainka kuwa hakukuwa na taratibu rasmi za utendaji zilizoandaliwa kwa ajili ya kuongoza shughuli za ukaguzi mipakani.

Kutokana na mapitio ya mipango-mkakati, ilibainika kuwa hakukuwa na mipango-mkakati iliyondaliwa kwa ajili ya shughuli za ukaguzi kwenye maeneo ya mipakani. Wakaguzi walibainisha kuwa Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu na Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea hawakuweza kuandaa mipango yoyote ya shughuli za ukaguzi. Ni maofisa wa Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea pekee ambao wapo chini ya Wizaya ya Kilimo ndiyo waliweza kufanya ukaguzi wa kutathmini magonjwa ya mbegu zinazoingizwa na kusafirishwa nchini.

### *(d) Kukosekana kwa vifaa vya ukaguzi*

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanywa na maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu Makao Makuu na Ofisi zake za Kanda, kulikuwa na upungufu wa vifaa vya kuwezesha kutekeleza shughuli za ukaguzi. Kwa sasa, ni Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu Makao Makuu pekee ndiyo iliyoweza kupatiwa vifaa vyote vinavyohitajika ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi. **Jedwali 4.11** linaonesha upungufu wa vifaa vya ukaguzi vinavyohitajika.

**Jedwai 4.11: Upungufu wa vifaa vinavyohitajika kwenye Ofisi ya Kanda ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu, Arusha**

| Jina la Kifaa | Idadi ya Vifaa Vinavyohitajika | Vifaa Vilivyopo | Asilimia ya Upungufu |
|---|---|---|---|
| Plastiki za Kupandia Mbegu | 120 Pcs | 40 | 67 |
| Kifaa cha Kuchuja Uchafu | 4 | 2 | 50 |
| Kifaa cha Kutambua Idadi ya Mbegu | 2 | 1 | 50 |
| Kabati la Kuzuia Moto wa Sumu | 2 | 1 | 50 |
| Makasha ya Kuchukulia Sampuli | 6 | 3 | 50 |
| Kasha la Kioo la Kuloekea Mbegu | 40 | 20 | 50 |
| Kifaa cha Kugawia Mbegu | 4 | 3 | 25 |
| Kifaa cha Kuoteshea Mbegu | 1 | 1 | 0 |


**Chanzo:** *Ripoti ya Hali ya Upungufu wa Vifaa na Uchambuzi wa Wakaguzi (2019)*

**Jedwali 4.11** linabainisha kuwa mwaka 2019 kulikuwa na upungufu wa asilimia 50 wa idadi ya vifaa vya maabara vinavyohitajika kwenye Ofisi za Kanda za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kila Ofisi ya Kanda ilikuwa ina gari moja ambalo lilitakiwa kuhudumia mikoa 4 hadi 5. Ilibainika kuwa idadi hii ya magari haikuwa inajitosheleza kutokana na ukubwa wa maeneo ya kufanyia kazi katika mkoa husika kwa sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu ilikuwa na magari 6 tu kati ya 13 yanayohitajika.

***(e) Uchache wa raslimali za kuwezesha kutekeleza ukaguzi***

Ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu kwenye fedha zinazotolewa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi na hivyo kusababisha utekelezaji mdogo wa shughuli za ukaguzi kama inavyoelekezwa zaidi kwenye **Kielelezo 4.2.**

**Kielelezo 4.2: Kiwango cha pesa kilichotengwa na kilichotolewa kwa Ofisi za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2018/18 (Viwango vya fedha ni vya milioni)**




**Chanzo**: Mpango wa Muda Mrefu wa Matumizi, 2013/14 hadi 2017/18

**Kielelezo 4.2** kinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko la kiasi cha fedha kilichopangwa na kile kilichotolewa kwa upande wa Ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu. Hata hivyo, ilibainika kuwa kiasi kilichopangwa hakikuwa kinatolewa chote kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi.

**ii. Sababu za Utekelezaji Hafifu wa Shughuli za Ukaguzi wa Mbolea**

***(a) Kukosekana kwa wakaguzi mipakani***

Ilibainika kuwa kuna jumla ya mipaka 57 nchini ambayo inatakiwa iwe na wakaguzi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu au Wizara ya Kilimo. Hata hivyo, ilibainika kuwa mipaka 47 kati 57 ilikuwa na

wakaguzi toka Wakala wa Afya ya Mimea tu ambao hawakuwa na ujuzi wa kufanya ukaguzi wa mbolea. Kadhalika, ilibainika kuwa Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea inafanya kazi katika Bandari ya Dar es Salaam tu kati ya mipaka 57 nchini.

**(b)** ***Uhaba wa fedha***

Kwa mujibu wa mahojiano ambayo timu ya ukaguzi iliyafanya na maofisa wa Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea, uhaba wa fedha ulikuwa ni miongoni mwa sababu za kushindwa kutekeleza shughuli za ukaguzi. Kulikuwa na utoaji mdogo wa fedha ili kuwezesha kutekeleza shughuli za ukaguzi nchini. Hii ilisababisha Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea ichague mikoa michache tu ya kufanyia ukaguzi. **Jedwali 4.12** linaonesha ugawaji wa fedha kuanzia mwezi Julai 2013 hadi Juni 2018.

**Jedwali 4.12: Mgao wa fedha kwa wakaguzi wa Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea kuanzia mwezi Julai 2013 hadi Juni 2018**

| Mwaka wa Fedha | Kiwango Kilichotengwa kwa Ukaguzi (Milioni/Sh.) | Kiwango Kilichotolewa (Milioni/Sh.) | Asilimia Iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 2013/14 | 82.5 | 42.5 | 52 |
| 2014/15 | 58.3 | 24.2 | 42 |
| 2015/16 | 62.8 | 29.8 | 47 |
| 2016/17 | 76.8 | 50.8 | 66 |
| 2017/18 | 148.7 | 147.2 | 99 |

***Chanzo***: *Mpango wa Muda Mrefu wa Matumizi ya* Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea *kuanzia mwezi Julai 2013 hadi Juni 2018 na Mchanganuo uliofanywa na Wakaguzi 2018*

**Jedwali 4.12** linaonesha kuwa Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea ilipatiwa asilimia 61 ya fedha ilizoomba, ambazo nazo haikuweza kuzitumia kikamilifu. Hii ni kwa sababu haikuweza kukagua mikoa yote iliyopanga kukagua kama ambavyo inaoneshwa kwenye **Jedwali 4.3.** Sababu iliyotolewa ya kutoweza kukagua mikoa yote haikujisheleza kwa kuzingatia tathmini hii iliyofanywa na wakaguzi.

Kwa mwaka wa fedha 2017/18, Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea iliweza kupokea asilimia 99 ya fedha ilizoomba, lakini ilifanya kaguzi 28 tu. Licha ya kuongezeka kwa utoaji wa fedha kwa shughuli za ukaguzi, kiwango cha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi zinazofanywa na Mamlaka wa Udhibiti wa Mbolea kilikuwa kidogo.

### 4.3.5 Athari za ukaguzi hafifu wa pembejeo za kilimo zilizofanywa kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo na mipakani

***i. Usambazaji wa pembejeo za kilimo zenye ubora mdogo***

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na malalamiko kuhusu ubora wa mbegu zilizosambazwa sokoni. Malalamiko yalihusu uwepo wa mbegu zisizomea kwenye soko. Hali hii ilibainika zaidi kwenye mikoa ya kanda ya kaskazini ya Kilimanjaro na Arusha, hususani wilaya za Hai, Meru, na Moshi. Ukaguzi ulibaini kulikuwa na na usambazaji wa mbegu zenye majina ya Pioneer 2859, DKC 90-89, SC 627, na SC 403, ambazo zililalamikiwa kuwa hazikuwa na uwezo wa kumea kama ambavyo ilithibitishwa na Mamlaka wa Udhibiti wa Mbegu. Wakulima pia walilalamika kuhusu uwepo wa mbegu ambazo zilikuwa zinamea ila hazikuweza kutoa mazao kama ilivyokusudiwa. Kadhalika, ilibainika kuwa viuwatilifu zisivyosajiliwa vilionekana kwenye wilaya na mikoa yote ya Tanzania, hali ikiwa mbaya sana katika mikoa ya inayopakana na nchi za jirani.

Timu ya ukaguzi ilifanya mapitio ya ripoti 12 za ukaguzi kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Disemba 2017, zilizoandaliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kwa lengo la kubaini utekelezaji wa shughuli mbalimbali kama vile kuingiza na kuuza viuwatilifu nchini. Mapitio hayo ya ripoti yalibainisha kuwa viuwatilifu kama vile Abamite, Doom, Boss, Lava, Lethal, na Romectin vilikuwa vinauzwa bila kusajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu.

***ii. Kuuza pembejeo za kilimo zilizofungashwa upya***

Iliripotiwa kuwa utekelezaji mdogo wa shughuli za ukaguzi imepelekea kuwepo na tabia kufungua kisha kufungasha upya pembejeo za kilimo kutoka kwenye ujazo mkubwa na kuweka kwenye ujazo mdogo. Hii ilidhihirika kwenye duka moja la muuzaji wa pembejeo za kilimo wakati timu ya ukaguzi ilipotembelea wauzaji wa viuwatilifu katika Wilaya ya Morogoro Vijijini.
Kadhalika, mahojiano yaliyofanywa na timu ya ukaguzi na wakulima kwenye wilaya 4 zilizotembelewa za Hai, Mbeya Vijijini, Masasi, na Kalembo wakulima waliripoti kuwa kumekuwa na tabia ya kurudia kufungasha magunia ya mbolea toka ujazo mkubwa na kuweka kwenye ujazo mdogo. Hali hii iliripotiwa kusababishwa na kukosekana kwa mbolea iliyofungwa kwenye ujazo mdogo ambao unalingana na mahitaji ya wakulima wengi. Ilibainika kuwa kwa sasa ufungaji wa mbolea ni kwenye magunia ya kilogramu 50 ambao wakulima wenye uwezo mdogo hawawezi kumudu.

***iii. Uingizaji usio halali wa pembejeo za kilimo***

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na viuwatilifu nchini ambavyo viliingizwa kwa njia zisizo halali. Hali hii ilisababishwa na kutofanyika kwa ukaguzi wa mara kwa mara mipakani. Hali hii ilibainika sana kwenye mikoa inayopakana na nchi zingine kama vile Mtwara, Mbeya, Kigoma, Tanga, Kagera, na Arusha.

## 4.4 Uenezaji Hafifu wa Maarifa kwa Wauzaji wa Viuwatilifu, Wakulima, na Maofisa Ugani

### 4.4.1 Uenezaji hafifu wa maarifa kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo

***(a) Uenezaji hafifu wa maarifa kwa wauzaji wa viuwatilifu***

Kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Mimea ya Mwaka 1997 na Kanuni zake za Mwaka 1998, wauzaji wa viuwatilifu wanatakiwa wapatiwe mafunzo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kabla ya kuanza kuuza viuwatilifu. Ilibainika kuwa mafunzo kwa wauzaji wa viuwatilifu ni muhimu ili kuwa na uelewa mzuri wa kuhifadhi viuwatilifu kwenye maduka yao, na kuweza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizu sahihi ya viuwatilifu.

Mapitio ya Ripoti za Mafunzo kwa kipindi cha ukaguzi huu yalibainisha kuwa kuanzia mwezi Septemba 2015 hadi Septemba 2017, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu ilitoa mafunzo kwa wauzaji wa viuwatilifu 998. Mafunzo hayo yalihusu taratibu za uendeshaji wa biashara ya viuwatilifu nchini kulingana na Sheria ya Udhibiti wa Mimea ya Mwaka 1997.

Kadhalika, ilibainika kuwa hakukuwa na kanzidata inayoonesha idadi ya wauzaji wa viuwatilifu waliopo nchini ikilinganishwa na wale waliopatiwa mafunzo, ambayo ingeweza kusaidia kuonesha kiwango cha upungufu wa wauzaji wa viuwatilifu ambao hawajapatiwa mafunzo. Kanzidata pia ingesaidia kwenye kuandaa mipango ya utekelezaji wa shughuli za mafunzo kwa wauzaji wa viuwatilifu. Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa mpango-kazi na utaratibu wa kurudia kutoa mafunzo kwa wauzaji wa viuwatilifu. Jambo hili ni muhimu kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara kwenye muundo wa utengenezaji na majina ya viuwatilifu.

Kutoka kwenye halmashauri sita ambazo timu ya ukaguzi ilizitembelea, ilibainika kuwepo kwa wauzaji wa viuwatilifu ambao hawakuwa wamepata kabisa mafunzo kama Sheria ya Udhibiti wa Mimea ya Mwaka 1997 inavyowataka. **Jedwali 4.13** linatoa maelezo Zaidi.

**Jedwali 4.13: Hali ya utoaji wa mafunzo kwa wauzaji wa viuwatilifu**

| Jina la Duka la Viuwatilifu | Mwaka Biashara Ilipoanza | Idadi ya Training | |
|---|---|---|---|
| | | Mafunzo ya Usajili | Urudiwaji wa Mafunzo |
| Duka la Viuwatilifu 1 | 2010 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 2 | 2015 | 1 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 3 | 2013 | 1 | 2 |
| Duka la Viuwatilifu 4 | 2016 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 5 | 2008 | 1 | 3 |
| Duka la Viuwatilifu 6 | 2015 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 7 | 2016 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 8 | 2008 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 9 | 1994 | 1 | 2 |
| Duka la Viuwatilifu 10 | 2015 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 11 | 2010 | 1 | 1 |
| Duka la Viuwatilifu 12 | 2005 | 0 | 0 |
| Duka la Viuwatilifu 13 | 1999 | 0 | 0 |

**Chanzo**: *Uchambuzi uliofanywa na Wakuguzi kutoka kwenye Mahojiano na Mofisa wa halmashauri zilizotembelewa (2018)*

**Jedwali 4.13** linaonesha kuwa wauzaji wa viuwatilifu 5 kati ya 13 walipatiwa mafunzo kabla ya kuanza kuuza viuwatilifu. Kati ya wauzaji hawa 5, wauzaji 4 walipata mafunzo ya marudio toka kwa CNFA/TAGMARK ambayo yalidhaminiwa na Mradi wa Wauzaji wa Pembejeo uliopo chini ya Wizara ya Kilimo.

Ilibainika pia kuwa licha ya mafunzo kutolewa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuatilifu kwa wauzaji wa viuwatilifu, si wauzaji wote walikuwa wanatoa huduma kwenye maduka yao. Ripoti ilibainisha kuwa wafanyakazi waliokuwa wanatoa huduma kwenye maduka mengi ya pembejeo hawakuwa na elimu ya usimamizi wa viuwatilifu. Kwa mfano, maduka 10 kati ya 13 yaliyotembelewa, wafanyakazi wake hawakupata mafunzo yeyote ya usimamizi wa viuwatilifu. Ilibainika pia kuwa kulikuwa na wauzaji wa viuwatilifu ambao

hawakupata kabisa mafunzo ya usimamizi wa viuwatilifu kama Sheria ya Udhibiti Mimea inavyotaka. Kwa mfano, katika maduka ya wauzaji 13 yaliyotembelewa, kulikuwa na wauzaji 8 ambao hawakuwa wamepata mafunzo kabisa.

***(b) Usambazaji hafifu wa maarifa kwa wauzaji wa mbegu na mbolea***

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea zinatakiwa ziwe na mipango ya utoaji wa elimu kwa wauzaji wa mbolea na mbegu ili kuhakikisha kuwa mbegu na mbolea zinazouzwa zinakidhi viwango. Mapitio ya ripoti za mwaka kwa kipindi cha ukaguzi huu yalibainisha kuwa mafunzo kwa wauzaji wa mbegu na mbolea yalifanyika mara moja tu. Ilibainika zaidi kuwa licha ya kuwa baadhi ya wauzaji wa pembejeo za kilimo walikuwa na elimu ya jumla kuhusu kilimo, wauzaji waliokutwa kwenye maduka hayo hawakuwa na elimu. Wauzaji hawakuweza kutoa hata elimu ya jumla kwa wakulima kuhusu matumizi ya mbolea na mbegu.

Kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na timu ya ukaguzi kwenye sampuli chache zilizochaguliwa kwa wauzaji wa mbegu na mbolea kutoka halmashauri zilizotembelewa za Hai, Mbeya, Kalambo, na Masasi, asilimia 80 ya wauzaji hawakuwa na elimu ya kilimo. Hii inaonesha kuwa wauzaji hao hawawezi kutoa ushauri wanapowauzia wakulima mbegu na mbolea.

**4.4.2 Uenezaji hafifu wa maarifa kwa maofisa ugani**

Kazi kubwa ya maofisa ugani kwenye halmashauri ni kuelimisha wakulima kuhusu masualaya ya kilimo ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata haki yao ya kuelemishwa kwa muda sahihi. Kadhalika, ilibainika kuwa maofisa ugani kwenye halmashauri hawakuwa wamewezeshwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima ambazo zilikuwa zinajumuisha matumizi sahihi ya mbolea, mbegu, na viuwatilifu. Wizara ya Kilimo na TAMISEMI zilibainisha kuwa hakukuwa na tathmini ya uhitaji wa mafunzo iliyofanyika wala kutoa elimu kwa maofisa ugani.

Kwa mfano, ilibainika kuwa maofisa ugani wengi hawakuwa wanapatiwa mafunzo vizuri kuhusu namna bora ya usimamizi wa viuwatilifu. Ilibainika kuwa maofisa hao walikuwa wanategemea elimu waliyoipata wakati wakiwa vyuoni. Hali hii ilibainika wakati timu ya ukaguzi ilipotembelea halmashauri sita za Itilima, Urambo, Morogoro, Masasi, Njombe, na Arusha. Katika halmashauri hizo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa nusu ya maofisa ugani waliohojiwa katika halmashauri za Morogoro, Njombe, na Masasi hawakuwa wamepata mafunzo ya usimamizi wa viuwatilifu. Kadhalika ilibainika kuwa kwa wale waliopatiwa mafunzo, mafunzo hayo yalifanyika miaka kumi iliyopita. Katika Halmashauri za Itilima na Urambo, maofisa ugani

wote waliohojiwa hawakuwa wamepatiwa mafunzo kabisa kwenye eneo la usimamizi wa viuwatilifu.

Kadhalika, kwa mujibu wa mapitio ya ripoti za utekelezaji kutoka katika halmashauri zilizotembelewa, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18, halmashauri ziliweza kuendesha mafunzo kidogo kwa maofisa kilimo kuhusu matumizi bora ya mbegu na mbolea. Iliripotiwa zaidi kuwa kwa halmshauri zilizotembelewa za Hai, Mbeya Vijijini, Masasi, na Kalambo, maofisa ugani waliopatiwa mafunzo walikuwa 2,120 kati ya 5000 ambao walipangwa kupatiwa mafuzno ikiwa ni sawa na asilimia 42 kwa miaka ya fedha kuanzia 2015/16 hadi 2017/18.

### 4.4.3 Uenezaji hafifu wa maarifa kwa wakulima

Kwa mujibu wa mahojiano na maofisa wa Wizara ya Kilimo na TAMISEMI, wakulima katika halmashauri wanatakiwa kuwezeshwa katika njia mbalimbali za kisasa za kilimo kama uaandaaji wa shamba, matumizi ya mbolea, utumiaji mbegu bora, mbinu za umwagiliaji na matumizi ya viuwatilifu.

Ilibainika kwamba njia kuu inayotumika kueneza ujuzi mpya wa kilimo na kilimo cha kisasa kwa wakulima ni matumizi ya shamba daras. Hivyo, maofisa ugani hasa vijijini wana jukumu la kuhamasisha wakulima kuunda vikundi vya wakulima vya wanachama kati ya 25 na 30 ili waweze kujifunza kupitia mashamba madogo kama shamba darasa. Wakaguzi walifanya tathmini ya uenezaji wa ujuzi wa matumizi sahihi na utunzaji wa pembejeo za kilimo na kugundua mapungufu yafuatayo.

***Mapungufu katika utoaji wa mafunzo ya viuwatilifu kwa wakulima***

Mahojiano yaliyofanyika baina ya timu ya ukaguzi na Maofisa wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, TAMISEMI, na halmashauri 6 zilizotembelewa yalibaini kuwa wakulima hawakupewa mafunzo ya kutosha ya utunzaji salama wa viuwatilifu. Pia, ilibainika kuwa TAMISEMI ilitoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa wakulima kupitia mamlaka za serikali za mitaa, lakini mafunzo hayo yalijumuisha elimu ya viuwatilifu kwa kiwango kidogo. Ilibainika kwamba katika halmashauri 6 zilizotembelewa, hayakutolewa mafunzo ya usimamizi wa viuwatilifu na masuala mengine ya kilimo.

Timu ya ukaguzi ilifanikiwa kushuhudia jinsi wakulima wanavyotunza na kutumia viuwatilifu. Kwa mfano, mkulima mmoja katika kijiji cha Ndatu alitunza viuwatilifu alivyonunua kwa kuning'iniza kwenye mti ambao upo karibu sana na jiko la nyumba yake. Katika kijiji cha Lagangabilili, mkulima alionekana akinyunyuzia viuwatilifu katika shamba la pamba bila kuvaa zana zinazoitajika kama kinga. Alivaa


mabuti na kofia ya pikipiki ambayo pia haikuwa kofia sahihi ya kukinga uso wake kama inavyooneshwa kwenye **Picha 4.1.**



**Picha 4.1:** Mkulima akiwa hajajikinga katika kijiji cha Lagangabilili Wilaya ya Itilima (Picha imepigwa na Timu ya Ukaguzi, Januari 17, 2018).

**Kielelezo 4.3** kinaonesha hali ya wakulima ambao hawajawezeshwa na elimu ya viuwatilifu katika halmashauri sita zilizotembelewa za Meru, Itilima, Urambo, Morogoro, Njombe, na Masasi.

**Kielelezo 4.3: Hali ya wakulima ambao hawajapokea mafunzo ya viuwatilifu kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18 katika halmashauri sita zilizotembelewa**




Kama inavyoonekana katika **Kielelezo 4.3**, zaidi ya asilimia 90 ya wakulima waliotembelewa hawakupewa elimu ya viuwatilifu na mafunzo ya utunzaji salama wa viuwatilifu.

### *(a) Mapungufu katika utoaji wa mafunzo kwa wakulima katika utumiaji mzuri wa mbegu na mbolea*

Ilibainika kuwa wakulima wachache walipata mafunzo ya matumizi mazuri na utunzaji wa mbegu na mbolea. Hii ilithibika kupitia taarifa za mafunzo za matumizi ya mbegu na mbolea kutoka halmashauri nne (4) zilizotembelewa ambazo ni Hai, Mbeya Vijijini, Kalambo, na Masasi. Kuanzia miaka ya fedha 2013/14 hadi 2017/18, jumla ya wakulima 13,874 kati ya 19,581 waliopangwa kufundishwa, ndiyo walifundishwa kama **Jedwali 4.14** linavyoonesha kwa kina.

**Jedwali 4.14: Hali ya wakulima waliofundishwa katika halmashauri nne zilizotembelewa kutoka mwaka 2013/14 hadi 2017/18**

| Mwaka wa Fedha | Waliopangwa kufundishwa | Waliofundishwa | Wasiofundishwa | Asilimia ya wasiofundishwa |
|---|---|---|---|---|
| 2013/14 | 1708 | 1203 | 505 | 30 |
| 2014/15 | 3592 | 2396 | 1196 | 33 |
| 2015/16 | 4693 | 3288 | 1405 | 30 |
| 2016/17 | 4578 | 3415 | 1163 | 25 |
| 2017/18 | 5010 | 3572 | 1438 | 29 |

**Jedwali 4.14** linaonesha kuwa asilimia 25 hadi 33 ya wakulima hawakufundishwa jinsi ya kutumia vizuri mbegu na mbolea.

### 4.4.4 Sababu zinazochangia kuwepo kwa mapungufu katika utoaji elimu

Sababu nyingi zimeorodheshwa kuwa ndizo huchangia udhaifu katika utoaji wa elimu wa matumizi mazuri ya pembejeo za kilimo kama zinavyoelezwa hapa chini.

**i. Sababu zinazochangia kuwepo kwa mapungufu katika utoaji wa elimu kwa wauzaji wa membejeo**

***Kukosekana kwa mpango wa mafunzo***

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu inatakiwa kuandaa mpango wa mafunzo ili kuwezesha kufanyika kwa mafunzo ya viuwatilifu kwa wauzaji wa viuwatilifu. Hata hivyo, imebainika hapakuwepo na mpango wa kimaandishi ulioandaliwa kuelekeza utoaji wa mafunzo ya viuwatilifu kwa wauzaji wa viuwatilifu. Sababu kuu ya kutokuwepo kwa mpango wa mafunzo ni ukosefu wa vipaumbele katika uandaaji wa mipango licha ya uelewa wa faida zake kwa wakulima na watumiaji wakuu wa pembejeo za kilimo.

**ii. Sababu zinazochangia kuwepo na mapungufu katika utoaji elimu kwa maofisa ugani**

***Upungufu wa fedha zinazotolewa kwa kitengo cha kilimo, umwagiliaji, na ushirika katika halmashauri***

Licha ya mamlaka za serikali za mitaa kupewa waraka wa fedha ambao unaagiza kubakisha asilimia 20 ya mapato yaliyokusanywa kutoka katika shughuli za kilimo ili kuwezesha kitengo kinachosimamia shughuli hizo, imebainika kuwa utekelezaji wa waraka huo umekuwa finyu.

Hii imeonekana katika halmashauri[7] zote zilizotembelewa kuwa fedha zilizobakishwa zilikuwa chini ya asilimia 20. Pia, ilionekana mafunzo yasiyo sahihi yaliyotolewa kwa maofisa ugani yaliathiri utekelezaji wa majukumu yao ya kuwashauri na kuwafundisha wakulima katika utumiaji na utunzaji wa viuwatilifu, mbegu, na mbolea.

**Sababu zinazochangia kuwepo kwa mapungufu katika utoaji elimu kwa wakulima**

***(a) Ukosefu wa tathmini ya mahitaji***

Maofisa wa Wizara ya Kilimo na TAMISEMI wamethibitisha kwamba hakukuwa na tathmini ya mahitaji ya mafunzo iliyofanyika ili kutambua mahitaji ya mafunzo kwa wakulima.

***(b) Upungufu wa maofisa ugani***

Ilibainika kwamba kulikuwa na upungufu wa maofisa ugani katika ngazi za vijiji na kata ambao walitakiwa kutoa mafunzo kwa wakulima katika halmashauri[8] zilizochaguliwa kama sampuli ya ukaguzi. Kwa mfano, halmashauri zilizotembelewa za Hai, Mbeya, Masasi, na Kalambo zilikuwa na maofisa ugani 272 kati ya 531 waliohitajika, sawa na asilimia 51 ya maofisa ugani wanaohitajika.

(c) ***Mafunzo ya wakulima kuwa nje ya mamlaka ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu***

Ilibainika kuwa ni mara chache sana Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu wanatoa mafunzo ya viuwatilifu kwa wakulima kwa sababu si jukumu lake. Mafunzo yanayotolewa kwa wakulima yanategemea maombi yanayowasilishwa na wakulima wenyewe kupitia makundi yao. Kwa kawaida, Taasisi hutoa mafunzo kwa wakufunzi kwa wakulima waliochaguliwa. Vilevile, hutoa mafunzo kwa wauzaji wa pembejeo vijijini ambao ni wakulima wanaofundishwa kuuza viuwatilifu kwenye vijiji vyao.

---

[7] Meru, Morogoro, Itilima, Urambo, Njombe, Masasi, Hai, Mbeya, na Kalambo

[8] Meru, Morogoro, Itilima, Urambo, Njombe, Masasi, Hai, Mbeya na Kalambo

## 4.5 Mapungufu katika Ufuatiliaji wa Shughuli za Udhibiti wa Ubora

### 4.5.1 Ufuatiliaji wa shughuli za udhibiti wa ubora wa viuwatilifu unaofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu

Mapitio ya Mpango-mkakati wa Mwaka wa Wizara ya Kilimo yalionesha kuwa ufuatiliaji wa shughuli za viuwatilifu unafanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu. Hata hivyo, ilibainika kuwa si vipengele vyote vya udhibiti wa ubora kwenye viuwatilifu kama usajili, ukaguzi, na ufahamu vilijumuishwa. Ufuatiliaji unaofanywa na Wizara ya Kilimo umejikita kwenye udhibiti wa shughuli za usajili kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ulinzi wa Mimea, na Kamati Ndogo za Kitaalamu za Uidhinishaji na Usajili wa Viuwatilifu ili kuhakikisha viuwatilifu vilivyosajiliwa vinavigezo vinavyohitajika.

Imebainika pia kuwa maofisa wote kutoka Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu wanalinganisha shughuli za ukaguzi zinazofanywa kwa wauzaji wa viuwatilifu na mipakani kuwa ndiyo shughuli za ufuatiliaji. Hii imeonekana kuwa dalili za Wizara ya Kilimo kushindwa kuweka vipaumbele kwenye ufuatiliaji wa shughuli zingine za viuwatilifu zinazojumuisha ukaguzi na mafunzo kinyume na kazi zake kama wizara inayosimamia utekelezaji wa sera zilizoundwa na miongozo mbalimbali iliyowekwa kuongoza eneo la viuwatilifu.

### 4.5.2 Sababu zinazochangia mapungufu kuwepo kwenye ufuatiliaji wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu

***Vipaumbele hafifu kwenye shughuli za ufuatiliaji na tathmini***

Ilibainika kuwa Wizara ya Kilimo haikuweka kipaumbele kwenye utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini. Ilibainika zaidi kuwa hali hii ilichangiwa na bajeti ndogo inayotengwa kwa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

***Matumizi hafifu ya zana za kukusanyia takwimu***

Imebainika kuwa Wizara ya Kilimo inatumia Mfumo wa Takwimu za Kilimo kuingizia na kukusanya taarifa muhimu zinazohitajika wizarani. Huu ni mfumo unaowezesha taarifa na mawasiliano kutoka ngazi ya chini hadi kufika wizarani, ingawa hautumiwi ipasavyo kupata taarifa zinazohitajika kutoka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu.

***Ukosefu wa muundo wa ufuatiliaji na mpango-kazi wa ufuatiliaji***

Mahojiano kati ya wakaguzi na maofisa wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu yalibaini kuwa hakukuwa na muundo wa ufuatiliaji wa kimaandishi wala mpango-mkakati ulioandaliwa wa kuwezesha

ufuatiliaji wa utendaji wa shughuli za udhibiti wa ubora zinazofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu.

Kwa hiyo, Wizara ya Kilimo imeshindwa kufuatilia maendeleo ya malengo yaliyowekwa kuhakikisha pembejeo za kilimo zinazosambazwa kwenye masoko zina viwango vinavyohitajika. Hivyo, kuna uwezekano wa kuwa na matatizo ambayo hayatapata suluhu kwa muda mrefu.

# SURA YA TANO

# USIMAMIZI WA MILIPUKO YA MAGONJWA NA VISUMBUFU VYA MIMEA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa ufanisi wa utekelezaji wa mikakati ya usimamizi wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Milipuko ya magonjwa na mimea imepunguza kiwango kikubwa cha uhakika wa chakula katika maeneo mbalimbali. Aidha, imeathiri biashara za kimataifa na upatikanaji wa masoko kwa sababu ya uzalishaji wa kiwango cha chini cha mazao.

Matokeo ya ukaguzi yamejumuisha masuala manne ambayo ni udhibiti, kinga, uratibu, na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za usimamizi wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Yafuatayo ni mapungufu yaliyojitokeza.

## 5.2 Mifumo Hafifu ya Kukinga Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea

Wizara husika bado haijaunda mifumo madhubuti ya kujikinga na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea kwa sababu ya udhaifu wa ukaguzi mipakani, na uelewa mdogo wa wakulima katika matumizi ya njia unganishi za kujikinga na visumbufu vya mimea na upatikanaji mdogo wa mbegu bora za kilimo.

Yafuatayo ni mapungufu yaliyoonekana kwenye changamoto za uzuiaji wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.

### 5.2.1 Udhaifu wa ukaguzi mipakani

Ukaguzi umebaini kuna kuna viuwatilifu vinavyoingia mipakani kwa kiwango kikubwa bila kukaguliwa na wakaguzi wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu. Ilibainika kuwa ukaguzi ulikuwa haufanyiki ipasavyo kutokana na upungufu wa wakaguzi na vifaa vya ukaguzi katika mipaka kama ilivyoainishwa hapo chini.

- *Upungufu wa wakaguzi mipakani:* Ilionekana kwamba kuna upungufu wa wakaguzi wa afya ya mimea waliopangwa mipakani walio chini ya Wizara ya Kilimo. Kati ya mipaka 51 inayotambulika, Wizara inafanya kazi katika mipaka 36 tu. Hii inamaanisha kuwa moja ya tatu ya mipaka ya Tanzania haina wakaguzi wa afya ya mimea na hivyo kuleta changamoto ya udhibiti wa uingizaji wa viuwatilifu kutoka nchi za nje.

- *Upungufu wa vifaa vya ukaguzi*: Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na udhaifu wa ukaguzi uliofanyika mipakani kutokana na uhaba wa wakaguzi. Pia, wakaguzi wachache waliopo walikabiliwa na uhaba wa vitendeakazi ambavyo ni muhimu katika ukaguzi

mipakani. Mfano wa vitendeakazi hivyo ni vyumba vya kutunzia ubaridi, vifaa vya kukinga uso wakati wa kazi, glavu, lenzi, na kompyuta yenye programu ya kuwezesha kuchunguza visumbufu hatarishi vya mimea.

- *Udhaifu katika kufuata viwango vya ukaguzi na taratibu*: Ukaguzi ulibaini udhaifu katika kufuata viwango vya ukaguzi na taratibu zake wakati wa ukaguzi mipakani. Hii ilithibitishwa katika mipaka ya Namanga, Mutukula, na Tunduma ambapo ilionekana viwango vya ukaguzi na taratibu zake kutofuatwa wakati wa ukaguzi. Hali hii ilisababishwa na kuwepo wafanyakazi ambao hawakujengewa uwezo wa kuchunguza visumbufu hatarishi vya mimea na kutokuwa na uelewa wa utaratibu na viwango vya ukaguzi kwa shughuli za afya ya mimea, na kuwa na orodha iliyopitwa na wakati ya visumbufu vya mimea.

### 5.2.2 Uelewa mdogo wa wakulima katika matumizi ya njia za mpango jumuishi wa udhibiti wa visumbufu vya mimea

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu, Wizara ya Kilimo, na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI ilitakiwa kuandaa mpango wa mafunzo ili kuwezesha mafunzo ya viuwatilifu kwa wauzaji, wakulima, na maofisa ugani. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa mpango huo. Vilevile, ilibainika kuwa hamna tathmini ya mahitaji ya mafunzo iliyofanyika kuonesha uhitaji wa mafunzo kwa wakulima na maofisa ugani.

Hivyo, kumekuwa na upungufu wa mafunzo yanayotolewa na maofisa ugani kwa wakulima kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 5.1**. Kiwango kidogo cha mafunzo kilichotolewa hakikuweza kufundisha masuala yanayohusiana na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Hivyo, udhaifu umeonekana katika uenezaji wa elimu ya visumbufu vya mimea na milipuko ya magonjwa kwa maofisa ugani na wakulima. Hali hii imepelekea kukosekana kwa uelewa wa kutosha katika kukabiliana na changamoto za milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea katika maeneo mbalimbali.

**Jedwali 5.1: Idadi ya wakulima waliofundiswa udhibiti wa visumbufu vya mimea na magonjwa katika halmashauri kuanzia mwaka 2011-2015**

| Halmashauri | Idadi ya watu wanaojishughulisha na kilimo | Idadi ya wakulima iliyopangwa kufundishwa | Idadi ya wakulima waliofundishwa | % Wakulima waliofundishwa |
|---|---|---|---|---|
| Mbarari | 270,465 | 120 | 0 | 0 |
| Nanyumbu | 135,771 | 0 | 0 | 0 |
| Bahi | 175,401 | 0 | 0 | 0 |
| Meru | 285,131 | 13,000 | 0 | 0 |
| Masasi | 313,117 | 1200 | 200 | 17 |
| Muleba | 540,310 | 549 | 549 | 100 |
| Lushoto | 177,818 | 223 | 223 | 100 |


***Chanzo***: *Ripoti za Maendeleo za kuanzia mwaka 2011-2015 kutoka halmashauri zilizotembelewa*

**Jedwali 5.1** linaonesha kuwa katika halmashauri saba zilizotembelewa, wakulima wa halmashauri nne hawajapata elimu kuhusu Mpango Jumuishi wa Udhibiti wa njia za kujikinga dhidi ya visumbufu vya mimea kuanzia mwaka 2011 hadi 2015.

Sababu ya upungufu wa mafunzo ni udhaifu wa kuwa na vipaumbele katika mafunzo ya wakulima. Pia, maofisa ugani waliopo hawakuwa na ujuzi wa kisasa kuhusu magonjwa na visumbufu vya mimea, na hivyo kushindwa kueneza maarifa mapya kwa wakulima kuhusu visumbufu vya mimea na magonjwa.

Matokeo yake, upungufu wa mafunzo kuhusu Mpango Jumuishi wa Udhibiti wa visumbufu vya mimea kwa wakulima umepunguza uwezo wa wakulima kuweka njia madhubuti za kujikinga dhidi ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, baada ya mafunzo, mavuno yaliongezeka kutoka tani 0.8/hekta hadi tani 3.2/hekta. **Kielelezo 5.1** kinaonesha ongezeko la mavuno baada ya mafunzo.

**Kielelezo 5.1: Matokeo ya mafunzo kwa kiwango cha uzalishaji (mavuno kwa tani/hekta)**




***Chanzo:** Mlinganisho wa Mkaguzi kwa kutumia taarifa ya Ripoti ya Utafiti Shirikishi ya Nanyumbu, 2015*

**Kielelezo 5.1** kinaonesha umuhimu wa mafunzo ya visumbufu vya mimea na milipuko ya magonjwa kwa wakulima. Uchambuzi unaonesha kuwa mwaka 2007/08 kabla ya mafunzo, mavuno yalikuwa pungufu kwa tani 2/hekta; ila baada ya mafunzo kutolewa kwa wakulima kuanzia mwaka 2008 hadi 2015 kumekuwa na maboresho kwenye mavuno ya wakulima hadi kufikia tani 3.2/hekta.

### 5.2.3 Upatikanaji mdogo wa mbegu bora za kilimo na viuwatilifu ili kuzuia milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Wakulima walipewa ruzuku ya pembejeo za kilimo lakini hazikuwa za kutosha kuwafikia wakulima wote nchini. Wakulima wachache tu ndiyo walifanikiwa kupata mbegu bora na viuwatilifu. Hali hii ilisababishwa na usambazaji mdogo wa pembejeo kwa wakulima. Mara nyingi kumekuwa na ucheleweshaji wa mbegu bora kupitia ruzuku. Wakulima wanapoomba ruzuku wamekuwa wakipata kipindi ambacho si cha uzalishaji kutokana na ucheleweshaji.

Hii imethibitishwa katika halmashauri saba zilizotembelewa na wakaguzi. **Jedwali 5.2** inaonesha kwa kina mchanganuo wa ruzuku ya mbegu ya mahindi katika Halmashauri ya Meru na Kata ya Kikwe.

**Jedwali 5.2: Mchanganuo wa ruzuku ya mahindi kwa wakulima wa Kata ya Kikwe**

***Chanzo:*** Ripoti ya usambazaji wa Pembejeo za Kilimo ya Kata ya Kikwe

| Mwaka | Kijiji | Ruzuku Iliyoombwa kwa Idadi ya Wakulima | Ruzuku Iliyotolewa kwa Idadi ya Wakulima | Asilimia ya Ruzuku Iliyotolewa |
|---|---|---|---|---|
| 2013/14 | Karangai | 311 | 57 | 18 |
| | Maweni | 250 | 50 | 20 |
| | Kikwe | 212 | 300 | 140 |
| | Nambala | 301 | 50 | 17 |
| 2014/15 | Karangai | 0 | 0 | 0[9] |
| | Maweni | | | |
| | Kikwe | | | |
| | Nambala | | | |
| 2015/16 | Karangai | 587 | 200 | 34 |
| | Maweni | 418 | 200 | 48 |
| | Kikwe | 450 | 200 | 44 |
| | Nambala | 591 | 300 | 51 |

**Jedwali 5.2** linaonesha mahitaji ya pembejeo za kilimo (mbegu zinazohimili magonjwa) ni makubwa ikilinganishwa na pembejeo zilizotolewa. Kwa vijiji vingi, pembejeo zilizotolewa ni pungufu kwa nusu ya maombi ya pembejeo (mbegu) kutokana na udhaifu kwenye tathmini ya mahitaji ya wakulima na upungufu wa bajeti kuwezesha upatikanaji wa mbegu.

**Sababu zinazochangia upatikanaji mdogo wa mbegu bora na viuwatilifu**

*(i)* *Udhaifu kwenye tathmini ya mahitaji ya wakulima*: Pembejeo nyingi za kilimo zitolewazo ni pungufu ya nusu ya mahitaji ya wakulima kutokana na udhaifu kwenye tathmini ya mahitaji ya wakulima.

*(ii)* *Ukaguzi dhaifu kwa wauzaji wa mbegu*: Mapitio ya mipango ya mwaka na ripoti za utekelezaji za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18 zinaonesha kuwa mpango wa ukaguzi wa mwaka ulilenga idadi pungufu ya nusu ya wauzaji halisi wa mbegu. Wauzaji wengi wa mbegu hawakukaguliwa kuhakikisha iwapo mbegu zinazouzwa kwa wakulima zinahimili magonjwa na visumbufu vya mimea. **Jedwali 5.3** linaonesha idadi ya wauzaji wa mbegu waliokaguliwa kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18.

**Jedwali 5.3: Idadi ya wauzaji wa mbegu iliyopangwa kutembelewa kwa ukaguzi kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18**

[9] Maombi yalifanywa baada ya kupokea taarifa kutoka kwa mamlaka za serikali za mitaa baada ya kupokea ruzuku kwa mwaka 2014/2015 lakini halmashauri hazikupokea ruzuku

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Wauzaji Waliosajiliwa | Wauzaji Waliokaguliwa | Asilimia ya Wauzaji Waliokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 2014/15 | 525 | 105 | 20 |
| 2015/16 | 765 | 0 | 0 |
| 2016/17 | 827 | 296 | 36 |
| 2017/18 | 987 | 296 | 30 |

**Chanzo**: Mpango wa utekelezaji kuanzia mwaka *2013/14 hadi 2017/18*

**Jedwali 5.3** linaonesha wastani wa asilimia 22 wa jumla ya wauzaji wa mbegu walikaguliwa kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18.

*(iii)* *Ukaguzi dhaifu kwa wauzaji wa viuwatilifu kwenye masoko:* ilibainika kuwepo kwa viuwatilifu vilivyo chini ya kiwango kwenye masoko. Hii imesababishwa na udhaifu kwenye ukaguzi wa viuwatilifu masokoni. Hali hii ilisababisha pia kuwepo kiwango kikubwa cha viuwatilifu vilivyo chini ya kiwango kwa wakulima. Kwa mfano, mapitio ya taarifa za ukaguzi za Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Disemba 2017 yanaonesha kuwa viuwatilifu "Abamite, Doom, Boss, Lava, Lethal, na Romectin" viliuzwa kwenye masoko bila kusajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu. Viuwatilifu vingi ambavyo vipo chini ya kiwango vilionekana kwenye mikoa iliyopo mipakani, ambayo ni Mtwara, Mbeya, Kigoma, Tanga, Kagera, na Arusha.

*(iv)* *Upungufu wa wauzaji wa pembejeo waliosajiliwa wenye elimu ya ubora wa viuwatilifu sokoni*. Ukaguzi umebaini kuwa elimu ya ubora wa pembejeo za kilimo ikiwemo viuwatilifu na mbegu kwa wauzaji pembejeo imetolewa lakini imeonekana wauzaji waliosajiliwa wanaotarajiwa kuuza pembejeo bora kwa wakulima ni wachache ikilinganishwa na mahitaji.

**Athari za upatikanaji mdogo wa mbegu bora za kilimo na viuwatilifu**

Hii inasababisha wakulima kutumia mbegu mbalimbali za asili ambazo zina uwezo mdogo wa uzalishaji na ambazo zipo hatarini kuathiriwa na magonjwa na visumbufu vya mimea. Hali hii inasababisha wakulima kupata kiwango kidogo cha mavuno na kusababisha uhaba wa chakula na mapato kupungua. Pia, imeonekana kuwa utumiaji wa viuwatilifu visivyo na ubora unaleta changamoto mbalimbali ikiwemo kuvuna mazao hafifu zaidi ya ilivyotarajiwa na wakulima.

## 5.3 Udhaifu kwenye Njia za Udhibiti wa Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea

Njia za udhibiti wa magonjwa na visumbufu vya mimea hazijazingatiwa ipasavyo na Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI kama inavyotakiwa na Sheria ya Afya ya Mimea ya Mwaka 1997 kama inavyofafanuliwa katika sehemu zifuatazo:

### 5.3.1 Uchambuzi wa kina hafifu uliofanyika kwenye kubaini milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Kwa kuwa Tanzania ni mwanchama wa IPPC, inawajibu wa kuwa na mfumo wa uchunguzi wa kina ili kubaini mapema milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Mfumo wa uchunguzi wa kina wenye ufanisi unasaidia kudhibiti na kupunguza uharibifu wa mazao. Visumbufu vya mimea aina ya viwavijeshi vinagundulika kwa njia ya utabiri wa kienyeji kupitia mitego aina ya felemoni. Wizara ya Kilimo ikishirikiana na utabiri wa kienyeji wa Viwavijeshi iliweza kuongeza usambazaji wa mitego aina ya filemoni ipatayo 400 katika halmashauri 29 kuanzia mwaka 2002.

Ukaguzi umebaini kuwa mitego iliyopo Kijiji cha Chigugu Wilayani Masasi inafanya kazi vizuri; lakini mitego iliyopo katika Wilaya ya Bahi ilionekana haifanyi kazi kutokana na ukosefu wa chambo cha kuweka kwenye mitego na uwezo wa kurekebisha mitego hiyo. Kadhalika, kulikuwa na mlipuko mkubwa wa ugonjwa wa mahindi katika maeneo ya Wilaya ya Meru, lakini wakulima na maofisa ugani hawakuwahi kupewa elimu ya kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo. Hali hii inaonesha kuwa licha uchambuzi wa kina ulifanyika, uenezaji wa elimu kwa wakulima na maofisa ugani bado umekuwa tatizo. Hali hii iliwaathiri wakulima kwa njia nyingi ikiwemo uhaba wa chakula na kupotea kwa mapato. Zaidi ya hapo, kushindwa kufanya uchunguzi wa kina kumechangia kukosekana kwa orodha ya visumbufu vya mimea ngazi ya kitaifa ambayo ni muhimu kwenye soko la mazao ya kilimo.

### 5.3.2 Mfumo wa kutolea taarifa na utekelezaji hafifu wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Katika kipindi cha utabiri wa matukio ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea, wakulima hutoa taarifa kwa Ofisa ugani wa kijiji, ambae nae kwa kupitia Ofisa ugani wa halmashauri anatoa taarifa kenywe Ofisi ya kanda ya Usalama wa mimea.Baada ya hapo, Ofisa wa usalama wa mimea wa kanda anachukua hatua, au kama tukio lililotolewa taarifa linaitaji wizara ya kilimo kuingilia kati, wanapeleka taarifa wizarani.

Utoaji taarifa wa matukio ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea umeonekana kutofuata muundo wa ngazi za uongozi, pia kumebainika udhaifu kwenye ushirikiano kati ya Wizara ya kilimo na

TAMISEMI licha ya kuwa TAMISEMI ndiye anayewajibika kusimamia halmashauri zote nchini.Hii ni kwa sababu,kutokana na muundo wa serikali za mitaa ,maofisa kilimo wote wanawajibika kwa halmashauri husika ambazo zipo chini ya TAMISEMI, ila issue za zinazohusiana na utaalamu wa kilimo zaidi huwa zinaratibiwa na wizara ya Kilimo.

Taarifa ambazo zilitumwa TAMISEMI zimeonesha kuwa ni taarifa za Miradi ya Maendeleo ya Kilimo (DADPs), na taarifa za utekelezaji ambazo zimeonesha kujumuisha suala la milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea kwa kiwango kidogo sana.Hii inaonesha masuala ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea havikupewa kipaumbele.

Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa hii imechelewesha utekelezaji wa shughuli za milipuko ambao unaitaji msaada wa kitaalamu kutoka wizara ya kilimo, sababu maofisa kilimo wengi wameonekana kufuatisha muundo wa ngazi za uongozi mfano TAMISEMI.

### 5.3.3 Mapungufu katika uandaaji wa Mipango inayozingatia viashiria hatarishi ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Wizara ya kilimo na halmashauri saba zilizotembelewa zilibainika kutumia Mpango Jumuishi (IPM) wa kujikinga na visumbufu vya mimea, kama mpango unaozingatia viashiria hatarishi ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalionekana katika mfumo huo:

Licha ya Wizara ya Kilimo kuwa na mipango mbalimbali inayozingatia viashiria hatarishi, mipango hiyo imeonekana kuandaliwa kwa dharura pale milipuko inapotokea. Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Kilimo, TAMISEMI, na mamlaka za serikali za mitaa hawana mipango inayohusiana katika kukabiliana na milipuko, kana kwamba halmashauri zote zinakutana na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea inayofanana.

Ukaguzi ulibaini kuwa halmashauri 4 kati ya 7 zilizotembelewa hazikuandaa mipango kwa sababu haikuwa kipaumbele chao. Mapitio ya muhtasari wa bajeti ya 2015 kutoka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu na mipaka mitatu iliyotembelewa imeonesha utekelezaji wa mipango ya viashira hatarishi haitekelezwi na taasisi hizi.

Hii imesababishwa na Wizara ya Kilimo na halmashauri kutoandaa kutoipa vipaumbele mipango inayozingatia viashiria hatarishi vya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.

### 5.3.4 Mfumo dhaifu wa kutunza taarifa za milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Mfumo mzuri wa kutunza taarifa ni chombo muhimu kinachohitajika katika kurahisisha uchambuzi wa magonjwa na visumbufu vya mimea, pia kuweza kuonesha kiwango cha usambaaji wa mlipuko wa magonjwa na visumbufu vya mimea nchini. Ilibainika kwamba kuna udhaifu katika mfumo wa kutunza taarifa wa milipuko. Katika maeneo yote yaliyotembelewa na wakaguzi ilionekana mifumo ya kutunzia taarifa ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea ni dhaifu.

Halmashauri nyingi zimeshindwa kutekeleza na kufunga mfumo wa kutunzia takwimu za kilimo ili kuweza kutunza kumbukumbu za masuala ya kilimo. Hii imesababishwa na kutokuwa na maofisa wenye uelewa na mfumo huo. Kwa mfano, katika Wilaya za Muleba na Meru wakaguzi walishindwa kuingia kwenye mfumo huo kwa sababu ya kutokuwepo kwa ofisa mwenye uelewa na mfumo huo.

Ukosefu wa vitendeakazi kama kompyuta na huduma za intaneti kumepelekea halmashauri nyingi kushindwa kutoa kwa wakati taarifa za milipuko ya magojwa na visumbufu vya mimea kati ya halmashauri na Wizara ya Kilimo. Pia, taarifa zinazopokelewa na wizara hazikuonesha uhalisia wa matatizo ya milipuko iliyopo katika halmashauri husika.

### 5.3.5 Mapungufu katika Mfumo wa ufuatiliaji na mrejesho wa taarifa katika shughuli za usimamizi wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Kulingana na Mpango-mkakati wa Miaka Mitano (2011-2016) wa TAMISEMI na Wizara ya Kilimo, zote zina jukumu la kufanya ufuatiliaji baada ya milipuko ya visumbufu vya mimea na magonjwa kutokea na kupata mrejesho kutoka kwa wadau husika hasa halmashauri.

Hata hivyo, imeonekana Wizara ya Kilimo hufanya ufuatiliaji pale milipuko inapotokea. Ukaguzi pia umebaini kuwa Wizara ya Kilimo hupokea taarifa za milipuko kutoka halmashauri lakini haipokei taarifa za utekelezaji na hivyo inaiwia vigumu Wizara ya na TAMISEMI kuweza kufanya ufuatiliaji wa milipuko. Sababu kuu ya kushindwa kutuma taarifa za utekelezaji kutoka halmashauri saba zilizotembelewa ilikuwa TAMISEMI inashughulikia zaidi shughuli za kiutawala kuliko za kitaalamu.

Ilionekana pia kuna mapungufu katika mfumo wa ufuatiliaji na urudishaji taarifa na Wizara ya Kilimo na TAMISEMI. Katika halmashauri saba (7) na taasisi tano za utafiti zilizochukuliwa kama

sampuli, imebainika kuwa ufuatiliaji ulikuwa unafanyika kama dharura tu pale matukio ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea ikitokea. Sababu ya kushindwa kufanya ufuatiliaji ni ukosefu wa mipango ya kutekeleza shughuli za ufuatiliaji wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.

Kutokana na mapungufu katika ufuatiliaji, hakukuwa na ushirikishanaji mzuri wa taarifa za utekelezaji wa shughuli za milipuko. Hii imepelekea kushindwa kudhibiti milipuko katika halmashauri mbalimbali.

Kwa sasa, Wizara ya Kilimo imejaribu kukabiliana na masuala ya milipuko kupitia Mfumo wa Taarifa za Kilimo ambao unawawezesha maofisa wenye ujuzi wa mfumo huo kutoka halmashauri kuweza kuingiza taarifa ambao upo kwa ngazi ya Wizara. Zaidi ya hapo, maofisa kilimo, umwagiliaji, na ushirika wanatakiwa kutoa taarifa za kilimo wizarani moja kwa moja. Hali hii inasaidia wizara kupata taarifa na kujibu kwa haraka.

## 5.4 Ushirikiano Hafifu katika Usimamizi wa Shughuli za Visumbufu vya Mimea na Magonjwa

Kushirikishana kwa taarifa miongoni mwa wadau wakuu ni jambo muhimu sana ili kusaidia kufanikisha usimamizi wa visumbufu vya mimea na magonjwa ya mazao. Ripoti ya ukaguzi imebaini kwamba mapungufu katika kushirikishana taarifa baina ya wadau wa sekta hii ni kama ifuatavyo.

### 5.4.1 Ushirikiano hafifu katika ngazi ya mkoa

Ukaguzi ulibaini kuwa kipindi cha milipuko ni mikoa miwili tu (Kagera na Arusha) kati ya mikoa 6 iliyochaguliwa kwa ukaguzi ndiyo iliweza kushirikiana na mkoa baada ya mlipuko wa magonjwa aina ya MLND na BXW.

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba kuna udhahifu kwenye ushirikiano wa kupeana taarifa za milipuko kwenye ngazi za mkoa na wilaya. Ofisa kilimo mkoa ana wajibu wa kutoa taarifa TAMISEMI juu ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Hata hivyo, ilibainika kwamba ripoti hazikujumuisha taarifa hizo za namna milipuko ilivyoshughulikiwa na mamlaka za serikali za mitaa pamoja na Wizara ya Kilimo. Hii ni kwa sababu Wizara hufanya kazi pamoja na mamlaka za serikali za mitaa katika kuzuia milipuko ya magonjwa bila kuhusisha mkoa.

Hii imepelekea kuwa ngumu kwa halmashauri kuratibu shughuli za masuala ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea kwa sababu haina taarifa ya milipuko hiyo. Kwa hivyo, imekuwa ngumu

kwa ofisi za mikoa kuweka mipango ya njia mbalimbali za kupambana na milipuko hiyo.

Kadhalika, TAMISEMI na ofisi za mikoa hazikuwa na taarifa za milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea jambo lililosababisha ugumu kwa TAMISEMI pamoja na ofisi za mikoa kupanga namna ya kupambana na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.

### 5.4.2 Ushirikiano hafifu kati ya Wizara ya Kilimo na wadau wengine

Ushirikiano hafifu ulionekana katika ngazi tofauti kama inavyojadiliwa hapa chini:

***i. Uratibu dhaifu kati ya serikali na sekta binafsi***

Ukaguzi ulibaini kuwa kuna ushirikiano hafifu baina ya wadau mbalimbali kama Wizara ya Kilimo, mashirika yasiyo ya kiserikali, pamoja na mamlaka za serikali za mitaa katika usimamizi ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Japokuwa kulikuwa na makubaliano kati ya serikali na sekta binafsi, baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali yalikuwa yanatoa huduma bila kuwasiliana na Wizara ya Kilimo au mamlaka za serikali ya mtaa. Hii iliathiri uratibu na ufatiliaji wa utekelezaji wa kazi mbalimbali.

***ii. Uratibu dhaifu baina taasisi za kiserikali***

Ukaguzi ulibaini uwepo wa uratibu duni baina ya maofisa kutoka Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu waliopo katika mipaka ya nchi. Wakaguzi kutoka Kitendo cha Afya ya Mimea katika mipaka hawakuwa na maabara yenye vifaa vya kutosheleza kwa ajili ya kufanya vipimo vinavyohitajika kwa mizigo iliyoshikiliwa kwa ufuatiliaji zaidi. Hivyo, maofisa wa Kitengo cha Afya ya Mimea huwa wanatuma sampuli kwenda Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu kwa ajili ya vipimo zaidi.

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na mfumo maalumu ambao ulisaidia ushirikishaji wa kufanya vipimo na matokeo ya vipimo baina ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu na Kitendo cha Afya ya Mimea. Hali hii ilisababisha baadhi ya mizigo kushikiliwa kwa muda mrefu bila kuwa na uhakika wa usalama wa mizigo hiyo.

### 5.4.3 Kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwenye milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea

Ukaguzi ulionesha kuwa kuna mfumo duni wa ufuatiliaji wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea katika ngazi mbalimbali kama inavyoelezwa hapa chini.

### i. Ufuatiliaji unaofanyika na Wizara ya Kilimo

Kitengo cha Huduma za Afya ya Mimea na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuatilifu ndizo zenye jukumu la kudhibiti milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea katika mipaka na kwa wakulima.

*Ufuatiliaji na tathmini kwenye maeneo ya mipakani*

Mapitio ya mpango wa bajeti wa kati wa mwaka 2013/12 na 2014/15 yalionesha kuwa kazi za ufuatiliaji zinazofanywa na Kitengo cha Afya ya Mimea hujumuisha kufanya ufuatiliaji na tathmini katika mipaka na kwenye kitengo cha kudhibiti visumbufu kwa kutumia viumbe hai ili kuweza kudhibiti na kuzuia magonjwa na visumbufu.

Pia, Mpango huo wa kati ulionesha kuwa shughuli nyingine zilizopangwa ni kufanya ufuatiliaji kwenye maeneo ya mipaka. Hata hivyo, ilibainika kuwa kazi za ufuatiliaji hazikufanyika kama zilivyopaswa kutokana na ufinyu wa bajeti.

*Ufuatiliaji wa viuwatilifu unaofanywa na Wizara ya Kilimo*

Wizara kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuatilifu inapaswa kuhakikisha kuwa viuwatilifu vinavyotumika vinawezesha kikamilifu kukabiliana na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea. Ufuatiliaji ulifanyika katika mipaka na kwa wauzaji wa pembejeo ili kuhakikisha kuwa viuwatilifu ambavyo havijasajiliwa haviingizwi wala kusambazwa nchini.

Ilibainika kuwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuatilifu huwa inafanya ufuatiliaji bila kuwa na mipango. Ufuatiliaji huwa unafanyika pale tu panapokuwa na malalamiko ya viwango duni vya viuwatilifu sokoni. Ilibainika pia kuwa kazi hizo za ufuatiliaji hazikuwa zinafanyika kwa maeneo yote.

### ii. Ufuatiliaji na tathmini ya visumbufu vya mimea na magonjwa unaotekelezwa na TAMISEMI

Ilibainika kuwa TAMISEMI hufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sekta mbalimbali ndani ya mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka. Hata hivyo, ilibainika kwamba ufuatiliaji wa magonjwa na visumbufu vya mimea haukufanyika kama ilivyopaswa. Hakukuwa na kipaumbele kilichowekwa kwenye shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea katika ngazi za mamlaka za serikali ya mitaa. Ilibainika kuwa mkazo uliwekwa kwenye shughuli za uratibu wa Mradi wa Maendeleo ya Kilimo, ambao haukuzingatia masuala ya usimamizi wa magonjwa na visumbufu vya mimea.

*Ufuatiliaji katika ngazi ya serikali za mitaa*

Ufuatiliaji na tathmini kwa ngazi ya mamlaka za serikali ya mitaa hutekelezwa na Kitengo cha Sera na Mipango. Hata hivyo, ilibainika

kwamba mamlaka za serikali za mitaa hufanya ufuatiliaji wa magonjwa na visumbufu vya mimea pale panapokuwa na milipuko. Sababu ya hali hii kutozingatia na kujumuisha kazi za ufuatiliaji wakati wa kutengeneza mipango. Hii ilipelekea matumizi makubwa ya raslimali hasa muda na fedha katika kudhibiti milipuko katika maeneo mbalimbali nchini.

# SURA YA SITA

## UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI

### 6.1 Utangulizi

Nchini Tanzania kilimo kimekuwa ni cha shaka na kisichokuwa na tija kutokana na uwepo wa mvua zisizotabirika kwa sababu ya ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi. Ili kupunguza utegemezi wa mvua na kupunguza upungufu wa chakula mara kwa mara, ni muhimu kuhakikisha upanuzi wa wigo wa ufikaaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo muhimu ili kuongeza uzalishaji wa mazao.

Sura hii inabainisha matokeo ya ukaguzi wa shughuli za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Ukaguzi huu umeonesha baadhi ya mapungufu ya Wizara ya Kilimo kupitia tume yake ya Taifa ya Umwagiliaji wakati wa usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Changamoto zimeonekana katika maeneo yote ya upembuzi yakinifu na utekelezaji wa shughuli za ujenzi. Katika eneo la shughuli za ujenzi, zimegusa maeneo ya ucheleweshaji wa kukamilisha ujenzi, ongezeko la gharama za ujenzi, na ubora endelevu wa shughuli za ujenzi. Matokeo ya jumla yameoneshwa katika kipengele cha 6.2, na matokeo ya kina yameoneshwa hapa chini.

### 6.2 Usimamizi Usiojitosheleza wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika Hatua Zote za Mipango na Utekelezaji

Ukaguzi huu umebaini kuwa katika kanda tulizotembelea, shughuli za ujenzi wa miradi ya umwagiliaji hazikusimamiwa kwa utoshelevu. Matokeo yake ni ujenzi wa skimu za umwagiliaji nje ya muda wa mkataba, gharama kuwa juu zaidi ya makubaliano ya kimkataba, na sehemu nyingine ubora wa kazi kuwa duni.

Upembuzi yakinifu haukupangwa vizuri kwa sababu ya kutokupewa kipaumbele kutokana na uhaba wa fedha ambao ni endelevu katika kanda za umwagiliaji. Ilibainika kuwa asilimia 76 ambayo ni sawa na skimu 63 kati ya skimu 83 zilizopitiwa zilijengwa nje ya muda wa kimkataba (zilichelewa).

Ukaguzi huu uligawa sababu za uchelewaji wa kukamilika kwa ujenzi wa miradi katika makundi ambayo ni mpango wa ujenzi usio sawa, usanifu usio na uhalisia, na ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi. Pia, asilimia 40 ambayo ni sawa na miradi 31 ilijengwa ikiwa na ongezeko la gharama. Jumla ya ongezeko la gharama za miradi lilikuwa shilingi milioni 665.6 kwenye kanda zote zilizotembelewa. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 2.9 ya jumla ya fedha zote za gharama ya miradi. Ongezeko hili lilitokana na ukosefu wa weledi

kwa wakandarasi, ongezeko la kazi, na usanifu usio na uhalisia. Kwa ujumla, ujenzi wa skimu zenye ongezeko la muda na gharama umesababisha moja kwa moja ucheleweshaji wa huduma za miundombinu zilizokusudiwa kwa wakulima. Maelezo ya kina ya matokeo ya ukaguzi huu ni kama inavyooneshwa katika vipengele vinavyofuata.

### 6.3 Mipango Isiyojitosheleza katika Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Ili kubaini uwezekano wa ujenzi wa mradi wa umwagiliaji, sheria ya umwagiliaji inataka miradi yote itekelezwe baada ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu. Upembuzi yakinifu hutoa dira kwa ajili ya kutathmini chaguo la namna ya kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji.

Mapitio ya randama za mipango ya bajeti na mahojiano yaliyofanyika na wahandisi wa miradi ya umwagiliaji katika kanda yalibaini kuwa katika kipindi cha miaka ya fedha 2014/15, 2015/16, na 2017/18 kanda za umwagiliaji za Morogoro na Mwanza hazikupanga kufanya upembuzi yakinifu. Pia, kanda ya Kilimanjaro haikufanya hivyo kwa miaka ya fedha 2016/17 na 2017/18. Ilibainika kuwa katika mapitio ya miaka ya fedha kuanzia 2014/15 hadi 2017/18 kanda za Mtwara na Mbeya ndizo zilizopanga kufanya upembuzi yakinifu.

Aidha, ilibainika kuwa jumla ya pembuzi yakinifu 360 zilipangwa kufanyika na zilizotekelezwa ni kumi na moja (11) tu. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 3 ya pembuzi yakinifu zote zilizopangwa kufanyika. **Jedwali 6.1** linaonesha utofauti kati ya idadi ya pembuzi yakinifu zilizopangwa kutekelezwa na zilizotekelezwa.

**Jedwali 6.1: Utofautiano kati ya idadi ya pembuzi yakinifu zilizopangwa kufanyika na zilizotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2017/18**

| Kanda ya Umwagiliaji | Jumla ya Pembuzi yakinifu zilizo pangwa kufanyika | Jumla ya Pembuzi yakinifu zilizofanyika | Utofauti (%) |
|---|---|---|---|
| Morogoro | 46 | 0 | 100 |
| Mbeya | 28 | 9 | 68 |
| Mtwara | 257 | 1 | 99.6 |
| Kilimanjaro | 16 | 0 | 100 |
| Mwanza | 13 | 1 | 92 |
| **Jumla** | **360** | **11** | **3** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa kikaguzi kwa kutumia taarifa kutoka kanda zilizotembelewa*

**Jedwali 6.1** linaonesha kuwa kanda za umwagiliaji za Morogoro na Kilimanjaro hazikutekeleza upembuzi yakinifu wowote kwa kipindi chote cha miaka minne. Kanda ya umwagiliaji ya Mbeya haikutekeleza mipango yake kwa asilimia 68. Kutokana na mapitio ya bajeti na mahojiano yaliyofanywa kwa maofisa umwagiliaji katika kanda zote tano zilizotembelewa, kulikuwa na sababu kuu mbili zilizochangia kushindwa kupanga na kutekeleza pembuzi yakinifu. Sababu hizo ni:

- Ofisi za kanda za umwagiliaji hazikuwa na wataalamu wa kutosha wenye ujuzi na vitendeakazi ili kupanga kwa kina na kutekeleza pembuzi yakinifu na shughuli nyingine za umwagiliaji.
- Ofisi za kanda zilikuwa na utegemezi mkubwa kwa fedha za wadau wa maendeleo ili kusaidia shughuli za umwagiliaji.

Ilibainika kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikuwa na upungufu kiuwezo (wataalamu wenye ujuzi na vitendeakazi) ili kupanga kwa kina na utekelezaji wa pembuzi yakinifu kwenye kazi nyingine za umwagiliaji. Kutokana na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu, miradi mingi ya umwagiliaji imeshindwa kuwa endelevu. Hii ilipelekea hatari ya uwekezaji uliowekwa kwenye umwagiliaji kutokuwa na uhalisia kitaalamu na kiuchumi. **Jedwali 6.2** linaonesha watumishi waliopo katika kanda zote za umwagiliaji zilizotembelewa na ukubwa wa eneo linalohudumiwa.

**Jedwali 6.2: Mahusiano kati ya eneo linalohudumiwa (wilaya) na idadi ya watumishi waliopo**

| Kanda za Umwagiliaji | Idadi ya Wilaya Zinazohudumiwa | Idadi ya Watumishi Wanaohitajika | Idadi ya Watumishi Waliopo | Tofauti | Asilimia ya utofauti |
|---|---|---|---|---|---|
| Morogoro | 19 | 69 | 32 | 37 | 54 |
| Mbeya | 16 | 42 | 27 | 15 | 36 |
| Mtwara | 15 | 31 | 16 | 15 | 48 |
| Kilimanjaro | 22 | 53 | 30 | 23 | 43 |
| *Mwanza* | 27 | 50 | 20 | 30 | 60 |

***Chanzo****: IKAMA na tathmini ya mahitaji kutoka Ofisi za Umwagiliaji za Kanda*

**Jedwali 6.2** linaonesha Kanda ya Umwagiliaji ya Mwanza inahudumia wilaya 27 na ina upungufu wa watumishi kwa asilimia 60. Kanda ya Umwagiliaji ya Morogoro ingawa inahudumia wilaya 19 ilikuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 54. Kanda ya Umwagiliaji ya Mbeya inahudumia wilaya 16 na ina upungufu wa watumishi kwa asilimia 36

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa ofisi za umwagiliaji za kanda zilikuwa na upungufu wa vitendeakazi, hasa kwa vifaa vilivyotumika kupima ubora katika shughuli zilizofanyika katika eneo la ujenzi. Mapitio ya ripoti ya mahitaji yalibaini kuna upungufu wa vitendeakazi vinavyohitajika wa asilimia 100 ya vipimaurefu na vifaa vya kupima mwendo wa maji. Aidha, kulikuwa na upungufu wa vitendeakazi kwa ajili ya kupima uimara wa zege na vifaa vya kupimia ardhi kwa asilimia 60.

Upungufu wa watumishi na vitendeakazi huathiri muda wa ukamilishaji wa miradi kwa kuwa kunakuwa na uwezekano wa mkandarasi kutofuata mpangokazi wake kutokana na upungufu wa wasimamizi. Pia, upungufu wa vitendeakazi unapelekea kuhitajika kwa muda mwingi ili kumaliza kazi ambayo ingeweza kumalizika kwa muda mfupi. Vilevile, upungufu wa vitendeakazi unaweza kupelekea athari kwenye ubora wa kazi. Mkandarasi anaweza kutumia mwanya huu kudanganya kuhusu vipimo na kiasi cha vitu viliyotumika bila kutambulika. Matokeo yake ukamilikaji wa miradi unaweza kupelekea ongezeko la gharama lisilo la lazima.

- **Utegemezi mkubwa wa fedha za wadau wa maendeleo ili kusaidia shughuli za umwagiliaji**


Ilbainika kuwa mchango wa wadau wa kilimo ulikuwa mkubwa kuliko mchango wa Serikali kwenye miradi ya umwagiliaji. Kwa miaka minne iliyopita, wadau wa maendeleo wamechangia kwa asilimia 89.6 ya fedha zote zilizotolewa kwenye miradi ya umwagiliaji.

Utegemezi huu umeathiri sana utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji kwani fedha nyingi zilizoidhinishwa kwenda Tume ya Umwagiliaji hazikutolewa kwa kiasi kikubwa kwa pande zote za Serikali na wadau wa maendeleo. Bajeti iliyopitishwa na Serikali na wadau wa maendeleo na kiasi kilichotolewa ni kama kilivyooneshwa kwenye **Kielelezo 6.1(a & b)**


**Kielelezo 6.1 (a&b): Ulinganisho kati ya fedha zilizoidhinishwa na zilizotolewa kati ya Serikali na wadau wa maendeleo kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2017/18**

**Kielelezo 6a** kinaonesha kuwa kiasi kikubwa cha fedha zilizoidhinishwa kwa miaka minne iliyopita kilitolewa na wadau wa maendeleo. Mwenendo unaonesha ongezeko la usaidizi wa kifedha kutoka shilingi bilioni 19 hadi 47 katika mwaka wa fedha 2017/18. Kwa upande mwingine, fedha zilizoidhinishwa ziliakisi kushuka kwa mchango wa Serikali kutoka shilingi bilioni 15 hadi 6 kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2017/18.

Kutokana na **Kielelezo 6b**, serikali ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 2.5 mwaka wa fedha 2016/17 na hakikutolewa kiasi kingine chochote katika miaka mitatu iliyobakia.




**Kielelezo 6.1a: Ulinganisho kati ya fedha iliyoidhinishwa kati ya Serikali na wadau wa maendeleo**




**Kielelezo 6.1b: Ulinganisho kati ya fedha iliyotolewa kati ya Serikali na wadau wa maendeleo**

Mwenendo huu wa kifedha unazifanya shughuli za umwagiliaji kuwa katika hatihati kutokana na utolewaji fedha usiokuwa wa kutegemewa kati ya Serikali na wadau wa maendeleo. Kutokana na utolewaji wa fedha usioaminika kwenda Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ofisi za umwagiliaji za kanda zimekuwa zikibadili vipaumbele vyake katika upangaji na ufanyaji wa upembuzi yakinifu. Kushindwa kupanga ufanyaji wa upembuzi yakinifu kumepelekea ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kuwa na ongezeko la gharama **(rejea jedwali 6.3).**

### 6.3.1 Ukosefu wa utoshelezi katika ufanyaji wa upembuzi yakinifu na utumiaji wa vipengele vya upembuzi yakinifu katika usanifu wa skimu za umwagiliaji

Ukaguzi huu umebaini kuwa asilimia 85 sawa na skimu 17 kati ya 20 zilizopitiwa zilifanyika bila ya kuwepo au kuwa na upembuzi yakinifu usio wa kina. Ilibainika kuwa ongezeko la gharama, ubora hafifu wa miundombinu iliyojengwa, na uchelewaji wa ukamilishaji wa ujenzi wa skimu ulichangiwa sana na ukosefu au ufanyaji usio wa kina wa upembuzi yakinifu.

Mahojiano yaliyofanywa na maofisa umwagiliaji wa kanda yalibainisha kuwa baadhi ya vipengele vya upembuzi yakinifu viliachwa kwani havikuwa vikipewa kipaumbele na wamiliki wa

miradi. Hii imekuwa ikipelekea kutokuwepo kwa bajeti ya ufanyaji vipengele hivyo va upembuzi yakinifu, na hata bajeti ikiwepo utolewaji wake ni mdogo. Kwa sababu hiyo, miradi mingi iliyokamilika inakumbwa na hatari ya tofauti za kiasili kama mabadiliko ya hali ya hewa kama vile mvua kubwa na ukame.

Kwa mfano, athari ya kurukwa kwa baadhi ya vipengele vya upembuzi yakinifu imeonekana katika skimu ya umwagiliaji ya Themi ya Simba ambapo kuta za mfereji zilianza kupinda kwa sababu ya uwepo wa udongo mweusi wenye tabia ya kutanuka na kusinyaa. Hali hii ilipelekea meneja wa mradi kutafuta kuidhinishiwa tofauti la ongezeko ili kurekebisha tatizo hilo. Hii ilipelekea ongezeko la gharama za mradi na utofauti wa shilingi milioni 11.8 **(rejea Picha 6.1).**

Athari nyingine ilibainika katika skimu ya umwagiliaji ya Wami-Luhindo, ambapo kipengele cha tathmini ya athari za mazingira na jamii vilipuuzwa. Matokeo yake, kalvati na kuta za mfereji za urefu wa takribani mita 10 ulivunjwa na maji kutokana na mvua kuwa kubwa. Ukaguzi ulibaini kuwa hapakuwa na njia zilizowekwa ili kakabiliana na athari hizi. Katika eneo hili hapakuwa na udhibiti wa shughuli za kilimo na mifugo na shughuli nyingine za kibinadamu ambazo zilipelekea kupanuliwa kwa mkondo wa maji hivyo kiasi cha maji kilichopita kwenye kalvati kilizidi kiasi kilichosanifiwa. Uharibifu huo uliongeza gharama za marekebisho. **Picha Na.6.2** inaonesha kalvati lililoharibika.

Kwa ujumla, ukaguzi huu ulibaini jumla ya shilingi milioni 112.6 zililipwa kama gharama za ziada zilizosababishwa na kutokufanyika kwa baadhi ya vipengere vya upembuzi yakinifu. Kwa maelezo zaidi rejea **Jedwali 6.3** linaloonesha matokeo ya kila athari iliyojitokeza kwa kila kipengele kilichoachwa.

**Jedwali 6.3: Vipengele vya upembuzi yakinifu vilivyoachwa na athari za kifedha zilizosababishwa**

| Kanda za Umwagiliaji | Skimu ya Umwagiliaji | Kipengele kilicho achwa | Tofauti ya kifedha (TSH millioni) |
|---|---|---|---|
| Kilimanjaro | Themi ya simba | Uchunguzi wa Udongo | 11.8 |
| | Kigongoni | Uchunguzi wa uimara chini ya ardhi | 4.9 |
| | Kirya | Uchunguzi wa uimara chini ya ardhi | 23 |
| Mwanza | Buhangaza | Usanifu wa awali | 26 |
| | Kyota | Usanifu wa awali | 4.9 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mbeya | Mgambalenga | Uchunguzi wa uimara chini ya ardhi | 42 |
| **Jumla** | | | **112.6** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi*

**Jedwali 6.3** linaonesha kuwa kuachwa kwa baadhi ya vipengele vya upembuzi yakinifu kumekuwa na athari katika miradi inayojengwa. Kanda ya Umwagiliaji ya Mbeya imekuwa na gharama za ziada shilingi milioni 42, ikifuatiwa na Buhangaza ambayo ilikuwa na tofauti ya shilingi milioni 26. Kama upembuzi yakinifu ungejumuisha vipengele vyote, kiasi hiki cha fedha kingetumika kujenga maeneo mengine ya mradi ambayo hayajakamilika.



***Picha 6.1:*** Athari ya udongo mweusi iliyosababisha sehemu ya ukuta wa mfereji wa skimu ya Themi ya Simba kupinda kuelekea ndani. Picha imepigwa na mkaguzi tarehe 26 Novemba, 2018



**Photo 6.2:** Kalvati lililoharibiwa na mvua (kwenye mduara mwekundu) na ujenzi wa vivushamaji vipya katika skimu ya umwagiliaji ya Wami-Luhindo. Uharibifu huu umechangiwa na kutofanyika kwa kipengele cha athari za mazingira. Picha imepigwa na mkaguzi tarehe 12 Julai 2018

## 6.4 Usimamizi usiojitosheleza kwenye shughuli za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupitia kanda zake za umwagiliaji imepewa mamlaka na Sheria ya Mmwagiliaji ya Mwaka 2013

kusimamia shughuli zote za umwagiliaji nchini. Licha ya kupewa mamlaka hayo, Tume bado haijayatumia kiusimamizi. Kutokana na usimamizi usiojitosheleza ilibainika kwamba asilimia 40 ya miradi iliyotekelezwa katika kipindi cha mapitio ilikuwa na ongezeko la gharama; wakati asilimia 76 ya miradi yote ilichelewa kukamilika.

Uchelewaji wa muda wa kukamilisha miradi, na kukamilisha miradi ikiwa na ongezeko la gharama huathiri ufikishaji wa huduma kwa wakulima. Vipengele vifuatavyo vinaelezea kwa kina ongezeko la muda na gharama za mradi.

### 6.4.1 Udhibiti usiojitosheleza kwenye usimamizi wa muda wa ukamilishaji wa ujenzi wa skimu za umwagiliaji

- **Ongezeko la Muda**

Timu ya ukaguzi ilifanya mapitio ya ripoti za maendeleo ya miradi na ripoti za ukamilishaji wa miradi na ilibainika kuwa asilimia 76 ya miradi yote iliyopitiwa ilichelewa kukamilika **(rejea Jedwali 6.5)**. Ilionekana kuwa ukamilisahji wa muda wa ujenzi katika skimu za umwagiliaji zilizopo kanda ya Morogoro ulikuwa ni wa asilimia 100.

Pia, ilibainika kuwa skimu zilizotekelezwa katika kanda ya umwagiliaji ya Mwanza zilichelewa kwa asilimia 63. Kanda nyingine za umwagiliaji miradi yake ilichelewa kwa zaidi ya asilimia 60. Uchelewaji wa muda wa kukamilisha ujenzi huweza kusababisha kuendelea kuharibika kwa miundombinu ambayo ingeweza kuwa imara kama ingekuwa imekamilika kwa wakati.


**Jedwali 6.5: Kiwango cha uchelewaji wa miradi ya umwagiliaji kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2017/18**

| Kanda za Umwagiliaji | Idadi ya miradi iliyo pitiwa | Idadi ya miradi iliyokamilika bila kuchelewa | Idadi ya miradi iliyokamilika kwa kuchelewa | Asilimia ya uchelewaji |
|---|---|---|---|---|
| Morogoro | 14 | 0 | 14 | 100 |
| Mbeya | 26 | 8 | 18 | 69 |
| Mtwara | 18 | 5 | 13 | 72 |
| Mwanza | 8 | 3 | 5 | 63 |
| Kilimanjaro | 17 | 4 | 13 | 71 |
| **Jumla** | **83** | **20** | **63** | **76** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Mkaguzi*

Kwa wastani, wa muda wa kimkataba wa miradi yote 83 ilikuwa siku 165, na ilibainika kuwa asilimia 25 ya miradi yote ilichelewa kwa zaidi ya siku 192. Uchelewaji huu ni zaidi ya wastani wa muda wa ujezi wa kimkataba. Wastani wa uchelewaji wa ukamilishaji wa

ujenzi umetofautiana kutoka kanda moja na nyingine kama ilivyooneshwa kwenye **Kielelezo 6.2.**




***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Mkaguzi*

**Kielelezo 6.2** kinaonesha siku za uchelewaji katika kanda zote zilizotembelewa. Ilibainika kuwa Kanda ya Morogoro ilikuwa na uchelewaji mkubwa, ambapo ujenzi ulichelewa kukamilika kwa wastani wa siku 370. Katika kanda hiyohiyo, kiwango cha chini cha uchelewaji kilikuwa siku 62 na kiwango cha juu kilikuwa siku 1054. Mapitio ya ripoti za maendeleo na mahojiano yaliyofanyika na maofisa wa miradi yalibaini kuwa programu ya kazi imekuwa ikipangwa katika kipindi cha mvua na katika kipindi cha mazao. Kwa upande mwingine, uchambuzi umebaini kuwa kanda ya umwagiliaji ya Kilimanjaro ilikuwa na wastani mdogo wa uchelewaji wa miradi, kwani ilichelewa kwa wastani wa siku 114. Katika kanda hiyohiyo, wastani wa chini wa uchelewaji ulikuwa siku 2 na wastani wa juu ulikuwa siku 297.

Mapitio ya ripoti za maendeleo ya miradi na ripoti za utekelezaji wa miradi[10]yalibaini sababu kuu za uchelewaji wa kukamilika kwa miradi ni:

- Udhaifu wa mkandarasi kutokana na kuwa na vifaa duni na upungufu wa wataalamu.
- Usanifu usio wa uhalisia
- Ubovu wa mpangokazi wa ujenzi
- Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi

[10] Repoti za eneo la ujenzi Namba 1-5 ya Skimu ya Umwagiliaji ya Lumuma, Ripoti za Maendeleo za mwezi Na.2 ya Chikwedu-Chipamanda; Taarifa ya Hali ya utekelezaji wa miradi kwenye kanda za Mtwara na Mbeya

Katika kila kanda zilizotembelewa, sababu hizi zimetengwa kutokana na zilivyojitokeza **(rejea Jedwali 6.6).**

| Sababu za Uchelewaji miradi | Kanda ya Umwagiliaji | | | | | Jumla ya kujirudia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Morogoro | Mbeya | Mtwara | Kilimanjaro | Mwanza | |
| | Idadi za Kujirudia | | | | | |
| Ubovu wa Mpangokazi wa ujenzi | 17 | 5 | 7 | 11 | 4 | 44 |
| Usanifu Usio wa uhalisia | 5 | 1 | 0 | 6 | 4 | 16 |
| Udhaifu wa mkandarasi kutokana na kuwa na vifaa duni na uchache wa wataalamu | 4 | 1 | 3 | 3 | 0 | 11 |
| Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi | 1 | 0 | 5 | 0 | 0 | 6 |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Mkaguzi kupitia ripoti ya hali ya miradi ya SSIDP I and II*

**Jedwali 6.6** linaonesha kuwa sababu ya ubovu wa mpangokazi wa ujenzi katika utekelezaji wa miradi ilijirudia mara mara 44. Hii ni kusema kwamba miradi mingi imekuwa ikichelewa kwa ajili ya mipangokazi mibovu ya ujenzi, kwani shughuli nyingi za ujenzi zilipangwa kufanyika wakati wa mvua au wakati kukiwa na mazao ya wakulima, ingawa miradi mingi ilikuwa na kipindi kidogo cha kimkataba.

Usanifu usio wa uhalisia ni sababu iliyofuata kwa kujirudia mara nyingi kama kisababishi cha ucheleweshaji wa miradi kukamilika. Sababu hii ilijirudia mara 16. Katika kanda zilizotembelewa, miradi iliyofanyika kanda ya Morogoro iliathirika zaidi na kuwepo kwa mpangokazi mbovu wa utekelezaji wa miradi, ambapo sababu hii ilijirudia mara 17 katika miradi yote iliyofanyika, ikifuatiwa na sababu ya usanifu usio wa uhalisia ambayo ilijitokeza mara 5. Sababu ya ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi ilijitokeza mara 5 katika miradi iliyotekelezwa katika kanda ya Mtwara. Sababu za ucheleweshaji wa ukamilfu wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji ni kama inavyoelezewa hapa chini.

- **Usanifu usio wa uhalisia**

Usanifu usio wa uhalisia ilikuwa ni kati ya sababu zilizochangia uchelewaji wa miradi, kwani kazi zilisimama ili kutafuta idhini ya


usanifu mpya, au kazi zilisimama kutokana na kupishana kati ya usanifu na hali halisi ya eneo la ujenzi. Kwa mfano, katika mradi wa umwagiliaji wa Kyota, kipengele namba 3.3 (vivusha maji katika umbali wa mita 480) katika makadirio ya gharama (BoQ) yenye thamani ya shilingi milioni 3.4 ilikuwa imeshafanywa katika mkataba uliopita. Haya ni matokeo ya kufanya usanifu bila ya kutembelea eneo la ujenzi na kuona hali halisi. Pia, kulikuwa na makosa katika hesabu za kupata kiasi cha nyavu za ujenzi na hivyo kupelekea tofauti ya kifedha ya shilingi milioni 4.9. Tofauti ni kati ya visababishi vilivyopelekea ongezeko la muda wa ujenzi kwa siku 127. Wakati huohuo, skimu ya umwagiliaji ya Mapama iliyo katika kanda ya Kilimanjaro ilikuwa na usanifu usio wa uhalisia kwani ilikuwa na upungufu wa baadhi ya vipimo na michoro ya tuta la kuzuia mafuriko. Matokeo yake kazi ilisimama ili kutafuta idhini ya siku 32.

- **Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi**

Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ulikuwa ni sababu ya uchelewaji wa ukamilishaji wa ujenzi wa miradi. Ukaguzi huu ulibaini kuwa miradi 5 kati ya 18 iliyojengwa katika kanda ya umwagiliaji ya Mtwara ilichelewa kwa sababu ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi. Pia, sababu hii ilionekana mara moja katika miradi 13 iliyotekelezwa katika kanda ya Morogoro. Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ilikuwa na athari kubwa katika maendeleo ya ujenzi wa miradi kama ilivyoonekana katika skimu ya umwagiliaji ya Nakahuga (**rejea Kielelezo 6.3**).

**Kielelezo 6.3: Athari za matokeo ya ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi kwenye maendeleo ya ujenzi wa mradi**

| | Siku 0 | Mwezi 1 | Mwezi 2 | Mwezi 3 | Mwezi 4 | Mwezi 5 | Mwezi 6 | Mwezi 7 | Mwezi 8 | Mwezi 9 | Mwezi 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia iliyojengwa | 0.0% | 0.0% | 12.0% | 24.0% | 30.0% | 31.0% | 31.0% | 33.0% | 40.0% | 41.0% | 43.0% |
| Fedha iliyotolewa | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 13.6% | 13.6% | 20.5% | 20.5% | 20.5% |




***Chanzo: Ripoti ya ufuatiliaji katika Skimu ya Nakahuga, tarehe 30 Aprili, 2018***

Kutokana na kielelezo 6.3, imeonekana kuwa, maendeleo ya kimradi yanategemea sana na mwenendo wa kifedha. Kwa mantiki hiyo, mkandarasi aliendelea kufanya kazi bila kulipwa kwa miezi 5, ambapo alifanikiwa kujenga asilimia 31 ya mradi kwa muda huo. Kwa miezi 5 iliyofuata, mkandarasi alifanikiwa kujenga asilimia 12 na kufanya jumla ya eneo la mradi lililojengwa kuwa ni asilimia 43 na muda wa mradi kuwa umekwisha, na jumla ya malipo yaliyolipwa kwa mkandarasi yalikua ni asilimia 20.5 pekee.

- **Udhaifu wa mkandarasi kutokana na kuwa na vifaa duni, na upungufu wa wataalamu**

Kulikua na matukio ambayo uchelewaji wa ukamilifu wa ujenzi, ulisababishwa na udhaifu wa wakandarasi walioletwa. Udhaifu wa wakandarasi umeelezewa kwenye maeneo yafuatayo:

- **Kutokuwepo kwa utoshelevu wa vifaa, mafundi mchundo na wafanyakazi wenye ujuzi**

Mapitio ya faili la miradi ya skimu za umwagiliaji za Buhangaza, na Kyota kutoka kanda ya umwagiliaji ya Mwanza, Chikwedu-Chipamanda kutoka kanda ya Mtwara, na Siginali kutoka kanda ya umwagiliaji ya Morogoro ilionesha kuwa, wakandarasi walitumia watumishi wasiokua na vigezo na ujuzi katika kazi. Mfano, skimu za umwagiliaji za Tulokongwa na Nyamweke, wakandarasi wake hawakuleta vifaa vya kutosha katika kazi zao za ujenzi. Kwa mfano mradi wa umwagiliaji wa tulo kongwa, mkandarasi aliondoa magreda mawili mara tu baada ya kulipwa fedha ya awali (advance payment). Athari zilizo bainishwa kutokana na udhaifu wa mkandarasi ni kama ilivyooneshwa kwenye **jedwali 6.9.1**

### 6.4.2 Kutokuwepo utoshelevu wa kudhibiti muda wa ukamilikaji wa mradi

- **Ongezeko la gharama za mradi**

Ilibainika kuwa miradi 31 kati ya 79 sawa na asilimia 40 ya miradi iliyopitiwa ilitekelezwa kwa gharama za juu zaidi ya makubaliano ya awali ya kimkataba. Kwa ujumla wake, asilimia 2.9 ya gharama zote sawa na shilingi milioni 665.6 ziliongezeka kwenye gharama za ujumla za kimkataba **(Rejea Jedwali 6.7).**

**Jedwali 6.7: Jumla ya Ongezeko la fedha kutoka kwenye mikataba ya awali**

| Kanda za Umwagiliaji | Jumla ya Mkataba wa awali (TSH Billioni) | Jumla ya kiasi halisia cha fedha ya mkataba (TSH Billioni) | Kiasi kilichoongezeka (TSH Billioni) | Asilimia iliyoongeeka |
|---|---|---|---|---|
| Morogoro | 3.71 | 3.724 | 0.014 | 0.37 |
| Mbeya | 10.601 | 10.853 | 0.252 | 2.4 |
| Mtwara | 3.515 | 3.648 | 0.133 | 3.8 |
| Kilimanjaro | 3.83 | 3.92 | 0.09 | 2.4 |
| Mwanza | 1.601 | 1.778 | 0.1766 | 11 |
| **Jumla** | **23.257** | **23.923** | **0.6656** | **2.9** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka kwenye ripoti za hali ya miradi*

**Jedwali 6.7** limeonesha kuwa katika kanda zilizotembelewa, asilimia iliyoongezeka ilianzia 0.37 hadi 11, ambapo Mwanza ndiyoiHakunaiokuwa na ongezeko la asiliia kubwa, kwani ilikua na asilimia 11, ambayo ni sawa na ongezeko la shilingi milioni 176. Kanda ya umwagiliaji ya Mtwara ilikua na ongeeko la gharama ya miradi kwa asilimia 3.8, ambyo ni sawa na shilingi milioni 133.

**Jedwali 6.8** linaonesha asilimia ya idadi ya skimu zilizojengwa zikiwa na ongezeko la gharama.

**Jedwali 6.8 Asilimia ya Skimu zilizojengwa juu ya gharama za kimkata za mradi**

| Kanda za Umwagiliaji | Jumla ya idadi ya skimu | Skimu zilizojengwa juu ya gharama za kimkataba | Asilimia | Idadi ya mikataba ya nyongeza |
|---|---|---|---|---|
| Morogoro | 10 | 2 | 20 | 2 |
| Mbeya | 26 | 10 | 38 | 21 |
| Mtwara | 17 | 8 | 47 | 6 |
| Kilimanjaro | 17 | 6 | 35 | 10 |
| Mwanza | 8 | 5 | 63 | 9 |
| **Jumla** | 78 | 31 | **40** | **48** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Mkaguzi kwa kutumia taarifa za hali ya miradi ya SSIDP*

Kutokana na **Jedwali 6.8**, ilionekana kuwa miradi 31 kati ya 78 sawa na asilimia 40 ya miradi yote ilikua na ongezeko la gharama za ujenzi. Hali hii ilikua kubwa katika kanda ya Mwanza, ambapo asilimia 63 ya miradi yote iliyojengwa hapo ilikua na ongezeko la gharama. Morogoro ilikua na ongezeko dogo la gharama za miradi kwani ni asilimia 20 ya miradi yote ndiyo iliyoogezeka gharama.

Kati ya kanda zilizotembelewa, Mbeya ilikua na jumla ya mikataba ya nyongeza 21 kaji ya mikataba 48 ilyoonekana. Ilibainika kuwa kanda ya Kilimanjaro, ilifuata kwa kuwa na mikataba mingi ya nyongeza kwani ilikua na mikataba 10 kati ya mikataba 48 ya nyongeza.

Kutokana na majarada ya miradi iliyopitiwa, ongezeko la gharma limesababishwa na sababu zifuatazo

- Udhaifu wa mkandarasi
- Ongezeko la kazi
- Usanifu usio na uhalisia

**Jedwali 6.9: Idadi ya sababu za miradi kuwa na ongezeko la gharama**

| Sababu ya ongezeko la gharama | Kanda ya Umwagiliaji | | | | | Jumla ya Sababu Zilivyojitokeza |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Morogoro | Mbeya | Mtwara | Kilimanjaro | Mwanza | |
| | Utokeaji wa Sababu | | | | | |
| Udhaifu wa mkandarasi | 1 | 1 | 1 | 4 | 2 | 9 |
| Ongezeko la kazi | 2 | 21 | 6 | 10 | 9 | 48 |
| Usanifu usio na uhalisia | 4 | 1 | 1 | 6 | 2 | 14 |

***Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi, 2019***

**Jedwali 6.9** linaonesha kulikuwa na ongezeko la mkataba wa kazi limejirudia mara 48 ukilinganisha na sababu nyingine. Hii inamaanisha kuwa ongezeko la kazi lilisababisha ongezeko la gharama za mradi kwenye ile miradi iliyopitiwa, kwa sababu kazi nyingi zilizoongezwa zilikua zimesababishwa na kutokuwepo kwa utoshelevu wakati wa ufanyaji upembuzi yakinifu.

Sababu za ongezeko la gharama za miradi zimeelezewa kama ifuatavyo:

- **Udhaifu wa mkandarasi**

Mapitio ya ripoti za maendeleo, na kumbukumbu za mahojiano na maofisa wa kanda, ilionesha kuwa, ubovu wa makandarasi umekua na athari sana kwenye maendeleo ya miradi. Udhaifu wa mkandarasi unachangiwa sana na usimamizi usiotesheleza wa meneja wa mradi na matokeo yake miradi inajengwa chini ya kiwango, ikiwa imechelewa kukamilika, na yenye ongezeko la gharama. Wakandarasi wengi inabidi kusimamiwa kwani wengi wao huwa na mradi zaidi ya mmoja wakati mtaji wao ni kidogo. Hivyobasi kunakua na hatari ya mkandarasi kuviondoa baadhi ya vifaa vyake na kuvipeleka eneo jingine la mradi kama hakuna meneja wa mradi aliye imara. Kwa mfano katika ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Tulokongwa, mkandarasi aliondoa magreda mawili mara tu baada ya kua amelipwa fedha ya awali wakati kazi haikua tayari imekamilika. Matatizo mengine ya wakandarasi na athari zilizojitokeza yameoneshwa katika **Jedwali 6.9.1.**

**Jedwali 6.9.1: Udhaifu wa wakandarasi na athari zilizojitokeza**

| Kanda ya Umwagiliaji | Skimu | Matatizo ya Mkandarasi yaliyobainishwa | Athari zilizoonekana |
|---|---|---|---|
| Kilimanjaro | Mapama | Mkandarasi alishindwa kumaliza mradi kwa wakati, ingawa alishapewa onyo | Mkandarasi alikatwa kiasi cha shilingi milioni 5.9 kama gharama za ucheleweshaji wa kukamili wa kazi |
| | Kituri | Mkandarasi alishindwa kumaliza mradi kwa wakati | Mkataba ulivunjwa |
| Morogoro | Signali | • Vifaa duni vya Mkandarasi<br>• Upungufu wa wataalamu wa kutosha | Mradi uluichelewa ka siku 483 |

| Kanda ya Umwagiliaji | Skimu | Matatizo ya Mkandarasi yaliyobainishwa | Athari zilizoonekana |
|---|---|---|---|
| | | • Ukosefu wa mtaji wa kifedha | |
| | Tulo/Kongwa | Mkandarasi alikua na uzoefu kwenye ujnzi wa barabara na majengo, lakini sio Umwagiliaji | Mradi uluichelewa ka siku 432 |
| Mtwara | Chikwedu-chipamanda | Mkandarasi hakuwa na wataalam muhimu na vifaa havikua eneo la ujenzi | Mradi uluichelewa ka siku 94 |

- **Nyongeza ya Kazi**

Katika kanda zilizotembelewa, Mbeya ilikua na nyongeza nyingi za kazi kupita kanda nyingine. Kati ya nyongeza za kazi 48 zilizobainishwa katika kanda zote tano, Mbeya ilikua na nyongeza 21 za kazi, wakati huo huo kanda ya umwagiliaji ya Kilimanjaro ilika na nyongeza za kazi 10. Ilibainika kuwa, katika nyongeza hizo zilizoonekana zilichangiwa na sababu nyingi lakini sababu iliyokuwa kuu ni usanifu usio na uhalisia kukosekana kwa utoshelevu kwenye makadirio ya gharama za ujenzi (BoQs) na ufanyaji wa upembuzi yakinifu usiojitosheleza.

- **Usanifu usio na uhalisia**

Ukaguzi huu ulibaini kuwa usanifu usio na uhalisia ulichangiwa sana na usanifu uliokua ukifanyika bila ya kuyatembelea maeneo husika Usanifu usiona uhalisia umeonekana katika skimu ya umwagiliaji ya Kyota, kipengele 3.3 (vivusha maji katika umbali wa mita 480), kwenye makadirio ya gharama za ujenzi (BoQ) chenye thamani ya shilling milioni 3.4, kilikuwa tayari kimekwisha fanyika katika kazi zilizo pita. Kiasi hiki hakikulipwa na ilibidi kipelekwe kwenye ujenzi wa bwawa ambao haukua umepangwa katika mkataba huo.

Wakati huo huo katika skimu ya umwagiliaji ya Mapama, katika kanda ya umwagiliaji ya Kilimanjaro, usanifu usio na uhalisia ulipelekea kuhamishwa kwa eneo la ujenzi kutoka urefu wa mita 600-1600 kwenda hadi sehemu nyingine mpya yenye mita 4000-5000. Pia ilibainika kuwa, katika mradi huo hapakuwepo na michoro ya tuta la kukingia mafuriko.

Gharama za ongezeko la utekelezaji wa skimu zilizo chini ya SSIDP zilikua sio kubwa sana kutokana na miradi kuwa na bajeti finyu. Ongezeko la gharama lilidhibitiwa kwa kupunguza wigo wa awali wa mradi **(Rejea jedwali 6.9.2)**

**Jedwali 6.9.2: Utofauti kwenye skimu uliopelekea kupunguza wigo wa awali**

| Kanda ya Umwagiliaji | Skimu | Utofauti uliopeleke kupuzwa kwa wigo wa awali wa mradi |
|---|---|---|
| Kilimanjaro | Kigongoni | • Usanifu wa ukuta wa kingo za banio zilibadilika kutoka kimo cha mita 3.4 kwenda mita 2.8<br>• Ongezeko la urefu wa vizuizi vya vipunguza kasi ya maji (stilling basin protection works) kwa mita 4.5 na ongezeko la urefu wa vipunguza kasi ya maji kutoka mita 22.47 hadi 23.85. |
| | Themi ya Simba | • Makosa katika kukadiria kiasi cha zege la chini kwenye makadirio ya gharama za ujenzi( B.O.Q) iliyopelekea kubadilika kwa usanifu wa mfereji(canal cross section)<br>• Uwepo wa udongo mweusi kwenye urefu wa mita 1,155 uliopelekea kuwekwa kwa zege la juu, na uwekaji wa tabaka la mchanga. Hii ilisababisha mabadiliko ya usanifu kwani mfereji ilibidi ukazwe kwa boriti (rainforced beam), na kusababisha gharama ya shilingi milioni 11.8 |
| Mwanza | Buhangaza | • Makosa katika kukokotoa kiasi cha nyavu za ujenzi (BRC) ambapo kwenye makadirio ya gharama ilionesha kiasi cha nyavu zilizo hitajika kuwa 3314.43 kg kwa urefu wa mita 1578.3m. Nyavu hizo zilikua zikitosha kwenye mfereji wenye urefu wa mita 466.55 pekee<br>• Mfereji uliokwisha chimbwa ilidhaniwa ni mita 1578.3 wakati ulikua mita 590 tu<br>• Makadirio ya gharama za ujenzi (BoQ ) yalishauri vigawa maji 10 vijengwe wakati vilihitajika vigawamaji 5 tu |
| | Kyota | Makosa katika kukotoa kiasi cha nyavu za ujenzi (BRC) kwani kiasi kilichotajwa kilikuwa kilo 847 kwa urefu wa mita 385. Kiasi hiki kilitosha kujenga urefu mita 119.23. Hivyo kiasi kilicho hitajika kilikua kilo BRC 1888.04 kwa urefu wa mita 385. |

***Chanzo**: Uchambuzi wa Mkaguzi kwa kutumia taarifa kutoka kwenye ripoti za maendeleo, 2019*

Athari za kupunguza wigo wa miradi ni kupungua kwa huduma ambazo ingebidi ziwakie wakulima kama mradi ungekua ukifanya kazi.

### 6.4.3 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji haikufanya udhibiti wa kujitegemea ili kuhakikisha viwango vinafikiwa

Katika miradi 20 iliyo angaliwa kutoka kwenye, kanda zilizotembelewa, hakuna kanda iliyofanya udhibiti wa kujitegemea. Hii ilisababishwa na mamlaka ya Tume pamoja na kanda zake hayatumiki kwa sababu maofisa wa umwagiliaji wa kanda wamekua wakifanya majukumu ya kutoa ushauri wa kiufundi (backstopping) badala ya usimamizi wa miradi. Ilibainika kua Mwongozo kabambe wa umwagliaji (Comprehensive guideline) unaotumika bado haujauishwa ili kuendana na matakwa ya sasa ya sharia ya umwagiliaji inayowataja maofisa wa umwagiliaji kanda kama wasimamizi wa shughuli zote za umwagiliaji.

Pia, usimamizi usiojitosheleza katika kazi za ujenzi ulibainika. Meneja wa mradi ndiye mwangalizi na msimamizi wa mkataba kwa niaba ya mmiliki wa mradi. Kwa miradi iliyokuwa ikisimamiwa na mameneja wa miradi kutoka halmashauri, imekua vigumu kusimamiwa na maofisa umwagiliaji kanda. Kwa sababu hiyo ufuatiliaji wa miradi hiyo umekua ukitegemea zaidi ripoti za maendeleo, ambazo hutumwa kwenda kanda, pamoja na barua za mialiko kwa ajili ya kuhudhuria vikao vya ujenzi (site meetings).

Ilibainika kuwa, Maofisa umwagiliaji kanda hawana mfumo maalumu wakuweza kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa miradi kutoka kwa mameneja wa miradi walio chini ya halmashauri, na matokeo yake kanda imekua ikitegemea ripoti za maendeleo kutoka kwa mameneja hao ili kufanya maamuzi. Maofisa umwagiliaji kanda hawana hali ya kujitegemea kwani hawezi kuchukua hatua yoyote pale sharia ya umwagiliaji inapovunjwa kwa sababu hawana mamraka ya kiutawala katika halmashauri.

Matokeo ya Kanda kutokufanya udhibiti unaojitegemea, ulibainishwa Zaidi katika kanda ya umwagiliaji ya Mbeya. Kwa mfano katika skimu ya umwagiliaji ya Mwenda-Mtitu (**Rejea picha 6.3),** kingo za kuta za mfereji hazikua zimejengewa ili kukinga maporomoka ya udongo ambayo yanaweza kuporomoka na kufunika mfereji wote kama usipo kingwa.



*Picha 6.3: Mfereji wa umwagiliaji wa Mwenda-Mtitu ambao uko katika hatari ya kufunikwa na udongo kama usipokingwa. Picha kama ilivyopigwa na mkaguzi tarehe 21 Julai, 2018*

# SURA YA SABA

# HUDUMA ZA UGANI

## 7.1 Utangulizi

Huduma za ugani ni moja ya masuala muhimu katika ukuzaji wa tija katika shughuli za kilimo na huleta mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya kilimo katika nchi. Huduma bora za ugani huleta hakikisho la upelekaji wa mbinu za kisasa za kilimo na uchakataji wa mazao yatokanayo na kilimo unaochangia ongezeko la uzalishaji na thamani ya mazao na bidhaa zitokanazo na kilimo. Sura hii ya Saba itajadili masuala yaliyobainika na yanayohusiana na utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima kama yalivyoripotiwa na kaguzi za ufanisi katika sekta ya kilimo kuanzia mwaka 2015 hadi 2019

Sura hii imejumuisha mambo mbalimbali yaliyobainishwa katika ripoti mbili za ukaguzi wa ufanisi pamoja na ripoti moja ya ufuatiliaji. Ripoti hizo ni:

- *Ukaguzi wa Ufanisi katika Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima*
- *Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Mikakati ya Udhibiti wa Milipuko ya Visumbufu na Magonjwa ya Kilimo*
- *Ufuatiliaji wa Ukaguzi wa Utoaji wa Huduma za Ugani*

Utoaji wa huduma za huduma za ugani nchini Tanzania hufanywa kwa kiasi kikubwa na Wizara ya Kilimo pamoja na Ofisi ya Raisii Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Jukumu la Wizara ya Kilimo ni kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera na miongozo ya kilimo katika utoaji wa huduma za ugani. Ofisi ya Raisii Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inawajibu wa kusimamia utekelezaji wa jumla wa huduma za ugani kupitia Sekretarieti za Mikoa.

Kwa hiyo, sura hii inatoa maelezo na uchambuzi wa mambo makuu yaliyojitokeza ambayo yanahusu utoaji wa huduma za ugani moja kwa moja. Sura inaangazia mambo tofauti yahusuyo miongozo ya utoaji wa huduma za ugani, udhaifu katika mipango ya utoaji wa huduma za ugani, utoaji wa huduma za ugani na usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za ugani zinazotolewa kwa wakulima nchini Tanzania.

## 7.2 Utoaji hafifu wa huduma za ugani kwa wakulima

Utoaji wa huduma za ugani hivi sasa haujawa kamilifu na pia hautoi hakikisho la upelekaji wa mbinu za kisasa za ukulima na uchakaji wa wa mazao yatokanayo na kilimo unaochangia kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao na bidhaa zitokanazo na kilimo. Mambo

yaliyojitokeza katika kaguzi zilizofanywa kwenye sekta ya kilimo zimebainisha udhaifu katika utoaji wa huduma za ugani kuhusu mbinu za utoaji wa huduma za ugani pamoja na uhamasishaji wa raslimali.

### 7.2.1 Uchache wa mbinu za utoaji huduma za ugani

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba kulikuwa na mbinu chache za utoaji wa hudumza za ugani kwa wakulima. Miongozo ya utoaji wa huduma za ugani inatoa nafasi ya utoaji huduma za ugani kupitia mbinu mbalimbali kama vile vitalu vya maonyesho/mashamba darasa, siku za wakulima mashambani, safari za kutembeleana mashambani/safari za mafunzo, machapisho ya ufundi wa kilimo, miongozo ya mafunzo, vipindi vya redio au televisheni, maonyesho ya video, maonyesho ya kilimo, vifaa vya teknohama ikijumuisha simu za mkononi, tovuti, barua pepe pamoja na matumizi ya vituo vya raslimali za kilimo vya kata. Hata hivyo, kaguzi ilibaini kwamba utoaji wa huduma za ugani ulitumia kwa kiasi kikubwa mbinu ya vitalu vya maonyesho huku kukiwa na matumizi machache ya vituo vya raslimali kilimo vya kata.

Kaguzi ya ufuatiliaji iliyofanyika baadae ilibaini kwamba Wizara ya Kilimo imeshaanza kutumia vipindi vya redio na televisheni katika utoaji wa huduma za ugani kuanzia mwezi Mei mwaka 2018. Hata hivyo, uchambuzi wa idadi ya maofisa ugani wanaotumia miongozo kwa mwaka kadiri ya matakwa ya mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika awali katika huduma za ugani hukufanywa.

Kaguzi zilibaini pia nyenzo za kiteknohama ziliundwa na kutumiwa na watoaji huduma za ugani. Miongozo ya mafunzo ya mashamba darasa; vipindi vya redio na televisheni; vitalu vya maonyesho; na miongozo ya maonyesho ya wakulima ya nane nane. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wenye kujitosheleza wa matumizi ya miongozo ya mashamba darasa na vitalu vya maonyesho.

### 7.2.2 Mbinu zisizo na ufanisi za utoaji wa huduma za ugani

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba wakulima wlikuwa hawashirikia katika vitalu vya maonyesho or programu za mashamba darasa ambazo zilikuwa zikitumika kama mbinu mojawapo za kuhamasisha mbinu bora za kilimo. Kumekuwa na kiwango cha chini sana cha utumiaji wa teknolojia zilizoboreshwa za kilimo na mbinu bora za kilimo ni licha ya kuwa ni mbinu inayotumika zaidi katika kupeleka teknolojia mpya za kilimo na mbinu nzuri za kilimo. Jedwali la 7.1 linaonesha ni kwa kiwango gani wakulima walishiriki katika vitalu vya maonyesho au mashamba darasa.

**Jedwali 7.1: Uwiano wa wakulima waliojiunga na kushiriki katika mashamba darasa katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa.**

| Mwaka wa Fedha | Jumla ya Wakulima[11] | Jumla ya Wakulima Walio katika Mashamba Darasa | Uwiano wa Wakulima Wanaoshiriki katika Mashamba Darasa |
|---|---|---|---|
| 2009/10 | 1,041,492 | 11,722 | 1:100 |
| 2010/11 | 1,077,834 | 8,912 | 1:100 |
| 2011/12 | 1,118,956 | 12,103 | 1:100 |
| 2012/13 | 895,644 | 9,025 | 1:100 |

***Chanzo:*** *Taarifa za kila Mwezi za Kilimo katika Kata*

Jedwali 7.1 Linaonesha kwamba kulikua na mwitikio mdogo na mwamko mdogo wa wakulima kujiunga na mashamba darasa katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa. Katika mikoa yote iliyotembelewa uwiano unaonesha kwamba katika kila wakulima 100 ni mkulima mmoja tu alikuwa amejiunga na kushiriki katika mafunzo ya mashamba darasa. Katika miaka kadhaa, idadi ya wakulima wanaoshiriki katika programu za mashamba darasa imekuwa ikipungua. Idadi ya wakulima katika mashamba darasa imekuwa ikipungua kutokana na kutokuwa na idadi ya kutosha ya maofisa ugani wanaoweza kuandaa na kutoa mafunzo kwa wakulima kwa mashamba darasa.

### 7.2.3 Uhamisho mdogo wa teknolojia na mbinu bora za kilimo

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba uhamisho wa maarifa na hasa katika teknolojia za kilimo na mbinu bora za kilimo kwa wakulima ulikuwa mdogo kutokana na kuwa na idadi ndogo ya mashamba darasa. Muongozo wa utoaji wa huduma za ugani unataka kuandaliwa kwa angalau mashamba darasa nane katika msimu mmoja katika ngazi ya kijiji.

Kupitia mahojiano yaliyofanywa na maofisa kutoka Wizara ya Kilimo, TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibainika kwamba idadi ya mashamba darasa yaliyoandaliwa ilikuwa ni chini ya nane kwa msimu hali iliyokwamisha uhamishaji wa wa teknoljia na mbinu bora za kilimo kwenda kwa wakulima. Mashamba darasa ni mbinu inayotumika sana na hivyo ilitegemewa kuwa ni mbinu yenye matokeo zaidi katika uhamishaji wa maarifa kwa wakulima. Sababu za kuandaliwa kwa mashamba darasa machache ni pamoja na kuwa na mipango isiyo na uhalisia ikiwa ni pamoja na kupanga kuandaa mashamba darasa katika maeneno ambayo hayakuwa na maofisa ugani wa kutosha kutoa huduma hiyo na pia matumizi ya fedha zilizotengwa kwa kuandaa mashamba darasa

[11] Hii ni takwimu ya wakulima waliosajiliwa katika mamlaka saba za serikali za mitaa zilizotembelewa pekee.

kinyume na vifungu vya bajeti katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa.

#### 7.2.4 Uchache wa vituo vya huduma za kilimo vya kata

Ilibainishwa kwamba idadi ya vituo vya raslimali kilimo vya kata ilikuwa ni ndogo kuliko idadi ya vituo vilivyopangwa kujengwa. Kulingana na miongozo ya vituo vya raslimali vya kata, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilitakiwa kuandaa angalao kituo kimoja katika kila kata, ili wakulima waweze kuongeza uwezo wa kuweza kupata teknolojia bora, taarifa na ushauri. Kwa mfano, kati ya kata 255 katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa katika mwaka 2012/13 ni kata 11 tu ambazo ni sawa na asilimia 4 ya kata zote ambazo zilikuwa zimeandaa vituo vya raslimali kilimo vya kata vilivyotumiwa na wakulima.

Uchambuzi wa mipango na utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya raslimali kilimo vya kata ulionesha kwamba mamlaka za serikali za mitaa zilipokea kiwango kinachofikia asilimia 95 ya fedha zilizotengwa katika bajeti kwa ujenzi wa vituo vya raslimali kilimo vya kata. Hata hivyo mamlaka ziliweza kujenga asilimia 17 tu ya idadi ya vituo vilivyopangwa kwa kiwango hicho hicho cha fedha. Kulingana na mahojiano yaliyofanywa na maofisa wa Wizara ya Kilimo, TAMISEMI na Sekretarieti za Mikoa ilibainika kwamba kiasi kikubwa cha fedha zilizotengwa kwa ujenzi wa vituo vya raslimali kilimo vya kata zilizoelekezwa na kutumiwa katika matumizi kwa kazi nyinginezo.

### 7.3 Mambo yaliyochangia utoaji hafifu wa huduma za ugani

Kaguzi zilizofanyika katika sekta ya kilimo zilibaini uwepo wa masuala mbalimbali yaliyochangia katika utoaji duni wa huduma za ugani. Masuala hayo ndiyo yaliyoathiri pia utendaji wa maofisa ugani katika maeneo yao ya kazi. Ripoti zilijadili mambo tofauti yanayojirudia katika kufuata miongozo iliyopo kwenye utoaji wa huduma za ugani, mipango hafifu kwa utoaji wa huduma za ugani, utoaji fedha kwa huduma za ugani usionuia matokeo, kujenga uwezo wa maofisa ugani, na usimamizi na ufuatiliaji hafifu wa huduma za ugani. Masuala yaliyobainishwa kuwa sababu za utoaji hafifu wa huduma za ugani yanaelezwa zaidi kama ifuatavyo.

#### 7.3.1 Miongozo isiyotosheleza ya utoaji wa huduma za ugani

Utoaji wa huduma za ugani haukuwa na miongozo toshelevu ya utoaji wa huduma za ugani kwa namna ambayo ingeweza kuhakikisha utoaji sahihi wa huduma za ugani kwa wakulima. Mapungufu yalibainishwa katika miongozo na namna miongozo ilivyokuwa inahuishwa. Sehemu ifuatayo inafafanua zaidi masuala yaliyobainishwa kuhusiana na miongozo ya utoaji wa huduma za ugani.

*i) Maofisa ugani hawakupatiwa miongozo ya utoaji wa huduma za ugani*

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba miongozo ya utoaji huduma za ugani haikukabidhiwa kwa maofisa ugani ili waweze kuitumia. Miongozo hiyo ilitakiwa kugawiwa ili iweze kutumiwa katika mamalaka zote za serikali za mitaa kwa kuwa ilitoa maelekezo kwa maofisa ugani yahusuyo majukumu na wajibu wao pamoja na namna ya kutekeleza majukumu hayo.

Kwa upande mwingine, kaguzi zilizofanyika katika utoaji wa huduma za ugani zilibaini kwamba miongozo ya utoaji wa huduma za ugani imegawiwa kwa wadau wanaojihusisha na utoaji wa huduma za ugani ikijumuisha Jukwaa Huru la Wadau wa Kilimo, *Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania*, TAMISEMI, ONEACRE, na mamlaka za serikali za mitaa. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa iwapo miongozo imezifikia sekretarieti zote za mikoa na mamlaka zake ambazo ni watendaji wakuu katika kuhakikisha miongozo hiyo inatumika katika ngazi za chini.

*ii) Miongozo isiyogusia shughuli za usisimamizi*

Kaguzi zilibaini kwamba miongozo ya utoaji wa huduma za ugani haikuzungumzia shughuli za usimamizi. Kutokana na mapitio ya miongozo, ilibainika kwamba miongozo haikuwa na maelekezo ya maeneno ya kutembelewa, vigezo vya kuchagua maeneo ya kutembelewa, wala vipaumbele vya maeneo ya kutembelewa. Mapitio zaidi ya miongozo yalibaini kwamba hakukuwa na maelekezo ya kiwango cha juu au cha chini cha idadi ya safari zinazoweza kufanywa isipokuwa mfumo wa ufuatiliaji na utathmini wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo wa Mwaka 2008 ambao unakitaka kikosi-kazi kikuu kufanya ziara za usimamizi kwa mamalaka za serikali za mitaa katika kipindi cha kila nusu mwaka.

*iii) Kutofuata maelekezo ya utoaji huduma za ugani*

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba miongozo ya utoaji wa huduma za ugani haikufuatwa na maofisa ugani. Ilibainika kwamba maofisa ugani wengi hawakutekeleza majukumu yao kulingana na maelekezo ya miongozo. Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Kilimo na TAMISEMI hazikutoa taarifa kwa maofisa ugani kuhusu umuhimu wa kutumia miongozo hii. Maofisa ugani hawakuwa na ufahamu wa wajibu na majukumu yao kutokana na kutokuwepo kwa nakala za miongozo katika ngazi ya kata na kijiji. Hivyo, huduma za ugani zilizotolewa hazikufuata taratibu zilizowekwa kwenye miongozo.

### 7.3.2 Jitihada hafifu za kuwajengea uwezo watoaji wa huduma za ugani

Ili kutoa huduma za ugani zilizo bora kwa wakulima, maofisa ugani wanahitaji kupata mafunzo endelevu na ya mara kwa mara, pamoja

na shughuli zingine za kuwajengea uwezo ili kuwapa mbinu mpya katika kutoa huduma za ugani pamoja na kupata taarifa mpya za madodoso ya kufundishia wakulima. Hii itatoa uhakikisho kwamba huduma zinazotolewa ni zenye ubora wa hali ya juu na zinakidhi matarajio ya wakulima. Hata hivyo, utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa ugani uliambatana na mapungufu katika maeneo yafuatayo:

*i) Kutokuwepo mipango ya mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa ugani*

Ukaguzi ulibaini kwamba hapakuwepo na mchanganuo wa mahitaji wala utekelezaji wa programu za mafunzo kwa watoaji wa huduma za ugani au kwa wakulima wenyewe. Hii ilikuwa kinyume na miongozo ya utekelezaji na usimamizi wa utoaji wa huduma za ugani unaotaka mamlaka za serikali za mitaa kutoa mafunzo kwa maofisa ugani kulingana na mahitaji yao. Ukaguzi wa ufuatiliaji uliofanywa baadaye ulibaini kwamba bado hakukuwa na mpango wa mafunzo ya kuwajengea uwezo. Maofisa ugani wamekuwa wakipokea mafunzo machache ya kuwajengea uwezo kwa kutegemea utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo, ambapo mafunzo yalifanyika mara moja tu tokea mwaka 2015.

*ii) Maofisa ugani kutopewa mafunzo kuhusu matumizi ya miongozo*

Utoaji wa huduma za ugani unategemea sana uwepo wa miongozo sahihi ya kusimamia shughuli za maofisa ugani. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba maofisa ugani hawakuwahi kupatiwa mafunzo ya miongozo na hasa mwongozo wa kudhibiti ugonjwa wa mahindi unaofahamika kama "Maize Lethal Necrosis Diseases (MLND)". Mwongozo huu uliandaliwa na Wizara ya Kilimo na ulitakiwa kuwapa mafunzo maofisa ugani waliokuwa na wajibu wa kufikisha elimu na maarifa yatokanayo na taaarifa za ufuatiliaji wa namna ya kukabiliana na ugonjwa wa "MLND". Kwa mfano, maofisa ugani na wakulima wa Vijiji vya Maweni na Makiba katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru hawakuwa na elimu na ujuzi wala maarifa ya namna ya kukabiliana na ugonjwa huo licha kwamba vilikuwa ni kati ya vijiji vilivyoathiriwa kwa kiasi kikubwa na ugonjwa wa MLND.

*iii) Maofisa ugani kutopewa mafunzo ya udhibiti wa viuwatilifu*

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba maofisa ugani hawakupewa mafunzo ya kudhibiti kikamilifu viuwatilifu. Hapakuwepo na nyaraka za mpango wa mafunzo kuongoza utoaji wa mafunzo ya udhibiti wa viuwatilifu yanayotolewa kwa maofisa ugani. Utekelezaji uliokuwa ukifanywa na Wizara ya Kilimo katika upelekaji wa maarifa ya udhibiti wa viuwatilifu haukuwa toshelevu. Wakulima na maofisa ugani hawakupewa mafunzo kwa ukamilifu kuhusu udhibiti wa viuwatilifu. Hii ilipelekea kuwa na matumizi yasiyo sahihi ya

viuwatilifu yaliyaoathiri ubora na kiwango cha mazao yanayozalishwa, afya za binadamu, na mazingira.

### 7.3.3 Kutoratibiwa kwa mipango ya utoaji wa huduma za ugavi

Ukaguzi ulibaini kwamba mipango ya utoaji wa huduma za ugani haikuratibiwa vyema kati ya Wizara ya Kilimo na TAMISEMI na hasa kuhusu uwiano uliopo kati ya raslimali-fedha na raslimali-watu zilizopo ikiendana na utoaji wa raslimali-fedha kwa ajili ya utoaji wa huduma za ugani bila kuwa na mipango sahihi ya utekelezaji wa shughuli hizo. Kukosekana huko kwa uwiano katika mamlaka za serikali za mitaa kulitengeneza uwezekano wa kuwa na fedha zisizo na matumizi zilizoshawishi matumizi nje ya bajeti katika shughuli nyingine.

*i) Kutowiana kwa raslimali-fedha na raslimali-watu zinazotolewa*

Ukaguzi wetu ulibaini kwamba kulikwa na upungufu wa maofisa ugani wanaowahudumia wakulima katika ngazi tofauti. Ukaguzi uliofanyika katika mamlaka saba za serikali za mitaa ulibaini kwamba idadi ya maofisa ugani wa kata iko chini ya kiwango kinachohitajika kulingana na Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997 wakati utoaji wa fedha ulikuwa juu kiuwiano. **Jedwali 7.2** linaonesha ni kwa kiwango cha upungufu wa maofisa ugani ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika kwa kila shamba familia.

**Jedwali 7.2: Uchambuzi wa uwiano kati ya maofisa ugani wa kijiji dhidi ya mashamba familia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotembelewa**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Maofisa Ugani wa Kijiji | Mashamba Familia | Uwiano wa Maofisa Ugani kwa Shamba Familia |
|---|---|---|---|
| 2009/10 | 177 | 418,901 | 1:2367 |
| 2010/11 | 182 | 439,283 | 1:2414 |
| 2011/12 | 268 | 459,213 | 1:1713 |
| 2012/13 | 365 | 475,001 | 1:1301 |

***Chanzo:*** *Takwimu za kilimo za kata kwa kila mwezi kadri ya maofisa ugani wa kata na vijiji*

**Jedwali 7.2** linaonesha kwamba uwiano kati ya maofisa ugani wa kata wanaohudumia mashamba familia ni kubwa ikilinganishwa na kiwango kinachotajwa katika Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997. Sera inataka ofisa ugani wa kata mmoja kuhudumia mashamba familia yasiyozidi 700. Hata hivyo, kulingana na hali ya sasa katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa, imebainika kwamba

ofisa ugani mmoja anahudumia wastani wa mashamba familia 1950 huku baadhi yao wakihudumia hadi mashamba familia 2414.

Kwa upande mwingine, uchambuzi katika **Jedwali 7.2** unaonesha kwamba hali inaimarika kwa sasa kwa kuwa uwiano wa maofisa ugani wa vijiji kwa kila mashamba familia unapungua kuanzia mwaka 2009/10. Hata hivyo, lengo lililowekwa na Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997 halijafikiwa. Uchambuzi zaidi uliofanywa kulinganisha raslimali-watu na raslimali-fedha zilizopo ulionesha kwamba kulikuwa na fedha zisizo na matumizi kati ya fedha zilizotolewa ambazo zingeweza kutumiwa na maofisa ugani. **Jedwali 7.3** linaonesha uwiano kati ya maofisa ugani wa vijiji waliopo dhidi ya fedha zilizotolewa kwa kila kijiji.

**Jedwali 7.3: Tathmini ya idadi ya maofisa ugani wa vijiji waliopo dhidi ya fedha zilizotolewa**

| Mwaka wa Fedha | Uwiano wa Ofisa Ugani wa Kijiji kwa Idadi ya Vijiji | Wastani wa Fedha kwa Kila Kijiji | Vijiji visivyo na Maofisa Ugani | Fedha ambazo Hazikuwa na Matumizi |
|---|---|---|---|---|
| 2009/10 | 1:5 | 855,429 | 4 | 3,421,716 |
| 2010/11 | 1:5 | 596,288 | 4 | 2,385,152 |
| 2011/12 | 1:4 | 725,859 | 3 | 2,177,577 |
| 2012/13 | 1:3 | 725,859 | 2 | 1,451,718 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Kilimo za kila Mwezi (Mamlaka za Serikali za Mitaa)*

**Jedwali 7.3** linaonesha kulikuwa na fedha zisizo na matumizi kwa baadhi ya vijiji kulingana na fedha zilizotolewa kuanzia mwaka wa fedha 2009/10 hadi 2012/13. Kulingana na miongozo ya utoaji wa huduma za ugani, ofisa ugani wa kijiji mmoja anaweza kuhudumia kwa ufanisi kijiji kimoja tu. Hata hivyo, kwa hali iliyopo sasa ofisa ugani wa kijiji mmoja anahudumia wastani wa vijiji vinne.

Kwa upande mwingine, hali iliyopo inaonekana kuimarika kutokana na kuwa uwiano wa fedha ambazo hazina matumizi umekuwa ukipungua kila mwaka kwa kipindi cha miaka kadhaa. Katika mwaka wa fedha 2009/10, fedha zisizo na matumizi zilikuwa ni takribani milioni 3.4 wakati katika kipindi cha mwaka 2012/13 kiwango kilipungua hadi kufikia milioni 1.5. Kupungua kwa kiwango cha fedha zisizo na matumizi kulisababishwa na kupungua kwa fedha zilizotengwa kwa kila kijiji kutoka shilingi 855,429 hadi shilingi 725,859 kwa kila kijiji kwa mwaka 2012/13.

Ilibainika pia kupitia ukaguzi wa ufuatiliaji kwamba zoezi la kuajiri maofisa ugani halijatekelezwa. Ukaguzi wa ufuatiliaji ulibaini pia kwamba TAMISEMI iliomba kibali cha kuajiri kutoka Ofisi ya Raisi -

Menejimenti ya Utumishi wa Umma lakini kibali cha kuajiri hakijapatikana.

### 7.3.4 Usimamizi hafifu wa fedha zitolewazo kwa ajili ya huduma za ugani

Utoaji wa fedha kwa huduma za ugani bado haujafanywa kwa ufanisi ili kurahisisha utendaji katika utoaji wa huduma za ugani. Raslimali-fedha zilizotengwa kwa shughuli za ugani hazikusimamiwa vyema na kulikuwa na ishara za matumizi ya fedha katika malengo ambayo hayakukusudiwa. Udhaifu katika utoaji wa fedha kwa shughuli za ugani yalibainika wakati wa uaandaaji wa bajeti na shughuli za fedha zilifanyika wakati wa utoaji wa huduma za ugani kama inayoelezewa hapa chini.

*i) Kutengwa bajeti chini ya kiwango kwa ajili ya huduma za ugani*

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba mipango ya utoaji wa huduma za ugani ilitengewa fedha chini ya kiwango kwa baadhi ya shughuli kitendo kilichoathiri kiwango cha utekelezaji na utoshelevu wa huduma za ugani zilizotolewa kwa wakulima. Kwa mfano, kuanzia mwaka wa fedha 2009/10 hadi 2012/13 kulitolewa fedha za kutosha kulingana na bajeti ya huduma za ugani ambayo ilijumuisha fedha kwa ajili ya manunuzi ya mafuta kwa ajili ya huduma za ugani. Hata hivyo, iliripotiwa kwamba maofisa ugani walikuwa wakitumia fedha zao wenyewe kununua mafuta na kufanya matengenezo ya vifaa vyao vya usafiri licha ya fedha kwa ajili ya kazi hizo zilitolewa kulingana na bajeti. Kwa upande mwingine, ujenzi wa vituo vya huduma za kilimo vya kata ulifanywa chini ya idadi iliyopangwa kulingana na bajeti licha ya kutolewa fedha zote kulingana na bajeti yake. Utengaji wa bajeti chini ya kiwango ulijitokeza pia kwa fedha zilizopangwa na kutolewa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa kikosi-kazi maalumu. **Jedwali 7.4** linaonesha kiasi cha fedha zilitengwa chini ya bajeti.

**Jedwali 7.4: Bajeti iliyotengwa kwa shughuli za usimamizi Wizarani**

| Mwaka wa Fedha | Fedha Iliyotengwa | Fedha Iliyotolewa | Asilimia ya Fedha Iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 2010/11 | 5.7 | 5.7 | 100 |
| 2011/12 | 5.7 | 5.7 | 100 |
| 2012/13 | 5.2 | 5.2 | 100 |

*Chanzo: Fedha za Mfuko wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa Miaka 2010/11 – 2012/13*

**Jedwali 7.4** linaonesha kwamba shughuli za usimamizi zilitengewa jumla ya shilingi milioni 5.7 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi kwa kila mwaka wa fedha katika kipindi cha kuanzia

mwaka wa fedha 2010/11 hadi 2012/13. Kiwango hicho hakikuweza kuruhusu kikosi-kazi maalumu kufanya shughuli za usimamizi kwa mwaka mzima. Licha ya kupokea fedha kwa asilimia 100 kama ilivyotengwa katika bajeti, shughuli za usimamizi hazikuweza kufanyika kwa kiwango cha kutosha katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kipindi cha nusu mwaka.

Aidha, timu ya ukaguzi ilibaini kwamba fedha kwa ajili ya kujenga uwezo katika sekta ya kilimo katika mamlaka ya serikali za mitaa zilizotembelewa zilipungua kwa zaidi ya asilimia 50 kwa kipindi cha miaka ya fedha 2011/12 na 2012/13, wakati fungu la fedha za huduma ya ugani hazikutolewa katika kipindi hicho. Maofisa kilimo waliohojiwa katika Kitengo cha Uratibu wa Kisekta - TAMISEMI walibainisha kwamba aina hizo mbili za mafungu ya fedha zimekuwa zikitumiwa na mamlaka za serikali za serikali kwa kubadilishana licha kwamba fungu la fedha za ugani lilitumiwa zaidi kwa utoaji wa ujuzi wa kilimo kwa wakulima na fungu la kujenga uwezo katika kilimo lilitumiwa zaidi kwa ajili ya kujenga uwezo wa maofisa ugani kama vile kozi fupifupi na kununua mafuta kwa ajili ya pikipiki. Hii ilipelekea Wizara ya Kilimo kuamua kusitisha kutoa fedha za kujenga uwezo na badala yake kuamua kuunganisha mafungu hayo mawili ya fedha. Mamlaka za serikali za mitaa zilibakiwa na fungu la fedha za kujenga uwezo pekee ambalo lilikuwa ni muunganiko wa mafungu hayo mawili ya fedha.

*ii) Fedha za huduma za ugani kutumiwa kinyume na bajeti*

Ukaguzi ulibaini kwamba fedha iliyopangwa awali kwa ajili ya kutoa huduma za ugani zilitumiwa kwa ajili ya shughuli nyingine ambazo hazihusiani kabisa na huduma za ugani. Kwa mfano, fedha kwa ajili ya kujenga uwezo katika kilimo ambazo zilitakiwa kutumika kugharamia kozi za mafunzo za muda mfupi kwa wakulima na maofisa ugani zilitumiwa kuwagharamia baadhi ya wafanyakazi wa mamlaka za serikali za mitaa kwenda masomoni kwa kozi za muda mrefu kama shahada na shahada za uzamivu badala ya shughuli mahsusi za mfuko huo wa kujenga uwezo. Hii ilithibitishwa na hali ya utekelezaji wa baadhi ya shughuli ambazo zilionesha kiwango cha chini cha utekelezaji licha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kupelekewa fedha zote kadiri ya bajeti kwa shughuli hizo. Jedwali 7.5 inaonesha asilimia ya fedha zilizotolewa dhidi ya kiwango cha utekelezaji wa shughuli husika.

**Jedwali 7.5: Kiwango cha utekelezaji wa huduma za ugani kikilinganishwa na kiwango cha fedha zilizotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa**

| | Ujenzi wa Vituo vya Raslimali Kilimo vya Kata (%) | Ujenzi wa Mashamba Darasa (%) | Mafunzo ya Maofisa ugani (%) | Mafunzo kwa Wakulima (%) |
|---|---|---|---|---|
| Kiwango cha Utoaji Fedha | 95 | 97 | 97 | 97 |
| Kiwango cha Utekelezaji | 17 | 30 | 59 | 1 |

*Chanzo: Mipango kazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*

**Jedwali 7.5** linaonesha kwamba kiwango cha utekelezaji wa shughuli nne kuu katika utoaji wa huduma za ugani kilikuwa kidogo ukilinganisha na kiwango cha fedha zilizotolewa kwa shughuli husika. Kiwango cha chini kabisa kilionekakana katika utekelezaji wa mafunzo kwa wakulima ambapo ni asilimia moja tu ya shughuli zilizopangwa ziliweza kutekelezwa.

### 7.3.5 Ufuatiliaji hafifu wa utoaji huduma za ugani

Ufuatiliaji wa utoaji wa huduma za ugani haukufanywa kwa ukamilifu kukabiliana na changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa hudumza za ugani. Shughuli zinazohusiana na ufuatiliaji hazikutoa taarifa kamili kuhusu utendaji wa viashiria pamoja na maendeleo kuelekea kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa huduma za ugani kama Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na shughuli nyingine za kilimo. Mapungufu yafuatayo yalibainika katika ufuatiliaji wa shughuli za ugani.

*i) Kutokuwepo kwa mipango ya ufuatiliaji na tathmini*

Timu ya ukaguzi ilibaini kwmba Wizara ya Kilimo na TAMISEMI hawakuandaa mpango wa ufuatiliaji kwa shughuli za ugani katika kipindi chote cha ukaguzi. Kuhusu kutoandaliwa kwa mpango wa ufuatiliaji na tathmini, maofisa waliohojiwa kutoka katika kitengo cha maendeleo ya mazao (Sehemu ya Huduma za Ugani) walisema kwamba shughuli za ufauatiliaji na tathmini hapo awali (kabla yam waka 2013/14) zilikuwa zikitekelezwa na Kurugenzi ya Sera na Mipango (Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini). Hii ilitokana na kwamba kitengo hicho ndicho kilikuwa na wajibu wa kufuatilia na kutathmini shughuli za wizara zote na hivyo kilitakiwa kuandaa mpango wa shughuli za ufuatiliaji.

Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ambacho kina jukumu hili kilianza kuandaa mpango wa ufuatiliaji kuanzia mwaka 2013/14. Hata hivyo, hakukuwa na mpango wa ufuatiliaji uliokuwepo kwa kipindi chote kabla na baada yam waka 2103/14. Ilibainika pia kwamba shughuli za ufuatiliaji na tathmini zilikuwa zikifanywa kila

mwaka kulingana na mipango kazi ya mwaka lakini hakukuwa na mpango-kazi mahsusi uliokuwa ukisimamia utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji.

Aidha, kupitia ukaguzi wa ufuatiliaji uliofanywa katika Wizara ya Kilimo ilibainika kwamba Wizara haikuwa na mpango jumuishi wa ufuatiliaji na tahmini. Wizara bado iliendelea kutumia mipango kazi ya mwaka kwa ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa huduma za ugani na hawakuwa na mpango wa muda mrefu wa ufuatiliaji na tathmini kwa uafuatiliaji wa huduma za ugani.

*ii) Uchache wa maeneo yanayofanyiwa ziara za usimamizi*

Kaguzi ilibaini kwamba maeneo yaliyofanyiwa ziara za usimamizi hayakutosheleza na ziara zilifanyika katika mikoa michache tu. Kwa mfano katika kipindi cha mwaka 2009/10 na mwaka 2010/11 TAMISEMI ilifanya ziara za usimamizi kwa mikoa miwili pekee (Lindi na Mtwara) ikijielekeza zaidi katika utekelezaji na utendaji wa miradi nane ya umwagiliaji. Ziara hizo za usimamizi zilifanyika bila kuwa na mipango ya kufanya ziara kwa Wizara ya Kilimo na TAMISEMI. Hapakuwa na vigezo kwa kuchagua maeneo ya kutembelewa au idadi ya maeneo ya kutembelewa. Hali hii ilifanya mikoa inayotembelewa iwe inatokana na hali inayojitokeza kwa wakati huo na hivyo chaguo la mikoa ipi ya kutembelea ilitegemea na utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa kadiri ilivyoonekana katika taarifa zao za utendaji.

Aidha, ilibainika pia kwamba, ziara za usimamizi zilizofanywa na Wizara ya Kilimo kama wizara ya kitaalamu ni mara chache sana zilijikita katika utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima. Kulingana na maofisa kutoka Wizara ya Kilimo, uchache wa maeneo yaliyofanyiwa ziara za usimamizi ulitokana na kutokuwa na bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli hizo husika.

*iii) Kutokuwepo kwa hatua za marekebisho ili kuboresha hali iliyopo*

Kaguzi ilibaini kwamba Wizara ya Kilimo na TAMISEMI ilishindwa kuchukua hatua za marekebisho ili kuboresha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima. Matatizo ya kudumu ya wakulima yanayohitaji utatuzi hayajaweza kutatuliwa. Mapungufu yaliyoko katika mamlaka za serikali za mitaa, na hasa katika vijiji ambayo yanakwamisha ubora wa ripoti na hatimaye mipango ya ujumla ya kisekta hayakuweza kutatuliwa kwa kuwa yalikuwa hayafahamiki kwa mamlaka za serikali za mitaa na hivyo hivyo kwa wizara. Mapitio ya ripoti nne jumuishi za mwaka na ripoti za robo mwaka kutoka katika mamlaka 35 za serikali za mitaa zilizowasilishwa Wizara ya Kilimo pamoja na mahojiano yaliyofanywa na maofisa kilimo na wakulima

yalionesha kuwepo kwa matatizo ya muda mrefu ambayo yamekwamisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima.

Kwa upande mwingine, ukaguzi wa ufuatiliji uliofanywa ulibaini kwamba kulikuwa na kutochukuliwa kwa hatua za kurekebisha hali kutokana na mambo yaliyobainika katika ziara za ufuatiliaji na usimamizi.

### 7.3.6 Matokeo ya utoaji hafifu wa huduma za ugani

Kaguzi zilizofanyika zilifanya tathmini ya matokeo ya utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima na kubaini na kuangalia iwapo kulikuwa na mabadiliko yoyote ya msingi kwa mbinu za kilimo zitumiwazo na wakulima ambazo zingeweza kuonesha maboresho au kufifia kwa ukuaji wa wakulima. Masuala yafuatayo yalibainishwa juu ya utendaji wa wakulima ikihusiana na utoaji wa huduma za ugani.

*i) Matokeo hafifu ya matumizi ya teknolojia za kilimo*

Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba, sehemu kubwa ya wakulima walikuwa bado wakitumia njia za asili katika kilimo chao. Kwa mfano, katika baadhi ya vijiji vilivyotembelewa, kilimo cha kuhamahama kilikuwa kikitumika kama mbinu ya kuhifadhi rutuba ya udongo, badala ya kutumia mbolea. Aidha, wakulima wachache tu ndiyo walikuwa wakitumia mbegu zilizoboreshwa, badala yake walikuwa wakitegemea mbegu walizohifadhi kutokana na mavuno ya msimu uliopita. Mambo haya yote yalitakiwa kutatuliwa na huduma za ugani zilizotolewa kwa wakulima na zilitegemewa kuwashawishi wakulima kutumia mbinu mpya za kisasa katika kilimo.

Matokeo hafifu ya utumizi wa teknolojia yalisababishwa na uandikishaji mdogo wa wakulima katika mashamba darasa na vitalu vya maonyesho na uchache wa ujenzi wa vituo vya raslimali kilimo vya kata ambavyo ni nyenzo kuu za uhamishaji maarifa kwa wakulima. Tathmini ya uandikishaji wa wakulima katika mashamba darasa ulionesha kwamba ni asilimia 1 tu ya wakulima walikuwa wamejiunga katika programu ya mashamba darasa kati ya wakulima wote. Kwa upande mwigine, ujenzi wa vituo vya raslimali kilimo vya kata ulifikia asilimia 17 tu ya vituo vilivyopangwa katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa.

*ii) Kuongezeka kwa mavuno kwa wakulima waliojiunga na mashamba darasa*

Kaguzi ilibaini kwamba kulikuwa na matokeo chanya katika wastani wa mavuno kwa wakulima waliokuwa wakipewa huduma za ugani ukilinganisha na wale ambao walikuwa hawapati huduma hiyo katika Mamlaka 7 za Serikali za Mitaa zilizotembelewa. Hii ilichangiwa na matumizi ya elimu iliyotolewa kuhusu teknolojia za kilimo zilizoboreshwa zilizokuwa zikitolewa kupitia huduma za ugani.

Uchambuzi ukifanyika kw akulinganisha wakulima waliopata usaidizi kupitia huduma za ugani dhidi ya wakulima ambao hawakupata usaidizi wowote. Jedwali 7.5 linaonesha wastani wa mavuno kwa gunia la kilogramu 100 kw akila hekta kw akipindi cha mwaka 2009/10 – 2012/13 kwa mamlaka 7 za serikali za mitaa zilizotembelewa.

**Jedwali 7.6: Mavuno ya wastani kwa gunia la kilogramu 100 kwa hekta kwa kipindi cha mwaka 20019/10 – 2012/13 katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa**

| Zao | Wakulima Wasiojiunga na Mashamba Darasa | Wakulima Waliojiunga na Mashamba Darasa | Ongezeko la Mavuno (mara) |
|---|---|---|---|
| Mahindi | 61 | 161 | 3 |
| Muhogo | 7 | 22 | 3 |
| Mtama | 1 | 13 | 13 |

*Chanzo: Ripoti za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo*

**Jedwali 7.6** linaonesha kwamba wastani wa mavuno kwa kila gunia la kilogramu 100 kwa hekta ulikuwa ni mkubwa kwa wakulima waliokuwa katika programu ya mashamba darasa ikilinganishwa na wale ambao hawakuwa katika programu hiyo katika halmashauri zilizotembelewa. Kwa mazao matatu yaliyochaguliwa, wanachama wa mashamba darasa walikuwa na wastani mkubwa zaidi wa uzalishaji mara 8 zaidi ya wale ambao hawakuwa katika programua ya mashamba darasa.

## SURA YA NANE

## UTOAJI WA HUDUMA SAIDIZI KWA WASINDIKAJI KWA MAZAO YA KILIMO

### 8.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha matokeo ya Ukaguzi wa utoaji wa huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo. Pia sura hii itazungumzia moja kati ya maeneo manne ya kimkakati ya kilimo yanakayofanyiwa ili kuboresha na kuleta ushindani kwenye uthamani wa mmazao ya kilimo nchini.

Matokeo ya Ukaguzi yamegawanyika katika maeneo ya mipango, ukuaji na utoaji huduma saidizi kwenye mafunzo, kifedha, teknolojia na masoko. Matokeo ya Ukaguzi kwenye utoaji wa huduma saidizi kwa wasindikaji kwa mazao ya Kilimo ndiyo yamejumuishwa kwenye kuelezea sura hii.

Wasimamizi wakuu katika utoaji wa huduma saidizi kwa wasindikaji kwa mazao ya Kilimo ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo. Wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati waliojumuishwa kwenye hii kaguzi ni wasindikaji wa mazao ya kilimo.

### 8.2 Utoaji wa huduma saidizi hafifu kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo;

Ukaguzi ulionesha kuwa Wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati hawakupatiwa huduma saidizi kwenye teknolojia, kifedha, masoko na mafunzo ambayo yangewasaidia kuongeza uthamani kwenye mazao ya kilimo kama inavyoelezewa hapa;

#### 8.2.1 Utoaji hafifu wa Huduma saidizi za Mafunzo

Idadi ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati walionufaika na mafunzo ya huduma saidizi yaliyotolewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ni wachache ukilinganisha na jumla ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati wanaotambulika na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji nchini na wote waliosajiliwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 8.1.**

**Jedwali 8.1: Asilimia ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati nchini kama ilivyokadiriwa na Wizara ya Viwanda waliopatiwa Mafunzo na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo**

| Mwaka wa Fedha | Makadirio ya Idadi ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati nchini | Idadi ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati waliopatiwa mafunzo na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | Asilimia ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati waliopatiwa mafunzo na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo |
|---|---|---|---|
| 2013/14 | 3,230,000 | 8,558 | 0.3 |
| 2014/15 | 3,320,000 | 16,490 | 0.5 |
| 2015/16 | 3,500,000 | 19,058 | 0.5 |
| 2016/17 | 3,800,000 | 16,782 | 0.4 |

**Chanzo:** *Wizara ya Viwanda (MITI), Makadirio ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati na Mfumo wa taarifa za kimenejimenti wa* Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo *(2018)*

**Jedwali 8.1** inaonesha kuwa mafunzo yaliyotolewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ikilinganishwa kwa nchi ni madogo. Kwa miaka minne iliyopita SIDO wameweza kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati 60,888 ambayo ni wastani wa 15,222 kwa mwaka. Hiyo inawakilisha asilimia 0.4 ya Makadirio ya Idadi ya wajasiriamali na ambao wana viwanda vidogo na vya kati nchini. Mafunzo yaliyotolewa kwa watu wachache ukilinganisha na idadi ya wahitaji wa mafunzo hayo.

Pia, ilibainika kuwa SIDO waliweza kutoa mafunzo kwa wastani asilimia 9 kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati wanaojulikana na SIDO. Aidha, hii ilichangia kwenye ongezeko la utoaji wa bidhaa zisizo na viwango ambazo zinashindwa ushindani wa soko na kupelekea ukuaji mdogo wa sekta ya viwanda nchini.

Ukaguzi ilibaini kuwa mafunzo yaliyotolewa yalikuwa ni machache kwenye maeneo ya wasindikaji wa mazao ya kilimo na uhandisi wa vyuma wadogo wadogo. Idadi ya wasindikaji wa mazao ya kilimo waliopatiwa mafunzo inawakilisha wastani wa asilimia 1.4 ya idadi ya wasindikaji wa mazao ya kilimo waliosajiliwa na SIDO. Aidha jumla ya wasindikaji wa mazao ya kilimo na uhandisi wa vyuma wadogo wadogo waliopatiwa mafunzo iwakilisha asilimiaa 2 ya idadi ya waliopewa mafunzo na SIDO, na inawakilisha asilimia 0.2 ya idadi ya waliosajiliwa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 8.2**.

**Jedwali 8.2: Asilimia ya wasindikaji wa mazao ya kilimo na uhandisi wa vyuma wadogo waliopatiwa mafunzo**

| Mwaka wa Fedha | wasindikaji wa mazao ya kilimo waliopatiwa mafunzo na SIDO | Asilimia kati ya waliopatiwa mafunzo | Asilimia ya waliopatiwa mafunzo kati ya waliosajiliwa | vyuma wadogo wadogo waliopatiwa mafunzo na SIDO | Asilimia kati ya waliopatiwa mafunzo | Asilimia ya waliopatiwa mafunzo kati ya waliosajiliwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013/14 | 910 | 10 | 1 | 168 | 2 | 0.2 |
| 2014/15 | 2470 | 15 | 2 | 291 | 2 | 0.2 |
| 2015/16 | 2893 | 15 | 1.5 | 206 | 1 | 0.1 |
| 2016/17 | 2799 | 17 | 1.2 | 284 | 2 | 0.1 |


**Chanzo:** *Taarifa za mwaka za utekelezaji na Mfumo wa taarifa za kimenejimenti kutoka SIDO (2018)*

Kwa upande mwingine, taarifa ya Ukaguzi iliangalia maeneo yaliyofanyiwa mafunzo kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo na uhandisi wa vyuma wadogo na iligundulika mafuzno yalitolewa kwa zaidi ya wastani uliopangwa kufikiwa kwa miaka minne iliyopita. Jumla ya aina ya mafunzo 341 yalifanyika wastani wa aina ya mafunzo 85 kwa mwaka, ukilinganisha na wastani wa aina ya mafunzo 16 kwenye uhandisi wa vyuma wadogo yaliyotolewa kwenye Ofisi za SIDO mikoani. Kukosekana kwa fedha za wahisani wa kimaendeleo ambao walisaidia mafunzo ya wasindikaji wa mazao ya kilimo kuliko mafunzo mengine.

### 8.2.2 Utoaji hafifu wa mikopo

Kupitia Mpango-mkakati wa Ushirika wa SIDO kifungu 4.5.1 kinaitaka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuzingatia mahitaji yao ili kuwaongezea uwezo wa kifedha. Lakini ilibainika mikopo iliyotolewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo haikukidhi mipango iliyowekwa. Kiammbatanisho Na.8.1 kinaonesha uwiano kati ya mikopo iliyoombwa na mikopo iliyothibishwaa na mikopo iliyotolewa.

**Kielelezo 8.1: Uwiano kati ya mikopo iliyoombwa na mikopo iliyothibishwaa na mikopo iliyotolewa Kupitia Mfuko wa taifa wa uendelezaji ya Wajasiliamali na Mfuko wa Mkoa wa Fedha za Mzunguko**




**Chanzo:** *Tathmini ya wakaguzi kwenye mikopo kwa kuzingatia mikopo iliyotolewa na taarifa za kimenejimenti kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo 2018*

**Kielelezo 8.1** kinaonesha mikopo iliyotolewa haikutosheleza kufikia mahitaji ya waombaji. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17 mikopo iliyoombwa na iliyothibitishwa ilikuwa ni mikubwa kuliko mikopo iliyotolewa. Hata hivyo, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo halikuweza kutoa mikopo iliyopangwa kutolewa. Idadi kubwa ya waombaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezajia Wajasiliamali ilionekana mwaka 2013/14 ambapo waliotuma maombi walikuwa 13,330, pia waliothibitishwa kupata mikopo walikouwa waombaji 9,872 na mikopo iliyotolewa ilikuwa ni 6,564.

Idadi kubwa ya waliotuma maombi kupitia Mfuko wa Fedha za Mzunguko wa Mkoa ilionekana mwaka 2016/17 ambapo waombaji mikopo walikuwa ni 561 na pia ilionekana pia kutolewa kwa kiasi kikubwa cha mikopo kwa mwaka huo kupitia Mfuko wa Fedha za Mzunguko wa Mkoa. **Kielelezo 8.1** pia kinaonesha uombaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezajia Wajasiliamali ilikuwa ikipungua kila mwaka laakini kwa upande wa RFF ilikuwa ikiongezeka. Uelekeo wa kiujumla unaonesha kuanzia mwaka 2013/14 Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilipokea na kuthibisha utoajo wa mikopo kwa maombi 35,315 lakini ilitoa mikopo kwa waombaji 22,563 sawa na asilimia 63 ya mikopo iliyothibitishwa. Hii inaonesha asilimia 37 ya waombaji hawakupatiwa mikopo ijapokuwa walikidhi vigezo vya kupewa mikopo.

### 8.2.3 Utoaji hafifu wa msaada saidizi wa kiteknolojia

Kupitia Mpango-mkakati kwa kipindi cha kuanzia 2014/15 hadi 2016/17, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilipanga

kutekeleza mikakati yenye lengo la kukuza uwepo wa kusambaza teknolojia na kutoa mafunzo juu ya kuelezea mpango-mkakati wa kiteknoloojia.

Mpango huo ulikwenda sambamba na mpango uliopo wa kuongeza teknolojia kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati kama ilivyoelezewa kwenye Mpango-mkakati wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

Katika ngazi ya usambazaji wa teknolojia mpya utekelezaji wake umekuwa ni mdogo kwa kulinganisha na malengo mahususi ya usambazaji wa teknolojia. Kwa miaka minne iliyopita kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17, idadi ya teknolojia iliyosambazwa ilikuwa ni chini ya lengo la usambazaji wa teknolojia 200 kwa mwaka. Hii inatokana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo liliweza kubaini teknolojia idadi ya 186 kwa mwaka 2015, kubaini teknolojia 178 kwa mwaka 2016 na kubaini teknolojia 197 kwa mwaka 2017.

Pia, kupitia kwa kitengo cha kuendeleza teknolojia na viwanda ilibainika kuwa usambazaji wa teknolojia umekuwa chini ya kiwango kwa miaka miwili mfululizo ambapo Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo liliweza kusambaza teknolojia kiasi cha 106 mwaka 2014/15 na 114 kwa mwaka 2015/16 lakini lengo la mwaka lilikuwa ni kusambaza teknolojia 136 kwa mwaka.

Japokuwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lina vituo saba vya kuendelezea teknolojia nchini vyenye lengo la kufanya ubadilishaji, ukarabati na uzalishaji wa mashine na vipuri. Lakini ilibainika vituo hivyo vinakosa teknolojia inayojiendesha ili kuzalisha mashine zitakazotumiwa na Wasindikaji wa mazao ya Kilimo. Hii huchangia utendaji hafifu kwa viwanda vya wasindikaji wa mazao ya Kilimo zinazozalishwa na vituo vya kuendeleza teknolojia nchini. Na hibyo kupunguza ushindani kwa wasindikaji wa mazao ya Kilimo kwenye soko la ndani na la kimataifa ambapo teknolojia inaongezeka.

Usambazaji hafifu wa teknolojia za kisasa husababisha wasindikaji wa mazao ya kilimo kuendelea kuwa nyuma ya teknolojia na kushindwa kuongeza thamani kwenye uzalishaji kama ilivyotakiwa kwenye mpango-mkakati.

### 8.2.4 Utoaji hafifu wa msaada saidizi kwa masoko

Hakukuwa na msaada saidizi kwenye kutafuta masoko ya Wasindikaji wa mazao ya Kilimo. Hakukuwa na mipango mkakati kuhusu masoko utakaohakikisha wasindikaji wanapata masoko ya bidhaa zinazo zalishwa. Msaada wa kimasoko hufanywa Kupitia maonesho ambapo ni wasindikaji wachache hupatiwa nafasi ya ushiriki kwenye

maonesho hayo kwa sababu wengine hushindwa kulipia gharama za kuhudhuria maonesho.

Msaada wa kimasoko unaotolewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo huwasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kutumia masoko yao ya asili ya mnada ambapo ni tofauti na ambao wanahimiza dunia kujikita kwenye soko la mtandaoni.

### 8.2.5 Kukosekana kwa Miundombinu mizuri ya viwanda

Sera ya Maendeleo ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ya Mwaka 2003 inailitaka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Wizara ya Viwanda na Biashara kushirikiana na sekta binafsi, halmashauri, na wadau wa kimaendeleo kuboresha miundombinu na kutoa huduma kwenye maeneo ambayo Wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati wanafanya kazi.

Hata hivyo, kupitia ripoti ya utekelezaji wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na mahojiano yaliyofanya kwa wafanyakazi wake ilibainika kuwa haukukuwa na ushirika kati ya Wizara ya Viwanda auShirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kushrikisha sekta binafsi katika kuleta maendeleo ya kuboresha miundombinu inayohitajika kwa ajili ya maendeleao ya ujasiriamali kama ilivyoelekezwa kwenye sera.

Kaguzi ilibaini pia hakukuwa na ushirikiano na wadau wote kwenye eneo la uendelezaji viwanda vinavyohitajika kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo. Maendeleo mengi yaliyofanyika ilishirikisha Halmashauri zilizopo nchini ambao ndiyo wamiliki wa maeneo na ambapo viwanda vinavyohitajika hujengwa au kuendelezwa.

## 8.3 Sababu zinazochangia utoaji hafifu wa huduma saidizi kwa Wasindikaji wa mazao ya kilimo

Zifuatazo ndiyo sababu zinazochangia utoaji hafifu wa huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo.

### 8.3.1 Kukosekana kwa Mipango ya utoaji huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo


Ukaguzi ulitathmini aina mbalimbali ya mipango kwenye mfumo na mchakato wa utoaji wa huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo kwa Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ili kujua iwapo mipango ilikuwa imepangwa ili kukidhi mahitaji ya wasindikaji wa mazao ya kilimo. Ilioneka kuwa kulikuwa na mapungufu wakati wa kupanga mipango juu ya utoaji huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

**(a) Kutopewa kipaumbele kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wakati wa kupanga bajeti**

Kupitia Mpango-mkakati wa matumizi wa Wizara ya Viwanda na SIDO kwa kipindi kuanzia 2013/14 hadi 2016/17 ilionesha kukosekana kwa Mipango ya utoaji huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo inayojumuisha wajasiriamali wadogo na wa kati.

Ilionekana pia kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati ilipungua katika kipindi cha miaka miwili mwaka 2015/16 na 2016/17 kwa kababu hakukuwa na kiasi kilichotengwa na kitengo cha wajasiriamali wadogo na wa kati kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati. Ilionekana kuwa katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Wizara ya Viwanda ilitumia wastani wa asilimia 16 kwa ajili ya maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati. Hii ilisababishwa na kukosekana kwa fedha ambapo ilipangiwa Wizara ya Viwanda ambapo walipokea kiasi cha asilimia 56 katika fedha iliyotengwa kwa matumizi na Wizara kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 8.2**.


**Kielelezo 8.2: Uwiano kati ya Kiasi kilichotengwa na kiasi Kilichotolewa na kwa ajili ya maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati Wizara ya Viwanda**




**Chanzo:** *Tathmini ya wakaguzi mwaka 2018*

Kaguzi ilibaini pia kuwa uwiano kati ya fedha za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na iliyotengwa kwa matumizi na kiasi Kilichopokelewa na Wizara ya Viwanda, kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho 8.3.

**Kielelezo 8.3: Uwiano kati ya kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17**




**Chanzo:** *Tathmini ya Wakaguzi ya mwaka 2018*

**Kielelezo 8.3** kinaonesha uwiano kiasi cha fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati ni ndogo ukilinganisha na kiasi kilichotolewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo. Katika miaka minne iliyopita, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilipokea kiasi cha Tsh Billioni 55 ili kutekeleza majukumu yake sawa na Tsh Billioni 14 kwa mwaka. Lakini, Wizara ya Viwanda ilitoa asilimia 30 tu ya fedha ya maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati na asilimia 70 ilionekana ni kwa ajili ya matumizi ya kila siku inayojumuisha stahiki za wafanyakazi. Kwa uelekeo huu inaonesha, kuna kutopewa kipaumbele kwa shughuli za kimaendeleo za wajasiriamali wadogo na wa kati kwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

**(b) Kutoshirikishwa kwa wadau kwenye mchakato wa kuandaa bajeti**


Ilibainika kuwa ushirikishwaji kwa wadau wakati wa kuandaa mipango ya utoaji wa huduma saidizi kwa wasindikaji kwa mazao ya kilimo. Kaguzi ilibaini kuwa, kwenye ngazi ya makao makuu ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na ofisi zake za mikoa kumekosekana ushirikishwaji kwa wadau, ushirikishwaji mkubwa ilionekana wakati wa utekelezaji wa huduma saidizi.

### 8.3.2 Utekelezaji wa huduma saidizi haukuzingatia Mipango iliyowekwa

Kupitia kwa Taarifa za utekelezaji za mwaka kutoka Wizara ya Viwanda na makao makuu ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, ilionesha Utekelezaji wa huduma saidizi haukuzingatia Mipango iliyowekwa. Ilibainika kulikuwa na mafanikio madogo kwa kulinganisha na malengo iliyowekwa katikaa kusaidia maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati inayowajumuisha wasindikaji kwa mazao ya kilimo.

Mpango mkaka wa kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2015/16 ulilenga mipango 12 ambayo ilitakiwa kufikiwa na Wizara ya Viwanda kama njia ya kuwaendeleza wajasiriamali wadogo na wa kati. Hata hivyo, ilibainika kutofikiwa kwa malengo yote waliyojiwekea hadi wakati mpaango mkakati unamalizika mwezi Juni 2016. Tathmini ya matokeo ya hali ya utekelezaji wa malengo kwa Wizara ya Viwanda imewasilishwa kwenye **Kielelezo 8.4**.

**Kielelezo 8.4: Maafanikio ya Wizara ya Viwanda katika utekelezaji wa malengo ya kuwaendeleza wajasiriamali wadogo na wa kati**




**Chanzo:** *Tathmini ya Mpango-mkakati wa Wizara ya Viwanda (MITI) 2011/12 hadi 2015/16*

**Kielelezo 8.4** kinaonesha asilimia kubwa ya malengo ya kuwaendeleza wajasiriamali wadogo na wa kati yaliyowekwaa na Wizara ya Viwanda hayakufanikiwa hadi kufikia Juni 2016. Malengo 9 kati ya 12 hayakufikiwa kabisa na malengo 2 kati ya 12 yalifanikiwa kwa kiasi. Lengo moja kati ya 12 ndiyo lilifanikiwa katika hali ya kuridhisha. Tathmini pia ilionesha Wizara ya Viwanda ilipanga kumalizia utekelezaji wa malengo menggine manne kati ya 12 hadi kufikia mwaka 2018 nikiwa ni miezi 20 zaidi baada ya kumalizika kwa Mpango-mkakati.

Kutofanikiwa kufikia Malengo inaoneshaa pia uwepo mafanikio madogo kwenye Sera ya wajasiriamali wadogo na wa kati ya mwaka

2003 kwa sababu malengo yaliyowekwa yalitokana na malengo ya sera ambayo yalitakiwa kuainishwa na Wizara ya Viwanda kutoka kwenye Mpango-mkakati.

### 8.3.3 Kutofanyika kwa tathmini ya mahitaji

Mpango-mkakati wa mwaka 2014/15 hadi 2016/17, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilitakiwa kufanya huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuzingatia mahitaji yao. Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilitakiwa kuwa na mfumo wa kuchukua mahitaji kutoka kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ili kuhakikisha ushirikishwaji wa mahitaji yote ya wajasiriamali.

Kupitia mahojiano na wafanyakazi kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo makao makuu na wa mkoani na kupiitia taarifa za mmahitaji kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17, ilionesha mfumo hafifu wa kufanya tathmmini ya mahitaji ya wajasiriamali wadogo na wa kati kwasababu ulikuwa na mapungufu mengi.

Pia, kupitia taarifa za utekelezaji za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kwa kipindi cha kuanzia 2013/14 hadi 2016/17 ilionesha kuwa tathmini ya malengo yalishindwa kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Mpango-mkakati. Kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo wameweza kufanya mahitaji 1779 ambacho ni chini ya lengo la 2150 kama mipango Mkakati wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo wa mwaka 2014/15 hadi 2016/17. Hiyo inaonesha utofauti wa asilimia 17 ya malengo yaliyopangwa ya kutathmmini mahitaji.

### 8.3.4 Uratibu hafifu utoaji wa huduma saidizi

Kifungu namba 5(i) cha Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo inatakiwa kusaidia au kuratibu shughuli za taasisi nyingine zinazotoa huduma ya mafunzo kwa watu waliojiajiri auwanaotaka kujiajiri kwenye viwanda vidogo. Lakini kwa kupitia mahojiano na wafanyakazi wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Wizara ya Viwanda ilionekana kwamba kuna uratibu hafifu kwa wadau mbalimbali waliopo kwenye sekta husika.

Kwenye huduma saidizi zinazofanya na wadau wengine wakati wa utekelezaji kumekuwa na ushirikishwaji mdogo wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo. Kwenye badhi ya mikoa watoaji huduma wamekuwa kama washindani baada ya kuwa kama wanaofanya jambo moja katika kutoa huduma. Wadau wengine kama vile halmashauri hawaku washirikisha Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, wakati wanatoa huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo

### 8.4 Ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati

Utoaji wa huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati inatakiwa ufuatiliaji wa karibu kutoka ngazi ya Wizara ya Viwanda na ndani ya SIDO. Ufuatiliaji una lengo la kuhakikisha utoaji bora wa huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kama ilivyo kwenye Sera na Mpango-mkakati.

#### 8.4.1 Ufuatiliaji hafifu wa shughuli za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo zinazotakiwa kufanywa na Wizara ya Viwanda

Wizara ya Viwanda inatakiwa kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ili kuhakikisha kufikia Malengo na viashiria vilivyowekwa kwenye maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati. Lakini ilibainika kwamba Wizara ya Viwanda imeweza kufanya ufuatiliaji kwenye shughuli za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kwa asilimia 50. Kielelezo 8.3 kinaonesha kiasi cha Ufuatiliaji uliofanywa na Wizara ya Viwanda kwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17.

**Jedwali 8.3: Asilimia ya ufuatiliaji uliopangwa kufanyika na uliofanyika na Wizara ya Viwanda kwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo**

| Mwaka wa Fedha | Ufuatiliaji uliopangwa kufanyika | Ufuatiliaji uliofanyika | Asilimia ya Ufuatiliaji uliofanyika (%) |
|---|---|---|---|
| 2013/14 | 4 | 2 | 50 |
| 2014/15 | 4 | 2 | 50 |
| 2015/16 | 4 | 2 | 50 |
| 2016/17 | 4 | 2 | 50 |

**Chanzo:** *Taarifa za Ufuatiliaji na utathmini kutoka Wizara ya Viwanda (2018)*

Kupitia mahojiano na wafanyakazi kutoka Wizara ya Viwanda ilibainika kwamba, ufuatiliaji wa mara mbili kwa mwaka hufanyika kwenye utekelezaji wa programu ya Muunganiko wa Ujasiriamali Vijijini na sio mahususi kuangalia shughuli za SIDO.

#### 8.4.2 Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kufanya tathmini hafifu kuhusu shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati

Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo linatakiwa kuwa na mfumo wa kuangalia uelekeo na kufanya tathmini kwenye shughuli zake wakati wa utoaji wa huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa

kati. Kupitia kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo linatakiwa kuratibu Mipango, Kufuatilia utekelezaji na kufanya tathmini kwenye shughuli zao za kila siku. Lakini ilibainika Ufuatiliaji unaofanywa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lina mapungufu yafuatayo:

a) **Mfumo hafiffu wa kutuma taarifa kuhusu wajasiriamali wadogo na wa** kati


Ukaguzi ulibaini mfumo wa kutuma ripoti za tathmini haufanyi kazi vizuri kwasababu hauwezi wa kuthibitisha taarifa zilizo kwenye ripoti. Mfumo unaruhusu kutuma taarifa zinazojumuisha namba ya viashiria vilivyopo kwenye malengo katika ngazi ya juu Zaidi ya kiutendaji, lakini taarifa za kitathmini kwa maneno huwa hazijumuishwi kwenye ripoti na ngazi ya juu ya kiutendaji.

Pia, ilibainika kwamba mfumo wa kutuma taaarifa uliwazuia wasimamizi na uongozi wa ngazi juu kujua changamoto wanazokutana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kusaidia wajasiriamali wadogo na wa kati.

**b) Tathmini hafifu baada ya utoaji huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.**

Ili kuhakikisha utoaji mzuri wa huduma zake, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo linatakiwa kutoa mwongozo na kufanya tathmini kwenye utekelezaji wake kwenye utendaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Kupitia mahojiano na wajasiriamali wadogo na wa kati ilibainika kumekuwa na ufanyaji hafifu wa tathmmini wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo baada ya kutoa huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. **Kielelezo 8.5** kilionesha tathmini zilizofanywa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kwenye maeneo yote ya wajasiriamali wadogo na wa kati ukijumuisha wasindikaji wa mazao ya kilimo wanaopata huduma saidizi kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

**Kielelezo 8.5: Idadi ya tathmmini zilizofanywa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.**



Majibu kutoka kwa Wasindkaji wa mazao ya kilimo zilionesha kuwa wasindikaji wachache ndiyo walifanyiwa au kutofanyiwa tathmini na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo. Kati ya wasindikaji 36 kutoka halmashauri 6 walionesha kuwa wajasiriamali wadogo na wa kati 7 ambao ni sawa na asilimia 19 hawakuwahi kutembelewa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini; 23 sawa na asilimia 64 wamekuwa waliotembelewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo mara chache. Wakati wajasiriamali wadogo na wa kati 6 kati ya 36 sawa na asilimia 17 wamekuwa waliotembelewa mara kwa mara na kufanyiwa tathmini na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

### 8.4.3 Kutofuata Mpango wa kufanya Tathmini

Ukaguzi ulipitia taarifa za utendaji za Wizara ya Viwanda ili kuangalia kama tathmini inaafanyika kwa kufuata mipango ya tathmini iliyowekwa kama ilivyoelezewa kwenye Mpango-mkakati wa Wizara ya Viwanda wa kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2015/16.

Ilibainika Wizara ya Viwanda haifanyi tathmini kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kama ilivyoelezewa kwenye Mpango-mkakati. Lakini ilionekana Wizara ya Viwanda ikifanya mapitio ya sera na programu mbalimbali. Wizara ilitakiwa kufanya tathmini mara 3 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kuangalia kupanda daraja la ujasiriamali na tathmini inayojumuisha wajasiriamali kuanzia mwaka 2013/14 lakini hakukuwa na utekelezaji. Aidha tathmini ya karibuni iliyofanywa iliangalia madhara ya uanzishwaji wa viwanda vya wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye sekta maalumu ya kiuchumi pia kuangalia uwezeshwaji wa ambao haukufanyika kuanzia mwaka 2016/17.

### 8.4.4 Sababu zinazosababisha kutofanyika kwa Ufuatiliaji na tathmini kwa wajasiriamali wadogo na wa kati

Mahojiano na wafanyakazi kutoka Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na pia kupitia Mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini wa Wizara ya Viwanda, Mpango-kazi na Taarifa za Mipango ya kibiashara kutoka Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ilionesha kuwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo haikuwa Mipango ya kufanya ufuatiliaji kwenye wakati wa utekelezaji wa huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Kwa Mfano, Kupitia kupitia Mpango-mkakati wa ushirika, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilipanga kutoa jumla ya ripoti 360 za ufuatiliaji hadi kufikia Juni 2017. Lakini hakukuwa na ripoti ya Ufuatiliaji iliyotolewa hadi wakati Ukaguzi unafanyika.

Pia, kupitia Mpango-mkakati wa ushirika, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo haikuonesha nani anatakiwa kufanya ufuatiliaji au kuonesha taarifa za ufuatiliaji. Mpango-mkakati wa ushirika ni mwongozo katika Mipango lakini haukuonesha njia ya kufanya

ufuatiliaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati au Ufuatiliaji kwenye Ofisi zake za mkoani au mbinu za kufanya ufuatiliaji.

Ilibainika pia, jukumu la ufuatiliaji ndani ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo linatakiwa kufanywa na kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, lakini ripoti za kitengo cha Ukaguzi wa Ndani zilionesha mambo ya fedha bila kuonesha taarifa za Ufuatiliaji kwenye maeneo waliotembelea.

### 8.4.5 Athari za kufanya ufuatiliaji hafifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati

Baadhi ya madhara yalioonekana kutokana na uwepo wa ufuatiliaji hafifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ni pamoja na;

**i. Kukosekana kwa taarifa za kuhusu utendaji kwa Wasindikaji wa mazao ya kilimo**

Kwa sasa, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo haina mfumo rasmi wa utunzaji taarifa za kuhusu utekelezaji wa wasindikaji wa mazao ya kilimo. Kuna utafiti wa Msingi uliofanyika mwaka 2012 kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, na ndiyo yenye takwimu za wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Pia, ilibainika kuwepo kwa mfumo usioeleweka wa kukusanya taarifa kuhusu utendaji wa wasindikaji wa mazao ya kilimo. Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo halikuwa na uwezo wa utekelezaji wa wasindikaji wa mazao ya kilimo kuhusu huduma saidizi zinazotolewa. Kwa Mfano, Ofisi 2 kati ya 6 za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo za mkoa zilizotembelewa haziokuonesha wafanyabiashara waliopanda daraja la kibiashara.

Mikoa yote iliyotembelewa wakati wa ukaguzi hawakuweza kuonesha mchango wa idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye uchumi na ajira.

**ii. Baadhi ya huduma saidizi kutofanyika vizuri**

Ili kutathmini mafanikio yaliyopo kwenye Mpango-mkakati na katika kutoa huduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo linatakiwa kuandaa Mfumo wa kupima mafanikio utakasaidia kupata taswira nzima wa hali ya utekelezaji wa maeneo yote maanne ya utoaji wahuduma saidizi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Kupitia Mpango-mkakati ilionesha ilikuwa ningumu kwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kukadiria maeneo waliyoyatekeleza kuhusianana huduma saidizi zilizotolewa kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo na aina zote za wajasiriamali wadogo na wa kati. Hii ni kwa sababu viashiria vya kiutendaji kwenye maeneo manne ya huduma

saidizi kama kifedha, teknolojia, masoko, na mafunzo hayakujumuishwa kwa ujumla wake ili kutoa kiashiria kimoja cha utekelezaji kitakachotoa taarifa mafanikio ya utekelezaji wa kwenye ngazi zote zilizotarajiwa.

Timu ya ukaguzi iliyapanga na kutathmini mafanikio ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo kwa kuzingatia maeneo tajwa manne ya huduma saidizi yanayotolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kama inavyyonekana Zaidi kwenye **Jedwali 8.3**.

**Jedwali 8.4: Hali ya Mafanikio kwa Huduma Saidizi kwa Wasindikaji wa mazao ya kilimo na wahandisi wadogo wa vyuma**

| Aina ya Huduma Saidizi iliyohitajika | Hali ya utoaji wa huduma saidizi (kwa asilimia) | |
|---|---|---|
| | Wasindikaji wa mazao ya kilimo | wahandisi wadogo wa vyuma |
| Huduma Saidizi za Kifedha | 20 | 20 |
| Huduma Saidizi za Kiteknolojia | 40 | 60 |
| Huduma Saidizi za Kimafunzo | 70 | 30 |
| Huduma Saidizi za Kimasoko | 40 | 40 |

**Chanzo:** *Taarifa za utekelezaji za SIDO (2018)*

**Jedwali 8.4** linaonesha utoaji wa huduma saidizi za kifedha na masoko kwa Wasindikaji wa mazao za kilimo na wahandisi wadogo wa vyuma ni chini ya asilimia 50%. Hali ni mbaya kwenye huduma saidizi za kifedha ambapo ni chini ya asilimia 20 kwa wote wasindikaji wa mazao za kilimo na wahandisi wadogo wa vyuma.

Kwa upande mwingine, huduma saidizi za mafunzo zilizotekelezwa kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo ni asilimia 40 zaidi ya huduma saidizikwa wahandisi wadogo wa vyuma ambao walipata asilimia 30. Sambamba na hilo, wahandisi wadogo wa vyuma walipatiwa hudumasaidizi ya kiteknolojiakwa asilimia 60 wakati wasindikaji wa mazao ya kilimowalipatiwa.

## 8.5 Madhara ya Utoaji Hafifu wa Huduma Saidizi kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati

Kupitia tafiti zilizofanyika kuangalia maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati nchini na mahojiano yaliyofanywa wafanyakazi wanaotoa huduma saidizi ilibainika kulikuwa na kukua kwa kiasi kidogo kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo na wajasiriamali wadogo na wa kati wengine kama inavyoonyweshwa kwenye maelezo yafuatayo;

### 8.5.1 Kutochangia ongezeko la ajira

Mahojiano na wafanyakazi kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Wizara ya Viwanda na Biashara, pia kupitia tafiti zilizofanywa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati yalionesha kuwa wasindikaji wa mazao ya kilimo hawachangii kwa kikubwa kwenye ukuaji wa ajira kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 8.5.

**Jedwali 8.5: Mchango wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye ngazi ya ajira nchini kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17**

| Maelezo | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|
| Malengo ya Wizara ya Viwanda kwenye kuongeza ajira nchini kupitia wajasiriamali wadogo na wa kati (%) | 50 | 55 | 60 | (-)[12]* |
| Ajira zilizotokana na wajasiriamali wadogo na wa kati (%) | 23.4 | *Hakuna takwimu* | *Hakuna takwimu* | *Hakuna takwimu* |
| Actual level of contribution as per other sources (reviewed researches) (%) | *Hakuna takwimu* | 20[13] | *Hakuna takwimu* | 40[14] |

**Chanzo:** *Mpango-mkakati Wizara ya Viwanda ya mwaka 2012/13 hadi mwaka 2015/16, Takwimu za ajira nchini kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu 2014 na Taasisi ya utafiti uchumi na masuala ya jamii mwaka 2016*

**Jedwali 8.5** linaonesha mchango wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye ongezeko la ajira imekuwa ni ndogo kuliko malengo yaliyowekwa na Wizara ya Viwanda kwa mwaka 2014/15 hadi 2016/17. Wizara ilipangwa kufikia malengo ya asilimia 60 na 65 ya ajira kwa mwaka 2014/15 na 2016/17, lakini taarifa kutoka tafiti zilionesha mchango kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ulikuwa ni chini ya malengo kwa kuchangia asilimia 20 kwa mwaka 2014/15 na asilimia 40 kwa mwaka 2016/17.

### 8.5.2 Mchango Mdogo Kwenye Uchumi

Kwa mujibu wa ukaguzi, sekta ya wajasiriamali wadogo na wa kati ilitegemewa kuwa miongoni mwa sekta ambazo zina mchango kwenye uchumi wa Taifa. Hata hivyo, ilibainika kuwa, kwa mujibu wa mwenendo wa takwimu za sasa, uchangiaji wa sekta hii katika uchumi sio wa kuridhisha. Timu ya Ukaguzi iliweza kubainisha

[12] Viashiria vilibadilika na kuangalia ongezeko kwa wanaume na wanawake

[13] Takwimu za ajira nchini kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda 2014

[14] Taasisi ya utafiti uchumi na masuala ya jamii mwaka 2016 Ushiriki wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye soko la Kimataifa

mwenendo wa ufanisi wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kulinganisha mchango wao kwenye uchumi kwa kutumia pato la taifa kwa muda wa kipindi cha miaka 4 kuanzia 2013/14 hadi 2016/17 kama inavyoonekana kwenye Jedwali 8.6.

**Jedwali 8.6: Mchango wa Wajasiriamali Wadogo na wa kati kwenye Pato la Taifa**

| Maelezo | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|
| Kadirio la Wizara ya Viwanda kuhusu mchango wa Wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye Pato la Taifa (%) | 36 | 38 | 40 | *Hakuna twakimu* |
| Uhalisia wa Ufanisi kwa mujibu na taarifa za Wizara (%) | 27 | *Hakuna twakimu* | *Hakuna twakimu* | *Hakuna twakimu* |
| *Uhalisia wa Ufanisi kwa mujibu wa vyanzo vingine (%) | *Hakuna twakimu* | *Hakuna twakimu* | *35* | *Hakuna twakimu* |

***Chanzo:*** *Mpango-mkakati wa Wizara ya Viwanda 2012/13- 2015/16, ILFS 2014 toka NBS & Ripoti ya Uhuishi toka ESRF 2016 (2018)*

**Jedwali 8.7** linaonesha kuwa mchango wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye pato la Taifa limekuwa chini ya makadirio ya Wizara. Licha ya kuwa Wizara ilijiwekea mkakati wa kuwa na ukuaji unaoongezeka kwenye kiwango cha mchango wa wajasiriamali kwenye pato la Taifa kwa mwaka 2014/15 hadi kipindi cha Ukaguzi hadi sasa, lakini wizara haikuweza kuonesha kama wameweza kufikia hilo lengo.

Takwimu zilizopatikana kutoka vyanzo vingine vya taarifa kama vile Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Masuala ya Jamii (ESRF) ya mwaka 2016, ilibainisha kuwa mchango wa pato la Taifa kutoka sekta ya wajasiriamali wadogo na wa kati kwa mwaka 2015/16 ilikuwa asilimia 35 ambayo ilikuwa ni chini ya kadirio la asilimia 40 ambalo liliwekwa na Wizara.


### 8.5.3 Kiwango cha juu cha anguko kuliko kiwango cha ukuaji

Shabaha kuu ya Sera ya Maendeleo ya Wajariliamali Wadogo na wa Kati ni kuwa na sekta mahiri ya wajariamali wadogo na wa kati, ambayo itahakikisha matumizi bora ya raslimali ili kuweza kufikia ukuaji wa kasi na endelevu. Kwa mujibu wa shabaha hii, Wizara ya Viwanda na Biashara na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo lilitakiwa kutengeneza mazingira mazuri yatakayowawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kuwa na ukuaji endelevu na kuhakikisha kuna matumizi bora ya raslimali nchini.

Kadhalika, uchambuzi wa takwimu za ukuaji na anguko la wajasiriamali wadogo na wa kati za Wizara ya Kilimo na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ulionesha kuwa, sekta hii haina ukuaji endelevu. Uchambuzi ulibainisha kuwa kiwango cha anguko kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ni cha juu kuliko kiwango cha ukuaji wao.

Ilibainika kuwa licha ya kuwa kumekuwa na ongezeko la kiwango cha ukuaji, kiwango cha anguko kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wakiwemo wasindikaji wa mazao ya kilimo ni cha juu. Takwimu zilizopatikana kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo zilionesha kuwa kiwango cha anguko kilikuwa cha juu kuliko kiwango cha ukuaji kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 8.6.**

**Kielelezo 8.6: Viwango vya anguko ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa sekta ya wajasiriamali wadogo na wa kati nchini**





Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, wastani wa kiwango cha anguko kwa miaka minne iliyopita ni kati ya asilimia 8 na 30 mtawalia. Kiwango cha ukuaji kilibainika kuwa asilimia 5.6; na takwimu za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo zilionesha kiwango cha juu cha anguko la wajasiriamali wadogo na wa kati. Hii inamaanisha kuwa wajasiriamali wadogo na wa kati waliosajiliwa pamoja na

wasindikaji wa mazao ya kilimo waliopo chini ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, wamekuwa wakiporomoka kiwango kwa asilimia 30 mara zote kuanzia mwaka 2013/14 hadi 201617.

### 8.5.4 Kiwango kisichoridhisha cha kupanda kwa daraja

Sera ya Maendeleo ya Wajariliamali Wadogo na wa Kati ya Mwaka 2003 inaitaka Wizara ya Viwanda kuweka mazingira wezeshi ili kuwezesha viwanda vya uzalishaji kupanda toka daraja moja la kiutendaji kwenda daraja la juu kabisa. Kwa mujibu wa Mpango-mkakati wa Wizara ya Kilimo (2012/13 -2016/17), twakimu zilizopatikana toka Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo zimeonesha kuwa wastani wa kiwango cha kupanda daraja kwa mwaka kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kilikuwa chini ya kusudio liliowekwa la asilimia 8. **Kielelezo 8.6** kinaonesha kiwango cha upandaji wa daraja kwa muda wa kipindi cha miaka mitatu.

**Kielelezo 8.7: Asilimia ya kiwango cha kupanda daraja kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kipindi cha miaka minne (2013/14 – 2016/17)**




Ukaguzi ulibaini kuwa kiwango cha ukuaji kwa aina zote za wajasiriamali wadogo na wa kati kiliathiriwa na utoaji dhaifu wa huduma saidizi toka Wizara ya Viwanda na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo. Maeneo yaliyobainika kusababisha udhaifu huu yalihusu uandaaji wa mipango, utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

# SURA YA TISA

# HITIMISHO

## 9.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mahitimisho kutokana na uchambuzi wa ripoti sita za ukaguzi wa ufanisi, na ripoti moja ya ufuatiliaji zilizojadiliwa katika ripoti hii ya jumla.

## 9.2 Hitimisho la Jumla

Kwa ujumla, ukaguzi ulitambua jitihada za Serikali kuhusu maendeleo ya kilimo nchini. Hata hivyo, mambo yaliyoonekana kwenye ripoti ya ukaguzi yamenifanya nihitimishe kwamba Serikali haijatekeleza ipasavyo mikakati mbalimbali iliyolenga kuifanya sekta ya kilimo kuwa na tija, endelevu, na uti wa mgongo wa uchumi wa nchi.

Mikakati mikuu iliyotambuliwa na Wizara ya Kilimo kama nguzo za maendeleo ya kilimo hazina utoshelevu wa usimamizi wa Wizara pamoja na wadau wengine. Udhaifu ulioonekana ulikua kwenye usimamizi wa pembejeo za kilimo; ubora wa udhibiti wa pembejeo za kilimo; visumbufu vya mazao na milipuko ya magonjwa; ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; uwepo wa hudumaa za ugani kwa wakulima; na utoaji wa huduma za usaidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo.

Mapungufu yaliyoonekana yalisababishwa na udhaifu wa mifumo ya kuhakikisha mipango, utekelezaji, usimamizi, na tathmini za mikakati iliyotekelezwa na serikali kwa lengo la kusaidia maendeleo ya sekta ya kilimo.

## 9.3 Hitimisho Maalumu

Uchambuzi wa ripoti sita za ukaguzi wa ufanisi, na ripoti moja ya ufuatiliaji zilizojadiliwa katika ripoti hii ya jumla unanipa nafasi ya kutoa mapendekezo maalumu sita kama ifuatavyo.

### 9.3.1 Usimamizi usiojitosheleza wa pembejeo za kilimo nchini

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuatilifu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu hazikuwa zimeweka mpango wa mahitaji ya pembejeo ya kilimo nchini. Mahitaji yaliyokuwa yamepangwa hayakuwa na uhalisia, kwani hapakuwa na utafiti uliokuwa umefanywa ili kujua idadi halisi ya pembejeo zilizohitajika kwa kuzingatia kanda za kiikolojia za kilimo. Nilibaini kuwa hakukuwa na njia nzuri ya kukadiria mahitaji ya pembejeo za kilimo. Hii ni kwa sababu hakukuwa na mfumo au njia sahihi na rahisi zilizotolewa wakati wa makadirio ya idadi kwa ajili kupanga mahitaji. Kulikuwa na mfumo usiojitosheleza wa kuhakikisha pembejeo zinasambazwa

kwa wakulima kwa wakati. Mfumo wa usambazaji ulikuwa na mapufungufu yaliyooonekana kwenye maeneo ya muda wa usambazaji, ubora, na udhibiti wa bei ambayo inaathiri ufanisi wa mfumo.

Kwa ujumla, udhaifu huu una uwezekano mkubwa wa kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo na kupelekea uhaba wa chakula pamoja na kushuka kwa kipato cha mkulima pamojammoja na nchi kwa ujumla.

### 9.3.2 Udhibiti usiojitosheleza wa ubora wa pembejeo za kilimo

Wizara bado haijadhibiti kikamilifu usambazaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo ili kuhakikisha wakulima wanatumia viuwatilifu bora, mbegu bora, na mbolea. Kulikuwa na mfumo usiojitosheleza wa kuhakikisha pembejeo za kilimo zinapatikana kwa wakulima na zinakidhi viwango vinavyohitajika. Wakulima nchini walitumia pembejeo ambazo zilikuwa ama na ubora wa chini, bandia, au chini ya kiwango kutokana na mfumo usiojitosheleza wa kuhakikisha pembejeo zenye ubora mzuri zinapatikana kwa wakulima.

Kulikuwa na upungufu katika ukaguzi ulizofanywa kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo mipakani ili kudhibiti ubora wa pembejeo zinazoingizwa na kuuzwa nchini. Hapakuwa na mpango na mwongozo ulioanzishwa wa ukaguzi. Badala yake, wakaguzi walitumia fomu za ukaguzi tofautitofauti na ambazo ziliathiri ubora wa ukaguzi uliofanyika na hivyo kushindwa kutambua mapungufu ya ukaguzi. Hali hii iliathiri bidhaa za kilimo katika masoko ya ndani na nje ambayo inaweza kupelekea athari mbaya kwenye uchumi wa taifa.

### 9.3.3 Usimamizi usiojitosheleza katika visumbufu vya mimea na milipuko ya magonjwa

Kutokana na ukaguzi huu, ninahitimisha kwamba kuna utekelezaji usiojitosheleza wa mikakati ya kinga na udhibiti japokuwa kulikuwa na taarifa za mara kwa mara za milipuko ya visumbufu vya mimea na magonjwa. Kulikuwa na ushirikiano usio imara kati ya watendaji muhimu. Ufuatiliaji na tathimini haukufanyika ipasavyo. Hii ilipelekea mwendelezo wa matukio ya milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea katika maeneo mengi nchini. Hivyo, kuna hatari ya kuwa na uhaba wa chakula na kupungua kwa kipato kwa wakulima kutokana na uzalishaji duni wa mazao. Matokeo yake mchango wa kilimo katika uchumi wa taifa utaporomoka.

### 9.3.4 Usimamizi usiojitosheleza kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

Serikali imewekeza sana kwenye miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na uhakika wa chakula. Mapitio ya miradi yamebaini kuwa asilimia 76 ya miradi yote iliyotekelezwa ilichelewa;

wakati miradi mingi ilitekelezwa chini ya kiwango kilichokubaliwa katika mwonekano na ubora wa usanifu. Kulikuwa na mapungufu katika shughuli za awali na shughuli za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Usimamizi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji haukujitosheleza kwani miradi mingi iliyojengwa haikuwa kwenye viwango vya ubora na haikujengwa kwa gharama zilizokubailiwa awali; na haikukamilika kwa muda uliopangwa. Kwa sababu hiyo, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji haifanyi vizuri kwa kuwa baadhi ya skimu za umwagiliaji zilijengwa maeneo ambayo hayakuwa na kiasi cha kutosha cha maji ili kuyafikia maeneo ya umwagiliaji. Skimu nyingi hazina uhalisia kwani baadhi yake zina miundombinu ambayo haijakamilika na ziko kwenye hatari ya kukumbwa na athari za mabadiliko ya kimazingira.

Mapungufu haya ni matokeo ya kutofanyika kwa upembuzi yakinifu unaohusisha Tume ya taifa ya Umwagiliaji na wadau wengine na hivyo kusababisha ujenzi wa miundombinu isiyofanya kazi vizuri na isiyo endelevu. Utoaji pungufu wa fedha wa serikali kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili kufadhili usimamizi wa shughuli za umwagiliaji umechangia kwenye ufanyaji kazi hafifu wa miradi mingi ya umwagiliji nchini. Uzalishaji wa mazao nchini upo kwenye hatari kwani miundombinu mingi iliyopo haitaweza kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji kwa wakulima, kwa sababu ya umuhimu wa umwagiliaji uliopo ili kuimarisha uhakika wa chakula.

### 9.3.5 Usimamizi usiojitosheleza wa utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima

Ukaguzi ulihitimisha kwamba, usimamizi wa utoaji wa huduma za ugani nchini haujatekelezwa ipasavyo na wizara husika. Raslimali zilizoelekezwa kwa utoaji wa huduma hizi za ugani hazikutumiwa vizuri. Ingawa kulikuwepo na ukusanyaji wa raslimali-fedha, ukusanyaji wa raslimali-watu haukufanyika katika kiwango cha kuridhisha na hivyo kupelekea kuathirika kwa matumizi ya raslimali ili kukidhi malengo yaliyowekwa katika utoaji wa huduma za ugani.

Utoaji wa huduma za ugani katika kiwango cha mashambani hazijawa toshelevu ikilinganishwa na mafanikio ya matokeo ya shughuli zilizotekelezwa. Utoaji wa huduma za ugani zimeendelea kukumbwa na changamoto za kurithi, hususani kwenye mabadiliko katika mbinu za kilimo kwenda kwenye njia za mbinu za kilimo cha kisasa. Changamoto hizi zimeendelea kuathiri matokeo ya huduma za ugani zilizotolewa kwa wakulima.

### 9.3.6 Huduma saidizi hazijajitosheleza kwenye kuchangia wa ukuaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati

Ukuaji wa wasindikaji wa mazao ya kilimo nchini hazijawezesha kikamilifu uchangiaji wa uchumi wa nchi kwa kiwango kinachoweza kupelekea nchi kuwa nchi ya viwanda vya kati kufikia mwaka 2025. Wasindikaji wa mazao ya kilimo wamekuwa wakiporomoka zaidi badala kukua, ambapo sekta imekuwa na wajarisiriamali wapya wasiokuwa na uzoefu kwenda sambamba na mabadiliko ya viwanda. Kwa miaka ya fedha 2014/15 na 2015/16 mchango wa wasindikaji wa mazao ya kilimo kwenye ajira ulikuwa chini sana kwani mchango wa wajasiriamali wadogo ulikuwa asilimia 20 na wa kati asilimia 40 ambayo ni ndogo sana ikilinganishwa na malengo ya asilimia 60 yaliyowekwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Huduma za usaidizi wanazopewa wasindikaji wa mazao ya kilimo bado hazijachangia kwenye ukuaji wao. Wasindikaji wa mazao ya kilimo wamekumbwa na changamoto zinazozuia ukuaji wao japokuwa wamepewa huduma saidizi kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo ambazo zilikuwa na ukomo wa kufikia huduma saidizi kwenye teknolojia, masoko, fedha, na mafunzo ya biashara.

Huduma za masoko zilizotolewa kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo zimefanyika zaidi kwenye maonesho ambayo hayawapi fursa nzuri wasindikaji wa mazao ya kilimo kuweza kuhudhuria. Mafunzo yatolewayo kwa wasindikaji hayana ufanisi kwani ni asilimia 9 tu ya wajasiriamali wadogo hupewa mafunzo. Mahitaji ya sasa ya teknolojia kwa maendeleo endelevu hayajakidhi mahitaji ya sasa ya wasindikaji kwa sababu ya kiwango cha sasa kilichopo kwenye masoko kuwa kimeendelea kuliko tekinolojia za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

# SURA YA KUMI

# MAPENDEKEZO

## 10.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mapendekezo yanayotokana na uchambuzi wa ripoti sita za ukaguzi wa ufanisi pamoja na ripoti moja ya ufuatiliaji. Uchambuzi umeonesha kuwa kulikuwa na maeneo mengi muhimu yaliyohitaji maboresho zaidi kwa ajili ya maendeleo ya kilimo. Maeneo haya muhimu kwa maendeleo ya kilimo ni: upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo; udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo; udhibiti wa visumbufu vya mimea na milipuko ya magonjwa; utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima; usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; na utoaji wa huduma saidizi kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo.

Sura hii inatoa mapendekezo kwa Wizara ya Kilimo kuhusu nini cha kufanya ili kutatua changamoto zilizoonekana ili kuboresha mipango, utekelezaji, usimamizi, na tathimini ya shughuli za kilimo nchini.

## 10.2 Mapendekezo Maalumu kwa Wizara ya Kilimo

Wizara ya Kilimo inapaswa:

1) Ihuishe taarifa zake na kuboresha hatua zilizopo za usajili, ukaguzi, na mafunzo kwa mawakala wa pembejeo na wakulima ikiwa njia ya kudhibiti ubora kwenye viuwatilifu, mbegu, na mbolea ili kujihakikishia uwepo wa pembejeo zenye ubora katika soko;

2) Iweke mfumo utakaohakikisha kuwa mikakati ya kudhibiti na kuzuia milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea inafanywa ya kisasa ili kuhamasisha ubora wa mazao ya kilimo na hivyo kupunguza kiwango cha vihatarishi vya chakula na kuimarisha ubora wa mazao katika soko la kimataifa;

3) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara iimarishe uwezo wake katika kutoa huduma saidizi kwa nyanja zote za wasindikaji ili kuhamasisha uongezaji wa thamani katika mazao ya kilimo na hivyo kuiwezesha nchi kuwa ya uchumi wa kati wa viwanda;

4) Iimarishe namna ya kuwasaidia wazalishaji wa ndani ya nchi wa mbegu, viuwatilifu, na mbolea ili kuhamasisha uzalishaji wa pembejeo za kilimo ndani ya nchi na hivyo kutoa uhakikisho wa kupatikana kwa pembejeo kwa wakati;

5) Ihakikishe kwamba programu za kuwaendeleza maofisa ugani zinaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji yao na zinatekelezwa kikamilifu zikiwa na malengo ya kuwapatia uwezo wa kutoa huduma za ugani kwa wakulima ikiwa ni pamoja na ujuzi na maarifa mapya kuhusu mbinu na teknolojia za kisasa za kilimo;

6) Ipitie mnyororo wake wa maagizo ili kuhakikisha kwamba hatua zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma za ugani katika mamlaka za serikali za mitaa zinatekelezwa katika namna itakayoleta matokeo;

7) Ihakikishe kwamba michoro ya miradi ya umwagiliaji inapitiwa ili kuthibitisha kutekelezeka na tija yake kabla ya kuanza shughuli za ujenzi;

8) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhakikisha kwamba Shirika la Viwanda Vidogo linakuwa mfumo wenye ufanisi wa kupata na kusambaza aina tofauti za teknolojia za gharama nafuu kwa wasindikaji ikiwemo kufanya uhandisi nakili ili kuimarisha uongezaji thamani kwa mazao ya kilimo;

9) Kuhakikisha kwamba Wakala wa Mbegu Bora za Mazao ya Kilimo unaimarisha namna ya uratibu kwa kuhakikisha kunakuwepo na hadidu za rejea kati yake na wakaguzi walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba wanafanya shughuli za ukaguzi na uhakiki wa mbegu bora za mazao katika mamlaka zao husika;

10) Kuhakikisha kwamba Wakala wa Mbolea nchini unafanya majaribio ya udongo nchi nzima ili kuongoza uandaaji wa mahitaji na usambazaji wa mbolea sehemu mbalimbali nchini kulingana na aina ya udongo na virutubisho vilivyomo;

11) Kuhakikisha kwamba Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaungana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuandaa namna ya kupitisha na kuisimamia miradi ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji kulingana na matakwa ya Sheria ya Umwagiliaji nchini; na

12) Kuhakikisha kwamba Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika Ukanda wa Kitropiki inazipitia na kuziboresha hatua zilizopo kwa sasa katika usajili wa viuatilifu na wauzaji wa viuatilifu ili kuongeza wigo na aina ya viuatilifu vilivyosajiliwa ili kukidhi mahitaji yake nchini.